# Nipashe

Jumamosi Machi 23, 2019 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0579873

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper



## Chadema yapinga kortini Sheria Vyama vya Siasa

UKURASA 3




UKURASA 13

# Waziri afuma simu, mihadarati gerezani

**ATAKA** maofisa wanne wasimamishwe kazi, aagiza kuundwa tume, mkuu wake akalia kuti kavu...*Endelea ukurasa wa 2*



Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani, Hamad Masauni. Kamishna Jenerali wa Magereza, Phaustine Kasike.

## YALIYOMO

**UKURASA WA 2**

**RC MAKONDA AWAWEKA KITIMOTO WAKURUGENZI WA MANISPAA MBILI DAR**

MKUU wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda, ametoa siku ...

**UKURASA WA 4**

**WAZIRI AIBANA NHIF MALIPO YA HOSPITALI**

WAZIRI wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, ameuagiza Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), kulipa...

## Tatizo nyonga tishio kiafya

UKURASA 3

## Nyuki wazua kizaazaa shuleni

UKURASA 2

**MICHEZO** SAMATTA ASEMA HAKUNA 'KUFELI' UK. 32

**MAONI, KATUNI UK.6**



Spika wa Bunge, Job Ndugai (kushoto), akizungumza na Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania, Prof. Florens Luoga (katikati), alipomtembelea ofisini kwake, Bungeni jijini Dodoma jana. Kulia ni Kaimu Mkurugenzi wa Benki Kuu ya Tanzania Tawi la Dodoma, Harry Mwansembo. **PICHA: OFISI YA BUNGE**

# Waziri afuma simu, mihadarati gerezani

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

NAIBU Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Masauni, amebaini kuingizwa kwa simu na dawa za kulevya ndani ya Gereza la Ruanda mkoani Mbeya kwa ushirikiano kati ya askari na wafungwa.

Kutokana na hali hiyo, amemwagiza Kamishna Jenerali wa Magereza, Phaustine Kasike, kuwasimamisha kazi askari wanne wa Gereza la Ruanda jijini Mbeya kwa tuhuma za kushirikiana na wafungwa kuingiza simu na dawa za kulevya.

Masauni alitoa agizo hilo jana, alipokuwa anazungumza na waandishi wa habari katika Ofisi ya Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, huku akisema alibaini ukiukwaji mkubwa wa sheria na maadili ya magereza kwenye gereza hilo.

Alisema alibaini wafungwa wanamiliki simu tisa na dawa za kulevya aina ya bangi ndani ya gereza na kwamba vyote vilikuwa vimeingizwa kwa ushirikiano kati ya askari wasiokuwa waaminifu na wafungwa.

Aliwataja askari hao wanaotakiwa kusimamishwa kazi kuwa ni Inspekta Longino Mwemezi, Ramadhan Mhagama, Alexander Mwinjano na Benjamini Malango ambao wote ni masajini taji wa Magereza.

Alisema baada ya kuzinasa simu hizo alizikabidhi kwa Jeshi la Polisi kwa ajili ya uchunguzi na kwamba taarifa za awali zilionyesha kuwa simu hizo zilikuwa zinatumika kwenye vitendo vya uhalifu ikiwamo rushwa.

"Namwagiza pia Kamishna Generali wa Magereza kuunda tume ya kuchunguza vitendo hivyo, ili kubaini mtandao mzima uliokuwa unahusika na wakibainika wengine hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yao," alisema Masauni.

Alisema vitendo vya aina hiyo vilishakemewa na Rais John Magufuli na aliagiza vidhibitiwe ndani ya magereza yote nchini ili kuepusha madhara yanayoweza kutokea.

Alisisitiza kuwa vitendo hivyo ni hatari kwa usalama wa magereza endapo askari wataendelea kutokuwa waaminifu kwa kuruhusu viendelee kufanyika ndani ya magereza.

Naibu Waziri Masauni aliwataka wakuu wa magereza yote nchini kuwa makini kwa kuzuia vitendo hivyo vya ukiukwaji wa sheria na maadili ili kulinda usalama wa maeneo hayo ambayo ni hatarishi.

Masauni alifanya ziara ya siku mbili mkoani Mbeya. Mbali na kutembelea gereza la Ruanda na kuzungumza na wafungwa, pia alitembelea Gereza la Kilimo la Songwe kwa ajili ya kukagua utekelezaji wa agizo la serikali la wafungwa kutumika kwenye uzalishaji.

## RC Makonda awaweka kitimoto wakurugenzi wa manispaa mbili Dar

**Na Romana Mallya**

MKUU wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda, ametoa siku tano kwa Mkurugenzi wa Manispaa ya Kinondoni kuhakikisha mkataba wa uendelezwaji wa Ufukwe wa Coco unasainiwa na unaanza mara moja.

Makonda alitoa agizo hilo jana, jijini Dar es Salaam, baada ya kukutana na wakuu wa wilaya na watendaji kujadili miradi ambayo haijafikiwa malengo.

Akizungumza kwenye mkutano huo, Makonda alimtaka Mkurugenzi wa Manispaa ya Kinondoni ahakikishe ndani ya siku tano awe ametia saini mkataba wa uendelezwaji wa ufukwe wa Coco na utekelezaji uanze.

"Ndani ya siku tano Mkurugenzi wa Kinondoni ninamwagiza awe ametia saini mkataba wa uendelezwaji wa ufukwe wa Coco na uanze mara moja," alisema.

Makonda alitaja mradi mwingine kuwa ni wa machinjio ya Vingunguti ambao amempa siku tatu Mkurugenzi wa Manispaa ya Ilala awe ametia saini mkataba wake.

"Zipo fedha zilizotengwa kwa ajili ya maendeleo ya wananchi ikiwamo machinjio ya Vingunguti na uendeshaji wa ufukwe wa Coco," alisema.

Alisema fedha hizo zilitolewa na Rais John Magufuli kwa ajili ya maendeleo ya wananchi na zipo kwenye akaunti, lakini manispaa husika hazijafanya utekelezaji.

# Nyuki wavamia shule, wajeruhi mwanafunzi

**Na Mwandishi Wetu,** MOROGORO

TAHARUKI imezuka katika Shule ya Msingi Kikundi, Manispaa ya Morogoro, baada ya nyuki kuvamia ghafla shuleni hapo na kumshambulia hadi kumjeruhi vibaya mwanafunzi mmoja wa darasa la kwanza.

Mwanafunzi aliyejeruhiwa ni Junior Benedict (11) na nyuki hao walisababisha masomo kusitishwa kwa muda na walimu kufunga ofisi wakihofia usalama wao.

Tukio hilo lilitokea jana mchana shuleni hapo na kuzua hali ya wasiwasi kwa walimu na wanafunzi kukimbia huku na kule wakijaribu kukwepa nyuki hao waliomvamia mwanafunzi huyo na kumng'ata maeneo ya kichwani na usoni.

Baadhi ya mashuhuda wa tukio hilo, Hussein Said na Rehema Ally, walidai mwanafunzi huyo aliokolewa na mwendesha bodaboda aliyekuwa akipita jirani, baada ya walimu na wanafunzi wenzake kukimbia kuwakwepa nyuki hao.

Jitihada za mwalimu mmoja kujaribu kumfunika kwa kanga ili kumnusuru hazikusaidia, lakini mwendesha bodaboda alivaa kofia ngumu na kumfunika mtoto huyo, huku akimburuza umbali kidogo kumkwepesha nyuki hao wasizidi kumshambulia na kufanikiwa kumwokoa.

Wazazi na walezi wenye wanafunzi wanaosoma shuleni hapo, walifika na kuulaumu uongozi wa shule kwa kushindwa kuchukua hatua kuwaondoa nyuki hao waliomshambulia vibaya mwanafunzi huyo na kuvimba zaidi maeneo ya usoni na kichwani.

Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Morogoro, Dk. Ritta Lyamuya, alikiri hospitali hiyo kumpokea mwanafunzi huyo ambaye amelazwa wadi namba nne akipatiwa matibabu.

Jitihada za kumpata mwalimu mkuu wa shule hiyo kutoa ufafanuzi zaidi wa tukio hilo, hazikuzaa matunda, lakini Ofisa Elimu Msingi wa Manispaa ya Morogoro, Abdul Buheti, akizungumza kwa njia ya simu, alikiri tukio hilo kufikishwa ofisini kwake.

Buheti alisema tayari wameshawasiliana na ofisa nyuki na kuripoti tatizo hilo ili kuwaondoa wadudu hao na kuruhusu masomo kuendelea kwa wanafunzi.

# HABARI ZA KITAIFA

## Trafiki waliopiga dereva na abiria waachiwa huru

**Na Romana Mallya**

ASKARI wawili wa Kikosi cha Usalama Barabarani, Kanda Maalum ya Dar es Salaam, waliokuwa wakishikiliwa kwa kutoa lugha ya matusi na kuwapiga watu waliokuwa kwenye gari wameachiwa huru.

Askari hao ni wale ambao siku nne zilizopita walionekana kupitia video iliyosambaa katika mitandao ya kijamii wakiwashambulia watu waliokuwa kwenye gari na kuwatolea lugha ya matusi. Baada ya kusambaa kwa video hiyo, Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Masauni, aliagiza askari hao wakamatwe na kuchukuliwa hatua za kisheria.

Jana, Kamanda wa Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Lazaro Mambosasa, alipoulizwa hatua zaidi zilizochukuliwa baada ya askari hao kuwekwa ndani, alisema wameshaachiwa.

"Wameachiwa hayo ni makosa ya kawaida kwa hiyo wamepewa adhabu na kuachiwa. Hawajapelekwa mahakamani, kwani kila kosa ni la kupeleka mahakamani? Mengine ni ya adhabu wamepewa adhabu," alisema.

**ALICHOSEMA MASAUNI**

Akizungumza na waandishi siku hiyo, Naibu Waziri Masauni alisema kitendo kilichofanywa na askari wake hakikubaliki ndiyo maana wamewachukulia hatua dhidi yao.

"Hao (askari) wako kituo cha Kanda Maalumu ya Dar es Salaam wakisubiri kuchukuliwa hatua," alisema. Masauni alisema kumekuwa na malalamiko mengi ya madereva kubambikwa makosa au askari kufanya vitendo vilivyo kinyume cha mwenendo mwema wa jeshi hilo, na walipoona tukio hilo, walichukulia hatua dhidi ya askari hao mara moja.

Aidha, aliwataka wananchi wanapoona kuna vitendo ambavyo wanafanyiwa kinyume cha sheria wasisite kutoa taarifa.

"Ikitokea uongozi wa askari unatetea au kutochukua hatua muafaka, mlalamikaji apande uongozi wa juu hata kwa waziri na naibu wake ili hatua zichukuliwe," alisema Masauni.

Alisema vitendo vinavyolalamikiwa na wananchi dhidi ya Jeshi la Polisi ni pamoja na askari wake kupokea rushwa, lugha chafu kwa madereva na kuwashambulia.

Masauni alisisitiza kuwa ikitokea uongozi jeshi hilo unatetea au kutochukua hatua stahiki, mlalamikaji awataarifu viongozi wa juu wa wizara.

"Ninawaasa askari wote kuwa serikali iko makini na haitaruhusu mwananchi yeyote aonewe na vyombo vya dola. Pia hatutaruhusu mwananchi au taasisi yoyote imuonee askari kwa sababu yoyote ile," Masauni alisema.



Wafanyakazi wa kampuni ya ujenzi ya CCECC, wakiendelea na ujenzi wa vituo vya mabasi katika Barabara ya Mlandizi inayoanzia Sinza Kijiweni hadi Tandale kwa Mtogole, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: HALIMA KAMBI**

# Chadema kupinga kortini Sheria ya Vyama vya Siasa

**Na Romana Mallya**

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), kimesema nia na dhamira ya kupinga Sheria mpya ya Vyama vya Siasa mahakamani iko pale pale.

Katika taarifa yake kwa vyombo vya habari jana, Mkurugenzi wa Itikadi, Mawasiliano na Mambo ya Nje wa Chadema, John Mrema, alisema wanashauriana na vyama vingine vya siasa na wadau ili kuona njia nzuri zaidi ya kufungua shauri hilo mahakamani.

"Nia na dhamira hiyo iko palepale na tunaendelea kushauriana na vyama vingine vya siasa na wadau mbalimbali njia nzuri zaidi ya kufungua shauri mahakamani mapema iwezekanavyo," alisema.

Katika taarifa hiyo, Chadema imeainisha vifungu 11 vilivyopo kwenye sheria hiyo mpya, huku wakielezea kuwa kila kimoja kimeweka adhabu na faini.

"Sheria hii ni mbaya kutokana na vifungu vyake ama kukiuka Katiba na misingi ya utawala bora pamoja na mikataba mbalimbali ya kimataifa ambayo Tanzania tumetia saini," alisema Mrema.

Mrema aliviainisha vifungu hivyo kuwa ni pamoja na kifungu cha 3 (b), kifungu cha 3 (g), kifungu cha 5A (i), kifungu cha 5B, kifungu cha 6B (d), kifungu cha 8C (2), kifungu cha 8D (2), kifungu cha 8E, kifungu cha 11A (2), kifungu cha 23(7) na kifungu cha 21E.

Januari 29, mwaka huu, Bunge lilipitisha Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Vyama vya Siasa wa Mwaka 2018, katikati ya msuguano mkali kati ya wabunge wa vyama vya upinzani na wale wa chama tawala.

Muswada huo uliwasilishwa bungeni Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Vijana, Ajira na Watu wenye Ulemavu), Jenister Mhagama, na baadaye mjadala kuanza, huku wabunge wote wa upinzani wakiupinga na Kamati ya Bunge ya Katiba na Sheria, ikipinga baadhi ya vifungu.

Baada ya mvutano mkali, Bunge liliketi kama kamati na ndipo Mwenyekiti wake, Spika wa Bunge, Job Ndugai, aliongoza wabunge kupitia kifungu kwa kifungu na baadaye alisema "Muswada umepita na kilichobaki sasa ni kuupeleka kwa mheshimiwa Rais ili autie saini uwe sheria."

Muswada huo ulipitishwa huku taasisi mbalimbali zikiwa zimetoa maoni yake na kupendekeza kufanyika marekebisho makubwa, jambo ambalo kwa kiwango kikubwa mapendekezo hayo hayakufanyiwa kazi.

Mathalani, muswada uliweka vifungu vinavyolimbikiza mamlaka na madaraka kwa msajili wa vyama, ikiwamo kinga ya kutoshtakiwa mahakamani.

Baadhi ya wadau waliofika mbele ya Kamati ya Bunge ya Katiba na Sheria, walipinga susala hilo kwa maelezo kuwa haiwezekani kwa msajili kujiwekea kinga, wakati yeye amebeba roho za umma; na kwamba pendekezo hilo "linamfanya Msajili kuwa Mungu mtu."

# Tatizo la nyonga sasa janga kiafya

**Na Beatrice Shayo**

DAKTARI Bingwa wa mifupa, viuno na kikombe cha kiuno katika Taasisi ya Tiba ya Mifupa Muhimbili (MOI), Edmund Ndalama, amesema tatizo la watu kuvunjika viuno ni kubwa na kwa siku wanawatibu wagonjwa watano.

Aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam, wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu kongamano kwa ajili ya kupeana uzoefu na wataalamu kutoka India.

Dk. Ndalama alisema kwa mwezi wanatibu wastani wa wagonjwa 20, idadi ambayo ni kubwa ikilinganishwa na nchi zingine.

"Tatizo la kuvunjika kiuno ni kubwa sana na inasababishwa na ajali. Mtu kuanguka au mtu akiwa katika shughuli zake za kawaida bahati mbaya anakuwa anakandamizwa yaani kitu kimoja anatembea, kingine kinamkandamiza na anavunjika kiuno," Dk. Ndalama alisema.

Alisema kuna aina 10 za mivunjiko na kwamba zisipotibiwa mgonjwa atalazimika kwenda kuwekewa kiungo cha bandia.

"Sehemu ya kiuno ni kitu kilichoachwa yaani imesahaulika inahitajika kupewa kipaumbele zaidi unapopata maumivu katika nyonga unaweza ukawa

INAENDELEA UK. 8


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA YA HAKIMU MKAZI KIVUKONI
KIONDONI/KIVUKONI
SHAURI LA MAPITIO JINAI NO 05 YA 2018
IDD BASHIRY.......................MWOMBAJI/MLETA MAOMBI
DHIDI YA
SAID KANYANI..................................................MJIBU MAOMBI

Kwa
Said Kanyani
Dar es salaam.

KUITWA SHAURINI

Kwa kuwa mleta maombi ameleta maombi yake ambayo yanaelezwa katika nakala ya maombi ambayo zinaweza kupatikana Mahakama Hi,Kwa hiyo unahitajika kuhudhuria katika Mhakama Hi binafsi aua kwa Wakili au mwakilishi ambaye ananuhusiwa siku ya **JUMANNE** Tarehe **26** Mwezi **03** 2019 saa 8:30 asubuhi.

Kwa mujibu wa maombi haya na kwa siku hiyo ni siku ya kutaja shauri hilo ni lazima ulete hati zote zinazohusu shauri hilo kwa ajili ya kujitetea katika shauri hilo.

ANGALIZO

Kama hukuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu na Mahakama ikithibitisha kama umepokea wito wa kuitwa shaurini itaweza kutoa hukumu kama umeshindwa.

Hati hii imetolewa kwa Amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo tarehe 28 mwezi 2 2019.

...................................
HAKIMU MKAZI MAHAKAMA YA WILAYA
KINONDONI

215133702

## Wanahabari wafundwa matumizi ya utafiti

**Na Enock Charles**

WAANDISHI wa habari wametakiwa kutumia matokeo ya utafiti wa kitaalamu kutoa taarifa zitakazosaidia kuleta mabadiliko katika jamii.

Mkurugenzi wa Utafiti wa Kimkakati wa Taasisi ya Utafiti wa Kuondoa Umaskini (Repoa), Dk. Jamal Msami, alisema hayo jana kwenye mjadala wa ukuaji wa uchumi wa ndani uliondaliwa na taasisi hiyo.

Alisema ili kupata maendeleo ya uchumi wa ndani ni muhimu kutumia utafiti uliopo ili kuchochea mabadiliko ya kiuchumi kwa kuwianisha utafiti huo na hali halisi za wananchi lengo hasa likiwa ni kuibua fursa zilizopo.

"Limekuwa suala la kawaida tunapozungumza au mwanataaluma anaposema uchumi umekua kunatokea miguno na watu kushindwa kuelewa kuwa uchumi unakua kwa maana kipato chake mfukoni au wananchi wote kwa ujumla," Dk. Jamal alisema.

Dk. Jamal pia alisema ni muhimu pawapo mfumo rasmi wa kuwasaidia wananchi wa kawaida kwa kuwa wamekuwa wakikutana na changamoto mbalimbali katika shughuli za uzalishaji mali hali inayosababisha kutokupata thamani halisi ya uzalishaji wao na kutotambua fursa zitakazowasaidia kiuchumi.

"Unakuta mkulima analima, halafu anahangaika anatafuta soko bila kujua atakutana na nani sokoni ndiyo maana wengine wanaamua kuwatumia madalali ingawa pia huo si mfumo rasmi," alisema.

Naye Mhariri Mtendaji Mkuu wa Mwananchi Communications Limited, Bakari Machumu, alisema utafiti ni muhimu kwa kuwa unasaidia kulijua tatizo, hivyo kutafuta majawabu sahihi na hatimaye kuhakikisha Watanzania hasa wa hali ya chini wanapata fursa za kiuchumi katika nchi yao.

"No research no right to speak (hakuna haki ya kuzungumza bila utafiti). Utafiti unatusaidia kujua tatizo na kupata majawabu sahihi kulingana na tatizo husika," alisema Machumu.

Mkurugenzi wa Utafiti wa Repoa, Dk. Blandina Kilama, alisema wananchi wa kawaida wana uelewa tofauti kuhusiana na umaskini, hivyo ni muhimu kuangalia viashiria na vigezo mbalimbali katika kutathmini hali ya uchumi nchini.

"Tulipomuuliza baba mmoja kuhusu uelewa wake kuhusu umaskini, alisema kwetu sisi mtu yeyote anayeshindwa kumpeleka mtoto wake shule binafsi ni maskini. Hapo ni Kilimanjaro. Huko Kakonko mtu mmoja alisema mimi si maskini kwa sababu nina uwezo wa kula milo miwili kwa siku kwa hiyo sisi kama wachambuzi tunaongeza na zile standards (viwango) nyingine tunazozijua ," alisema.




Naibu Waziri wa Maji, Jumaa Aweso, akizungumza na waandishi wa habari wakati wa kilele cha Maadhimisho ya Wiki ya Maji, katika viwanja vya Mnazi Mmoja, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Waziri aibana NHIF malipo hospitali

**Na Romana Mallya**

WAZIRI wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, ameuagiza Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), kulipa madeni ya hospitali zinazotoa huduma za bima ndani ya mwezi mmoja.

Ummy alitoa agizo hilo jana, jijini Dar es Salaam, baada ya Ofisa Mtendaji Mkuu wa Hospitali ya CCBRT, Brenda Msangi, kusema hiyo ni changamoto wanayokutana nayo katika utoaji wa huduma kwenye jengo la huduma binafsi lililozinduliwa hospitalini hapo.

Mtendaji mkuu huyo alieleza changamoto hiyo wakati wa uzinduzi wa jengo la kutoa huduma binafsi za kibingwa kwa wagonjwa wa nje.

Msangi alisema miongoni mwa changamoto wanazokabiliana nazo kwenye utoaji wa huduma binafsi ni ongezeko la wagonjwa, hivyo mifuko ya bima ya afya, ukiwamo NHIF usipotoa malipo kwa wakati husababisha shida kwao.

Kutokana na changamoto hiyo, Waziri Ummy, wakati akizindua jengo hilo, alisema alishaielekeza NHIF kwamba kama mtu ameshatoa huduma kwa wateja, alipwe ndani ya mwezi mmoja.

"NHIF mpo hapa? Nataka ndani ya mwezi mmoja muwe mmewalipa watoa huduma kwa wanachama wenu. Kama mtu amefanya kazi mjitahidi mumlipe, maana mnajificha kwenye kivuli cha kuhakiki. Mnahakiki kitu gani kisichoisha?" Alihoji.

"Nanawaomba na nyie watoa huduma mpeleke madai yenu kwa wakati ili wayahakiki mapema," alisema.

Katika mkutano huo, Waziri Ummy alibaini kwamba tatizo hilo haliko kwa watoa huduma bali NHIF kutokana na CCBRT kueleza kuwa madai ya mwezi uliopita yameshapelekwa NHIF.

"Kumbe tatizo liko kwetu NHIF. Nawaelekeza tusiwe kikwazo cha huduma bora kwa sababu mtoa huduma anategemea hizi fedha kulipa mishahara, kununua vifaa, kulipa umeme na maji. Tunataka watu waone raha ya kuwa na NHIF, sitaki mwisho wa siku watoa huduma waseme hatuzipokei bima kwa sababu malipo hawayapati kwa wakati," alisisitiza.

Waziri Ummy pia aliwataka Watanzania waone umuhimu wa kuwa na bima kwa sababu ndiyo njia rahisi ya kupata huduma bila kikwazo cha fedha.

Alisema alikutana na kijana ambaye analipa fedha taslimu Sh. 50,000 ili kumwona daktari, gharama ambayo haihusishi vipimo na dawa.

"Nimemwambia NHIF kwa watu sita ni Sh. milioni 1.5, ukiigawa ni kama 250,000 kwa hiyo sisi tumeangalia mkiwa watu sita hawawezi kuumwa wote, kwa hiyo tunakamilisha utaratibu tuwe na bima ya afya ya mtu mmoja mmoja ili kila mtu ajipimie kifurushi chake," alisema.

Alisema ndani ya wiki tatu, serikali itatangaza vifurushi vya mtu mmoja mmoja ambavyo vitawezesha Watanzania kupata huduma bora za afya.

Kuhusu kliniki hiyo kwa wagonjwa wa nje, alisema hata hospitali za serikali wamezielekeza ziiweke ili kusaidia kujiendesha.

Pia alisema katika bajeti ya mwaka jana walihakikisha wanapunguza tozo kwenye vifaa tiba vinavyotolewa kwa msaada.

"Mamlaka ya Chakula na Dawa Tanzania (TFDA) nimeshawaelekeza kuwa wapunguze tozo kwenye vifaa tiba vinavyoletwa na kliniki binafsi na hospitali binafsi, kwa sababu hii si biashara. Tutatoa taarifa kabla ya mwezi mmoja kuonyesha ni tozo gani za kupunguza kwenye vifaa tiba, dawa na vitenganishi," alisema.

Wakati huo huo, Waziri Ummy alisema wagonjwa wa fistula wamepungua kwa sababu serikali imeviboresha vituo vya afya 350 ambavyo sasa vinatoa huduma bora za uzazi.

Pia alisema serikali imefanikiwa kupunguza vifo vya uzazi kwa asilimia 40 kuanzia mwaka 2012 hadi 2018.

Awali, Msangi alisema malengo ya kuanzisha huduma hiyo kwa wagonjwa wa nje ni kwa sababu hawataki kutegemea wafadhili.

"Ukija kutibiwa katika huduma hii ya binafsi ujue utaokoa maisha ya watu wengi ambao hawana uwezo," alisema.

Nesia Mahenge kutoka Shirika la Kuhudumia Watu wenye Ulemavu (CBM), aliiomba CCBRT ifike mikoa mingi Tanzania ili wagonjwa wasisafiri umbali mrefu kutafuta huduma.

# Uswisi yazijaza asasi mabilioni

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

UBALOZI wa Uswisi nchini kupitia Shirika la Maendeleo na Ushirikiano la Uswisi (SDC), umezindua awamu ya tatu ya programu kwa ajili ya kuziwezesha asasi za kiraia kuboresha uwajibikaji.

Uswisi ina nia ya kuchangia zaidi katika kuimarisha utendaji kazi na uwajibikaji wa mamlaka za umma ili zitoe huduma bora kwa wananchi. Hayo yalisemwa jana mjini Dodoma na Balozi wa Uswisi nchini, Florence Tingly, kwamba katika mpango huo SDC itachangia Sh. bilioni 18 kwa miaka minne ijayo kwa asasi kadhaa za kiraia ikiwa ni pamoja na Foundation for Civil Society (FCS), Policy Forum na Twaweza.

Alisema Ubalozi wa Uswisi unashirikiana na asasi hizo zinazohusika na uanzishwaji na usimamizi wa sera za maendeleo ili kuboresha maisha ya wananchi wa kawaida.

Pia alibainisha kuwa Uswisi inaamini kwamba asasi za kiraia ni moja ya wadau muhimu kwa nchi ya Tanzania ili kufikia malengo yake kwenye Dira ya Maendeleo ya Taifa ya 2025.

Alisema Uswisi tayari ina ushirikiano wa muda mrefu na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) katika kuimarisha uwezo wake wa uchunguzi.

Aliongeza kuwa pia inachangia mpango wa utawala bora wa fedha unaotekelezwa na Shirika la Ujerumani (GIZO na kwamba hiyo inafanya kazi ya kuzijengea uwezo na kutoa msaada wa kiufundi kwa Ofisi ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Serikali (CAG), Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani na halmashauri za wilaya.

## HABARI KITAIFA



Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu (kulia), akipata maelezo kuhusu mashine ya kutoa mionzi ya kutibu macho kutoka kwa Mkuu wa Kitengo cha Macho cha Hospitali ya CCBRT, Dk. Cyprian Ntomoka, baada ya kuzindua jengo jipya la kliniki binafsi ya hospitali hiyo, jijini Dar es Salaam jana. Kushoto ni Ofisa Mtendaji Mkuu wa CCBRT, Brenda Msangi. **PICHA: JOHN BADI**

# Wanaushirika tumbaku kujenga kiwanda

**Na Halima Ikunji,** UYUI

UMOJA wa Vyama Vikuu vya Ushirika wa Tumbaku (TCJE) umependekeza na kudhamiria kuanza ujenzi wa kiwanda cha kuchakata zao hilo mkoani Tabora na kujiwekea lengo la kupata Sh. milioni 700 hadi mwisho wa msimu wa kilimo wa mwaka huu.

Mwenyekiti wa TCJE, Emanuel Charahani, alisema jana kuwa wazo la kiwanda hicho limeshajadiliwa na wajumbe wa vyama vyote kutoka Kigoma, Kahama na Mpanda na kuafikiwa, sasa kilichobaki ni utekelezaji tu.

Alisema wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Chama Kikuu cha Ushirika wa Wakulima wa Tumbaku Kanda ya Magharibi (WETCU) kwa kauli mmoja, wameazimia kujengwa kwa kiwanda hicho wilayani Urambo.

Charahani alisema katika kikao hicho, wajumbe hao ambao wote ni wakulima wa zao hilo, walisema kiwanda hicho kitasaidia kuhamasisha kilimo bora cha tumbaku na kuongeza uzalishaji maradufu tofauti na hali ilivyo sasa.

Mwenyekiti huyo alisema vyama hivyo wamedhamiria kujenga kiwanda hicho ambacho kitaondoa urasimu wa makisio na kuongeza tija katika uzalishaji wa tumbaku na kutoa zaidi ya ajira 3,000 kila msimu wa kilimo.

Charahani alisema ili kufanikisha ujenzi huo, alishauri wenyeviti na mameneja wa vyama vikuu vya ushirika, wenyeviti na wakurugenzi wa halmashauri zinazolima tumbaku, mwakilishi wa Mkuu wa Mkoa na Mrajisi Ushirika wa Mkoa wakutane Aprili 15, mwaka huu katika ofisi za Bodi ya Tumbaku Tanzania ili kuunda kamati ya utekelezaji.

Alishauri kuanza mara moja kwa mchakato na upembuzi yakinifu, huku akiutaka uongozi wa WETCU kusimamia ipasavyo mchakato huo ili kuharakisha ujenzi.

Kwa mujibu wa Charahani, hizo ni juhudi za wakulima kuhakikisha wanaungana na wadau kuunga mkono jitihada za serikali ya awamu ya tano katika maendeleo ya viwanda.

Naye Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Uyui, Said Ntahondi, alisema ujenzi wa kiwanda hicho unasubiriwa kwa hamu kubwa na wakulima wa tumbaku nchini kutokana na umuhimu wake.

Alisema wazo la ujenzi wa kiwanda hicho limepata baraka za vyama vyote vikuu vya ushirika wa wakulima wa zao hilo katika mikoa yote na kila mkulima amekubali kuchangia Sh. Tisa kwa kila kilo atakazouza ili kufanikisha ujenzi huo.

Kwa kuchangia kiasi hicho katika msimu huu pekee, alisema wanatarajia kukusanya zaidi ya Sh. milioni 700 kwa ajili ya kazi hiyo na kwamba eneo la ujenzi wa kiwanda limeshapatikana.

Naibu Mrajis wa Vyama vya Ushirika nchini, Collins Nyakunga, aliutaka uongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Urambo kukaa meza moja na vyama vikuu vya ushirika vya Milambo na WETCU kabla ya kuanza ujenzi huo ili kuepusha migogoro ya ardhi.

# Wabunifu 3,000 kushindanishwa

**Na Elizabeth Zaya**

ZAIDI ya wabunifu 3,000 wanatarajia kushiriki katika wiki ya ubunifu mwaka huu, itakayoanza Machi 25 hadi 29 katika mikoa ya Dar es Salaam, Arusha na Iringa.

Wiki ya Ubunifu nchini imeandaliwa na Mfuko wa Ubunifu kwa Maendeleo ya Binadamu (HDIF) na Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (Costech), kwa ufadhili wa Uingereza.

Akizungumza juzi na waandishi wa habari kuhusu wiki hiyo jijini Dar es Salaam, Mkurugenzi Mkuu wa Costech, Dk. Amos Nungu, alisema tume kupitia Mfuko wa Taifa wa Uendeshaji wa Sayansi na Teknolojia (Mtusate), unaopata fedha serikalini na wadau wengine wakiwamo DHIF, walifungua dirisha kwa wabunifu mwaka 2017 ili kuendeleza ubunifu nchini.

"Wiki ya ubunifu mwaka huu, inabeba kaulimbiu ya kukuza na kuendeleza ubunifu kwa maendeleo ya watu, lengo ni kuhakikisha tunavitambua na kuendeleza vipaji na kazi zote za kibunifu," Dk. Nungu alisema na kuongeza:

"Na mwanzoni mwa mwezi huu, kwa kushirikiana na HDIF pamoja na Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Sweden (Sida), tulikabidhi Sh. bilioni 1.9 kwa wabunifu bora 32 na kumbi za ubunifu 15 zilizoshinda mashindano ya Costech mwaka 2018."

Dk. Nungu alisema tume kwa kushirikiana na taasisi zilizo chini ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, imeanzisha utaratibu wa kuwatambua wabunifu wote nchini kwa kuwaweka katika makundi kulingana na kiwango cha ubunifu wao.

INAENDELEA UK 8

# Walilia uhaba taulo za kike

**Na Steven William,** MUHEZA

WANAFUNZI wanaosoma katika shule za sekondari mkoa wa Tanga wamelalamikia kukosekana kwa taulo za kike, hivyo kufanya kuwa kero kwao katika kujisitiri wanapokuwa madarasani au katika shughuli zingine.

Hayo waliyasema juzi katika risala ya mtandao wa Tanga Fema Club Mentors, iliyosomwa na Mwanaisha Lissu mbele ya mgeni rasmi, Mkuu wa Wilaya ya Muheza, Mwanasha Tumbo, kwenye tamasha lililofanyika katika Shule ya Msingi ya Magila.

Alisema watoto wa kike katika shule nyingi za sekondari mkoa wa Tanga wanakosa taulo za kike, hivyo kuwafanya wawe katika mazingira magumu wakati wa masomo na shughuli zingine.

Lissu alisema kuwa klabu za Fema zina changamoto nyingi kama vile kukosa muda wa kutosha katika kufanya shughuli kwa ufanisi. Pia alisema zinakosa rasilimali fedha na mapokeo hasi kwa jamii kuhusu shughuli za mtandao huo.

Kuhusu mafanikio ya mtandao huo katika mkoa huo, alisema klabu zimekuwa zikishiriki kongamano

INAENDELEA UK 8



# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Mungu ibariki Stars, Mungu ibariki Tanzania

**DUA** na sala zote za Watanzania na hasa wapenda michezo kesho zitaelekezwa kukiombea kikosi cha Timu ya Soka ya Taifa maarufu Taifa Stars.

Kikosi hicho kinachoongozwa na Mnigeria, Emmanuel Amunike kesho kuanzia saa 12:00 jioni kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam, kinatarajiwa kuwakaribisha wapinzani wao Uganda (Cranes).

Taifa Stars na Uganda zitakutana katika mechi ya mwisho ya Kundi L ya kuwania tiketi ya kufuzu fainali zijazo za Kombe la Afrika (AFCON 2019) ambazo zitafanyika Juni huko Misri.

Katika mechi ya kesho, Taifa Stars inayoongozwa na Nahodha Mbwana Samatta inahitaji matokeo ya ushindi tu ili iweze kutimiza ndoto zake za kucheza fainali hizo zinazochezwa kila baada ya miaka miwili.

Mara ya mwisho Taifa Stars kushiriki fainali hizo ilikuwa ni mwaka 1980, na nahodha wa kikosi hicho alikuwa ni Leodegar Tenga, ambaye sasa ni Mwenyekiti wa Baraza la Michezo la Taifa (BMT), Mjumbe wa Kamati ya Utendaji ya Shirikisho la Soka Afrika (CAF) na rais wa zamani wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF).

Kikosi hicho kilichojaa wachezaji nyota wanaocheza nje ya Tanzania na hapa nyumbani, wote wako tayari kwa mchezo huo muhimu, lakini kinachohitajika ni kuendelea kuiombea timu yetu iweze kufanya kile ambacho wadau wa soka wanakisubiri. Nipashe inaungana na wadau hao kuiombea dua njema Taifa Stars kwa sababu kufanya vema kwa timu hiyo, inamaanisha jina la Tanzania litaendelea kutajwa katika medani mbalimbali za kimataifa.

Tunaamini kuwa hakuna kisichowezekana kwa Taifa Stars kupata ushindi katika mechi ya kesho na hatimaye kuwapa furaha Watanzania ambao kwa muda mrefu walikuwa watazamaji kwenye fainali hizo zinazofanyika chini ya usimamizi wa CAF.

Kama ilipokwenda Kampala Septemba mwaka jana iliweza kupata pointi moja, hali ya kuwa wenyeji wote waliamini watapata ushindi katika mchezo huo, basi kesho nyota wa Taifa Stars mnatakiwa kuongeza bidii na hatimaye kupata ushindi katika uwanja wa nyumbani.

Lakini ili nyota au askari wetu ambao tunatarajia wapeperushe vema bendera ya Tanzania, ni nafasi yetu kwa Wazalendo kujitokeza kwa wingi kwenda kwenye Uwanja wa Taifa ili kuwashangilia.

Ili timu iweze kufanya vema katika mechi yake yoyote, ni lazima iwe na kikosi kamili chenye wachezaji 12. Wachezaji 11 wanakuwa uwanjani na mchezaji wa 12 ni wewe shabiki ambaye unatakiwa kufika na kukaa jukwaani kuishangilia timu yako. Hakuna miujiza katika soka, ili Taifa Stars iweze kufanya vema katika mchezo wake wa kesho, sibudi kila mmoja wetu akatimiza jukumu lake na kuwa sehemu ya mafanikio ambayo yatapatikana baada ya kuifunga Uganda.

Hata hivyo, Nipashe linawakumbusha mashabiki wote kuhakikisha wanaingia kuishangilia timu yao kwa utulivu, bila kufanya vitendo vyovyote vya uhalifu au kuvunja amani.


Kwa kufanya hivyo, itaiweka Tanzania katika nafasi nzuri na kujiepusha na adhabu yoyote kutoka CAF au Fifa ambayo inasisitiza Fair Play katika mechi zote.

Nipashe linaendelea kuwakumbusha Watanzania kuiombea dua Taifa Stars ambayo inajukumu zito la kuhakikisha inashinda na kufuzu fainali hizo za mwaka huu wakati tayari wapinzani wao Uganda wameshafuzu na mchezo wa kesho wanakamilisha ratiba.

Mungu ibariki Taifa Stars, Mungu ibariki Tanzania. AFCON 2019 ni zamu yetu.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311.
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Barnabas Maro

## Simba tutoeni kimasomaso

**MAANA** ya 'kimasomaso' ni aibu, haya au tahayuri ambayo mtu ataka kuikwepa; tendo la kujiondoa katika haya; jitoa katika aibu. Hili ndilo Watanzania kwa ujumla wetu twapaswa kuiombea timu ya Simba katika mbio zake za Ligi ya Mabingwa Afrika.

"Mgema akisifiwa, tembo hulitia maji." Kwa kawaida mgema apewapo sifa kutokana na tembo lake, badala ya kutengeneza tembo zuri hulitia maji na kuliharibu. Ni methali ya kutumiwa kuwanasihi watu kutomsifu mtu sana asije kufura kichwa na kuharibika. Pia hutumiwa kwa mtu ambaye asifiwapo huishia kujivuna.

Hii ni maalumu kwa viongozi, wanachama, mashabiki na zaidi sana wachezaji wa Simba. Ni dhahiri kuwa Simba imefanya vizuri katika michuano ya kimataifa baada ya kuingia kwenye hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Timu zingine zilizoingia hatua hiyo ni TP Mazembe ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC), Esparance Sportive de Tunis ya Tunisia, ambayo imetwaa ubingwa nchi yao mara 28. Nyingine ni Wydad Athletic Club.

Esperance Sportive de Tunis ni timu pekee iliyomaliza mechi zake bila kupoteza mchezo wowote na kupata alama 14. Imetwaa taji la Ligi ya Mabingwa Afrika mara tatu na kuwa katika nafasi ya pili mara nne miaka ya 1999, 2000, 2010 na 2018.

Kwa ufupi, timu zote hizo zina uzoefu mkubwa kuliko Simba yetu. Kwa hiyo si timu za kubezwa kama idhaniwavyo na wengi. Kwa sababu hii, badala ya viongozi, wanachama na mashabiki wa Simba kujinasibu kuwa watapata ushindi kirahisi ni muhimu kuwajenga wachezaji kisaikolojia ili watambue timu watakazokutana nazo zina uzoefu zaidi katika mashindano hayo kuliko Simba yetu.

Wachezaji wanatakiwa kuwa makini na kutokuwa na uwoga kwa kuwa timu zote zina wachezaji 11 kila mmoja akiwa na miguu miwili kama walivyo Simba. Muhimu ni kuwa na nidhamu ya mchezo na kucheza kwa ari kwa kuwa hakuna kubwa lisiloshindwa, chambilecho wahenga.

Maneno haya hutumiwa kumhimiza mtu anayekabiliana na hali ngumu kuwa lazima atafanikiwa. Wachezaji wa Simba wanapaswa kutambua kuwa penye nia pana njia. Hii ni methali ya kuwakumbusha wachezaji wetu kuwa wakiwa na nia ya ushindi ni lazima watafanikiwa.

Wahenga walisema: "Simba mwenda pole (kimya) ndiye mla nyama." Maana yake Simba aendaye taratibu bila ya kujitambulisha ndiye awezaye kuwagwia (kuwakamata) wanyama bila shida. Hii ni methali ya kuwanasihi wachezaji wa Simba wawe na umakini na utaratibu katika uchezaji wao, wasipapie mambo na mwisho watafanikiwa, Inshallah (apendapo Mwenyezi Mungu)!

Kwanza nijitambulishe kwa wana Yanga wenzangu. Nilijiunga na Yanga tarehe 2 Desemba, 1966 na kupewa kadi ya kwanza yenye namba 447. Kadi zilipobadilishwa mwaka 1976, nikapewa kadi namba 01868 kisha kadi namba 0340 ya mwaka 1993 na ya sasa ni namba 007887 iliyotolewa mwaka 2008. Wakati wote nitakuwa mkweli kwa klabu yangu.

Ni ukweli usiopingika kuwa ingawa Yanga tumetwaa ubingwa mara nyingi zaidi kuliko timu zote zinazoshiriki Ligi Kuu, wakiwamo watani zetu, Simba, tumeshindwa kuiwakilisha vema Tanzania kwenye mechi za kimataifa ipasavyo. Simba wamekuwa mabingwa wa Tanzania mara chache lakini wamekuwa wakifanya vizuri kwenye mechi za kimataifa kuliko Yanga. Sasa ndiwo wanaoiwakilisha Tanzania kwenye michezo ya Afrika.

Simba ilikuwa timu ya kwanza Tanzania kucheza fainali ya Klabu Bingwa Afrika mwaka 1993 jijini Dar es Salaam na kufungwa mabao 2-0 mbele ya Rais wa awamu ya pili, Alhaj Ali Hassan Mwinyi kwenye Uwanja wa Taifa (siku hizi Uhuru) jijini Dar es Salaam.

Rais Mwinyi aliwaasa watazamaji waliojaa uwanja ule kuwa waache tofauti zao za kiitikadi na waishangilie Simba kwa kuwa ilikuwa inaiwakilisha Tanzania. Tukaombwa tuonyeshe uzalendo wetu.

Kweli ilikuwa hivyo hata pale Simba ilipofungwa bao la kwanza kwani uwanja ulikuwa kimya; lakini ilipofungwa la pili, uzalendo ukawashinda watazamaji wa upande ulee ... wakaimba "Uzalendo umetushinda ... uzalendo umetushinda ..." wakifurahia Simba kushindwa! Wageni wakaondoka na kombe lao na kutuacha Watanzania tukikodoa wakati wageni wakikabidhiwa kombe lao kwenye uwanja wetu. Ilikuwa fedheha iliyoje!

Baada ya hapo kulikuwa na maneno ya chini chini kuwa eti kuna fedha zilizotumika kuwapa baadhi ya wachezaji muhimu wa Simba ili timu ishindwe! Eti kuna tajiri wao fulani alifanya hivyo ili kuepuka kutoa mamilioni ya fedha alizowaahidi wachezaji kama wangeshinda! Kama kuna ukweli ama la, Allahu ya aalam (Mwenyezi Mungu ndiye mwenye kujua zaidi).

Leo Taifa Stars itapambana na Timu ya Taifa ya Uganda (The Cranes) kwenye uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam. Twende kwa wingi ili kuujaza Uwanja wa Taifa pomoni (katika hali ya kujaa au kwa wingi) tukiwa na mavazi yanayolandana na bendera ya taifa letu, mavuvuzela, ngoma na nyimbo za kuwatia mori (hima, ari na hamasa ya kutenda jambo) wachezaji wetu ili kuwakatisha tamaa Waganda.

**marobarnabas@yahoo.**




Mkuu wa Wilaya ya Nyang'hwal mkoani Geita, Hamim Gwiyama, akizungumza katika hafla ya makabidhiano ya vitanda na magodoro kwa Shule ya Sekondari ya Kakola, kulia kwake ni Meneja wa Benki ya NMB Kanda ya Ziwa, Abraham Augustino, msaada huo una thamani ya Sh. milioni 10. **PICHA NA NMB**

# Wapewa miezi mitatu kuondoka shambani

**Na Mwandishi Wetu**

NAIBU Waziri wa Maliasili na Utalii, Constantine Kanyasu, ametoa miezi mitatu kwa wananchi waliovamia na kuendesha shughuli za kibinadamu ndani ya shamba la miti Biharamulo kuondoka mara moja ifikapo mwishoni mwa Juni, mwaka huu.

Ametoa muda huo ili kuwapa nafasi wananchi hao waliolima mazao ikiwamo pamba na mahindi kuvuna kabla ya operesheni ya kuwaondoa iliyopangwa kufanywa mwanzoni mwa Julai, mwaka huu, itayoendeshwa na Wakala wa Huduma ya Misitu Tanzania ( TFS) kwa kushirikiana na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya hiyo.

Kanyasu alisema juzi kuwa operesheni hiyo haiwezi ikasubiri taarifa ya wizara tano inayoendelea kufanyiwa kazi kwa vile eneo hilo halihusiani na vijiji 366 vilivyokutwa ndani ya hifadhi.

Naibu Waziri Kanyasu alitoa agizo hilo wakati akizungumza na wananchi hao katika ziara yake ya kikazi ya siku moja ya kutembelea shamba la miti Biharamulo lililoko katika Wilaya ya Chato mkoani Geita.

Alisema haiwezekani wananchi hao wakaachwa kuendelea kuvamia maeneo ya shamba hilo kwa kisingizio cha kauli ya Rais John Magufuli kuhusiana na vijiji 366.

Aidha, Kanyasu aliwaonya wananchi ambao wameitafsiri visivyo kauli ya Rais aliyoitoa Januari 15, mwaka huu, kuhusu vijiji 366 vilivyokutwa ndani ya hifadhi mbalimbali nchini.

Alisema baada tu ya tamko hilo, baadhi ya wananchi hata wale waliokuwa wakiishi nje ya hifadhi katika maeneo mengi, wameendelea kuvamia maeneo ya hifadhi, huku wakijimilikishia maeneo makubwa wakidai kuhalalisha tamko la Rais.

Akizungumzia kuhusu taarifa inayoendelea kufanyiwa kazi na timu ya mawaziri na makatibu wakuu kutoka wizara tano, Kanyasu alisema hadi sasa zaidi ya vijiji 700 vimekutwa ndani ya hifadhi badala ya vile 366 alivyokuwa amevitaja Rais.

Kutokana na hali hiyo, Kanyasu alisema baadhi ya wavamizi wa hifadhi nchini wataendelea kutolewa pasipo kusubiri kukamilika kwa kazi inayoendelea kwa vile wengi wameendelea kuvamia maeneo ya hifadhi kwa kisingizio cha tamko la Rais, huku maeneo hayo yakizidi kuharibiwa kwa kukatwa miti pamoja na kuendesha shughuli nyingi za kibinadamu.

Katika hatua nyingine, Kanyasu ameiagiza Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) kutenga bajeti ya kugharamia operesheni ya kuwaondoa wavamizi ndani ya shamba hilo.

Alisema operesheni hizo zifanyike mara kwa mara ili wananchi wajue serikali ipo kazini muda wote.

Awali, Mkuu wa Wilaya ya Chato, Mtemi Simeon, alimwomba Naibu Waziri huyo kuona haja ya kuendesha operesheni kutokana na baadhi ya wananchi kutoka katika maeneo nje ya wilaya hiyo kuanzisha shughuli za kibinadamu ndani ya shamba hilo, suala ambalo ni kinyume cha sheria.

Mkuu huyo wa wilaya alisema wananchi katika maeneo hayo wana mahitaji makubwa ya ardhi, hivyo wizara ione namna ya kuwasaidia ekari 5,000 ili wapate maeneo ya kulima na kuchungia mifugo yao.

Naye Thadeus Shirima, Meneja wa shamba hilo alimweleza Naibu Waziri licha ya kuwa hadi hivi sasa zaidi ya ekari 900 tayari zimepandwa miti, lakini shamba hilo limekuwa likikabiliwa na uhaba wa watumishi pamoja na vitendea kazi yakiwamo magari.

# Wapigwa 'stop' kuagiza vifaa vya hali ya hewa

**Na Faustine Feliciane**

SERIKALI imetoa onyo kwa watu na mashirika binafsi wanaoagiza na kutumia vifaa vya upimaji hali ya hewa bila kuwa na kibali cha Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) na kuwataka waache mara moja.

Akizungumza kwenye ufunguzi wa Mkutano wa Baraza la Wafanyakazi wa Mamlaka hiyo, Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Isack Kamwelwe, alisema baada ya kupitishwa kwa Sheria ya Mamlaka ya Hali ya Hewa, ni marufuku kwa taasisi au watu binafsi kuagiza vifaa hivyo bila kupitia TMA.

"Sheria hii mpya ambayo imepitishwa na Bunge mwaka huu, inaipa mamlaka kamili TMA katika utabiri wa hali ya hewa, sasa kwa wale wote wanaoagiza vifaa vya utabiri bila kuwa na mawasiliano na kibali cha TMA kuacha mara moja," alisema Kamwelwe.

Aidha, alisema kuwa kwa sasa wale wote wanaotumia huduma za utabiri kibiashara wanapaswa kulipia ili kuongeza kipato kwa TMA.

Aidha, Waziri Kwamwelwe, ameitaka TMA kuharakisha utungaji wa kanuni za sheria hiyo ili aweze kuzipitia na kuzipitisha kuanza kutumika.

"Tayari sheria imepitishwa, sasa naagiza TMA kuandaa kanuni zake niweze kuzipitia kabla ya kuzipitisha zianze kutumika," alisema.

Waziri Kamwelwe, pia aliweka wazi kuwa serikali ilipitisha bajeti ya ununuzi wa rada tatu na fedha hizo zipo tayari, lakini hazijatolewa kwa kuwa TMA inachelewesha mchakato wa ununuzi wa rada hizo.

"Fedha hizi zipo, lakini lazima niseme ukweli ninyi (TMA) mmechelewesha kukamilisha mchakato wa manunuzi wa rada hizi na ndio maana fedha hazijatolewa," alisema.

Mkurugenzi Mkuu wa TMA, Dk. Agnes Kijazi, alisema mkutano huo wa Baraza la Wafanyakazi pamoja na mambo mengine, utajadili bajeti ya mamlaka hiyo kabla ya kuiwasilisha wizarani tayari kwenda bungeni.

Akimkaribisha Waziri Kamwelwe, Dk. Kijazi alielezea changamoto zinazoikabili mamlaka hiyo kuwa ni pamoja na upungufu wa wafanyakazi ambao wengi wao wanahamia taasisi nyingine kutafuta maslahi bora, pia kutokuwa na jengo la kudumu licha ya kumiliki kiwanja.

Akijibu changamoto hizo, Waziri Kamwelwe, aliutaka uongozi wa TMA kuandaa kikao cha menejimenti kwa ajili ya kuangalia namna ya kuboresha maslahi ya wafanyakazi.

"Lakini kuhusu kutokuwa na jengo, kwa sasa serikali inahamia Dodoma na kuna majengo mengi yapo wazi, sasa kazi kwenu mchague jengo mnaloona litawafaa. Serikali itawapitia kabla ya kuanza ujenzi wa jengo lenu wenyewe," alisema Kamwelwe.

Mkutano huo uliofanyika jijini Dar es Salaam ulihudhuriwa na wawakilishi wa kanda zote wa TMA.

# Magari, bidhaa za mamilioni zanaswa mpakani Tunduma

**Na Ibrahim Yassin,** TUNDUMA

MAGARI matatu yakiwa na bidhaa mbalimbali zenye thamani ya Sh. milioni saba, yamekamatwa katika mji wa Tunduma mpakani mwa Tanzania na Zambia katika operesheni ya kusaka wahalifu ikiwamo uvushaji wa mali za magendo.

Mji wa Tunduma ni wa kibiashara kutokana na mwingiliano wa watu kutoka nchi za Zambia na Congo. Kutokana na hilo, watu hutumia mwanya huo kufanya kile wanachoona kitawarahisishia kujipatia kipato ikiwamo biashara za magendo.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Songwe, George Kyando, alisema jana kuwa magari hayo yamekamatwa baada ya kuvushwa nchini Zambia kisha kurejeshwa Tanzania.

Pia alisema gari lingine aina ya Toyota Cresta lililokuwa likiendeshwa na Zachariah Boniface, limekamatwa likiwa na bidhaa za magendo zikiwamo zilizopigwa marufuku na Shirika la Viwango Tanzania (TBS).

Kamanda Kyando alisema magari hayo na mali hizo vimekutwa katika mazingira tofauti na pikipiki moja ambayo dereva wake hajafahamika ikiwa imetelekezwa na mzigo.

Kutokana na operesheni hiyo, alisema watu sita wanashikiliwa katika kituo cha polisi Tunduma kwa mahojiano na bidhaa na magari yaliyokamatwa.

Dotto Mashaka, mkazi wa Tunduma, alipongeza hatua ya Jeshi la Polisi kwa operesheni hiyo, huku akisema inapaswa kuwa endelevu ili kudhibiti wafanyabiashara wasio waaminifu wanaongoza kuuza bidhaa kwa njia za magendo huku wakiinyima mapato serikali.

Mahamoud Hamza, mkazi mwingine wa Tunduma, alisema kitendo cha wafanyabiashara kununua bidhaa Dar es Salaam wakidai wanazipeleka Zambia, wakati wakifika mpakani wanashusha mizigo vichakani kisha inabebwa kwa bodaboda kutunzwa stoo kunaikosesha mapato serikali.

Alisema licha ya Jeshi la Polisi kufanya jitihada kubwa ya kunasa bidhaa hizo, pia kuna haja ya kufanya kazi hizo usiku na mchana pasipo kukoma ili kudhibiti hali hiyo.

HABARI KITAIFA

# Kitoweo nyama chaadimika kisa uchafu

**Na Idda Mushi,** MOROGORO

WAKAZI wa Manispaa ya Morogoro wamekosa nyama kwa siku ya tatu mfululizo na kuwaondolea walaji fursa ya kupata kitoweo hicho baada ya Mamlaka ya Chakula na Dawa Tanzania (TFDA), kufungia machinjio yaliyopo kutokana na uchafu.

Baadhi ya wananchi, Kassim Juma, Sofia Saleh na Yona Kibirizi, walisema kukosekana kwa nyama katika maeneo yote ya manispaa kumesababisha usumbufu mkubwa kwa walaji wakiwamo watu binafsi na wafanyabiashara wanaotumia kwenye migahawa na hoteli.

Walishauri mamlaka husika kufanyia kazi sababu zilizotajwa na TFDA za kutoridhishwa na hali ya usafi katika machinjio hayo ambayo yako katikati ya mji wa Morogoro, hivyo kuhatarisha afya ya walaji na wananchi wanaoishi jirani.

Nao wafanyabiashara wa nyama na mazao mengine yatokanayo na mifugo katika Manispaa ya Morogoro, Yona Chilendu, Kepha Mazengo na Matola Kisiwa, kwa nyakati tofauti walisema wameathirika kwa kiasi kikubwa kutokana na kufungwa kwa machinjio hayo kwa kuwa wanategemea biashara hiyo kuendesha maisha yao.

Walielezea kushangazwa na kufungwa mara kwa mara kwa machinjio hayo, huku uongozi wa Halmashauri ya Manispaa ukishindwa kuchukua hatua mwafaka kurekebisha upungufu uliotajwa licha ya kwamba wanaolipa ushuru.

Walidai machinjio hayo yalifungwa bila taarifa na kusikia pembeni kuwa ni kutokana na uchafu uliokithiri kwenye eno la kuchinjia na kwenye chemba za vyoo zilizoelezwa kuvuja kinyesi na kutiririsha ovyo maji machafu yenye harufu kali.

Katika machinjio hayo, shughuli za kawaida za uchinjaji zilionekana kusimama, huku zaidi ya ng'ombe 150 wakionekana kufungiwa ndani bila kupewa huduma zozote muhimu kwa mifugo.

Diwani wa Mwembesongo, Ally Kalungwana, alibainisha kuwa ziko hujuma zinazofanywa kukwamisha kuendelea kwa machinjio hayo ikiwamo kubadilishwa matumizi kwa fedha zinazotengwa kwa ajili ya ukarabati wa machinjio hayo.

"Nimekuwa nalisemea hili bila mafanikio na zaidi kuhusu ubovu wa mtandao wa maji taka. Zilitengwa Sh. milioni 22 ili mtandao huo uunganishwe na mtandao mkubwa ulio chini ya Moruwasa (Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Morogoro), lakini cha ajabu matumizi yakabadilishwa kienyeji," alisema.

Pia alielezea kushangazwa na machinjio hayo kuzuiwa kuendelea na kazi bila kuwapo kwa barua maalumu wakati eneo hilo linategemewa kama ajira kuendesha maisha ya wengi na kutoa mahitaji ya kitoweo cha nyama kwa wananchi.

Mkurugenzi wa Manispaa ya Morogoro, John Mgalula, alipohojiwa alisema hatua mbalimbali zinaendelea kuchukuliwa ili kurejesha huduma hiyo ya upatikanaji wa nyama kwa wananchi na tayari wamekodi gari la mtu binafsi kwa ajili ya kuhakikisha maji machafu yananyonywa.

Mkurugenzi huyo alisema wanaendelea pia kuharakisha ukarabati wa eneo la kuchinjia ili wakati wowote kuanzia sasa, shughuli za uchinjaji ziendelee kama kawaida.



Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Jasinta Mboneko, akikagua gwaride la Jeshi la Polisi mkoani Shinyanga, wakati wa Siku ya Wanafamilia wa Polisi na kuuaga mwaka 2018 na kuukaribisha 2019, iliyofanyika juzi. **PICHA: MARCHO MADUHU**

# Tatizo la nyonga sasa janga kiafya

INATOKA UK 3

unakufa, huku unaongea ndiyo maana tunawaelimisha watu wajifunze," alisema.

Alisema mtu aliyepata shida ya nyonga asipotibiwa anapata matatizo makubwa na kushindwa kufanya tendo la ndoa jambo ambalo linaumiza kisaikolojia.

Aidha, alisema wana takwimu ambazo bado hazijachapishwa hivyo kwa sasa wanazifanyia uchambuzi ifikapo Novemba mwaka huu zitatangazwa rasmi.

Naye Daktari Mwandamizi wa Mifupa MOI na Mhadhiri Mwandamizi wa Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili (Muhas), Billy Haonga, alisema kuna mivunjiko ambayo inahatarisha maisha kama hatua za haraka hazijachukuliwa kwa kuwa mgonjwa anaweza kupoteza maisha.

"Kama mvunjiko umeenda kugusa kwenye mshipa mkubwa wa damu hapa hatuna cha kufanya mgonjwa atakufa pale pale alipopatia ajali ndiyo maana unaona mtu kagongwa ghafla anakufa na hata kwenye ajali unaona wengine wanakufa na wengine wanapona," alisema.

Dk. Haonga alisema wako ambao wanavunjika mishipa midogo midogo ambayo iko katika nyonga. Alisema mtu huyo hujikuta anavuja damu kidogo kidogo, hivyo ana uwezo wa kufika hospitalini na ni lazima kuwapo na huduma ya haraka ili damu isiendelee kutoka.

Alisema mgonjwa wa nyonga kama hajapatiwa huduma ya kwanza anaweza kupoteza maisha, endapo haitaungwa vizuri mwili wake mmoja utakuwa uko juu na mwingine utakuwa chini, hivyo kutembea na maumivu.

"Kwa bahati mbaya matibabu haya yanapatikana Tanzania hapa MOI, hivyo aliyepata ajali mkoani Kigoma asipokuja Dar es Salaam anaweza kubaki na kilema cha maisha au kuwa na mguu mfupi, mguu usiokuwa na ufahamu na kupata maumivu kutokana na eneo aliloumia kushindwa kuunga," alisema.

Alisema gharama nyingi ziko kwenye vifaa katika kumtibia mgonjwa na changamoto kubwa ni upatikanaji wa damu wakati wa kumhudumia mgonjwa.

"Ni lazima damu iwapo kwa kuwa inapokosekana unapoteza uhai wa mgonjwa, hivyo kikubwa kinachotuathiri ni upatikanaji wa damu, vile vyuma tunavyowawekea wagonjwa sio gharama kubwa," alisema.

## Walilia uhaba

INATOKA UK 5

la vijana kitaifa la Femina kila mwaka, mtandao wa mkoa wa Tanga umepata tunzo ya mkoa bora kitaifa mwaka 2019.

Mwenyekiti wa Fema Mkoa wa Tanga, Mayombo Charles, alisema mkoa wa Tanga una klabu 118 za Fema katika wilaya zote nane ambazo ziko katika mtandao wa malezi ya vijana ambao ulianzishwa mnamo mwaka 2017.

Wakati huo huo, wanafunzi wanaosoma shule mbalimbali za sekondari katika mkoa wa Tanga wameiomba serikali kutoa adhabu kali kwa wanaume wanaowapa mimba wanafunzi wa kike ili kukomesha mimba za utotoni.

Ibrahim Athumani, mwanafunzi wa Shule ya Sekondari Songa na Mwanahawa Mohamed wa Shule ya Sekondari ya Kerenge zote za Muheza na Kiondo Kilua wa Kwagunda wilayani Korogwe, kwa nyakati tofauti walisema wanaume wanaofanya hivyo wapewe adhabu kali.

## Wabunifu 3,000

INATOKA UK 5


"Mwanzo mwa mwezi huu, tulifanikiwa kuratibu mashindano ya kitaifa ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu (Makisatu) na wabunifu 60 walichaguliwa kushindana kutoka katika makundi ya shule za sekondari, sekta isiyo rasmi, vyuo vya ufundi, vyuo vikuu na taasisi za utafiti na maendeleo. Washindi watatu katika kila kundi la ubunifu walipewa tuzo na kuahidiwa kuendeleza ubunifu wao," Dk. Nungu alisema.

Kiongozi Mkuu wa HDIF, David McGinty, alisema hii ni mara ya tano kwao kushirikiana na tume kuendesha wiki ya ubunifu kwa ufadhili wa UKaid na tayari kuna mafanikio makubwa na mabadiliko katika eneo la ubunifu nchini.

McGinty alisema tayari Tanzania imefikia nafasi ya 31 juu katika rekodi za kipimo cha ubunifu cha dunia.

Makamu Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Kimataifa ya Serikali ya Uingereza ya DFID, Jane Miller, alisema kila mwaka wiki hiyo ya ubunifu imekuwa ikitoa fursa kwa wabunifu, wafadhili na sekta binafsi kukutana kubadilishana uzoefu na kuhamasisha kukuza sekta ya ubunifu.

Alisema wiki hiyo inatarajiwa kuwa na shughuli zaidi ya 60 na maonyesho zaidi ya 30 katika maeneo mbalimbali jijini Dar es Salaam.



# Pinda ajitosa kuisaidia CCM kusaka wanachama Chadema

**Na Mwandishi Wetu,** SIMANJIRO

WAZIRI Mkuu mstaafu, Mizengo Pinda ambaye ni mlezi wa CCM Mkoa wa Manyara, amewapokea wanachama wapya 233 wa upinzani akiwamo aliyekuwa Katibu wa Chadema Wilaya ya Simanjiro na Mwenyekiti wa Vijana (Bavicha), Mkoa wa Manyara, Frank Oleleshwa.

Wanachama hao wa Chadema wamepatiwa kadi za CCM na Pinda ambaye yupo katika ziara ya siku nane mkoani hapo akitembelea majimbo saba.

Akizungumza kwa niaba ya wanachama hao wapya, Oleleshwa alisema sababu za kuhamia CCM zipo nyingi.

Alisema kwa mfano, masuala yaliyokuwa yanapiganiwa na Chadema yanafanyika CCM.

"Kazi zinazofanywa na Rais John Magufuli ndizo nilizokuwa ninataka zifanyiwe nikiwa Chadema, hivyo nimeamua kumuunga mkono.

"CCM imeonyesha utashi mkubwa wa kizalendo katika kuongoza nchi, hivyo tumeamua kuhamia huku ili kuunga mkono juhudi hizo," alisema.

Akizungumza baada ya kuwakabidhi kadi wanachama hao wapya wa sehemu mbalimbali wilayani Simanjiro, Pinda aliwapongeza kwa kujiunga na CCM.

Alisema hivi sasa Rais Magufuli, ambaye ndiye Mwenyekiti wa CCM Taifa, anafanya kazi kubwa ya kufanikisha maendeleo, hivyo Watanzania wanapaswa kumuunga mkono.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Manyara, Simon Lulu, alimpongeza Katibu wa CCM Wilaya ya Simanjiro, Ally Kidunda, kwa kuongoza mkoani humo kwenye kazi ya kusajili upya wanachama wao kwa njia ya elektroniki.

"Katibu nakupongeza mno kwa kazi nzuri ya kusajili wanachama wetu kwa njia ya elektroniki kwa kuwa ninyi Simanjiro ndiyo mnaoongoza Manyara nzima kwa kusajili wanachama wengi," alisema.

Kidunda alisema bado wanaendelea na suala hilo la kusajili wanachama wao katika sehemu mbalimbali za eneo hilo.

"Kazi ya kusajili wanachama wetu kwa njia ya kielektroniki kwenye wilaya yetu inaendelea na tunashukuru kwa pongezi hizo kutoka kwa Mwenyekiti wa CCM wa Mkoa wa Manyara," alisema.

Pinda baada ya kumaliza ziara yake kwenye wilaya za Kiteto na Simanjiro, anatarajia kwenda wilaya za Babati, Hanang' na Mbulu.



Makamu Mkuu wa shule ya sekondari Mirerani Benjamin Mkapa, wilayani Simanjiro, mkoa wa Manyara, Thomas Senteu na wanafunzi wa kidato cha kwanza wakiangalia sehemu iliyoezuliwa na upepo juzi, ambapo mdau wa elimu Peter Toima ametoa msaada wa mabati 50. **PICHA: GIFT THADEY**

# AfDB yaahidi kusaidia kilimo, viwanda EAC

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

BENKI ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), imeahidi kutoa msaada zaidi katika sekta ya kilimo na viwanda katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki, (EAC).

Ahadi hiyo ilitolewa na Mkurugenzi Mkuu wa ukanda wa Afrika Mashariki wa benki hiyo, Gabriel Negatu, wakati alipokwenda kujitambulisha ofisini kwa Katibu Mkuu wa EAC, Balozi Liberat Mfumukeko juzi.

Alisema uwekezaji katika kilimo na viwanda ni jambo linalopewa umuhimu kwa maendeleo katika ukanda wa Afrika Mashariki.

Akizungumza na waandishi wa habari baada ya kuonana na Katibu Mkuu, Negatu alisema ni wazi kwamba uchumi wa nchi za Afrika Mashariki umejikita zaidi katika kilimo ambacho ni mhimili wa uchumi unaochangia asilimia 75 hadi 90 ya idadi ya watu wake.

Alisema ili kukidhi masoko ya kikanda na kimataifa, bidhaa za mazao zinatoa fursa kwa ukuaji wa viwanda.

"Mafanikio katika kilimo ni muhimu kwa ajili ya kuwainua wananchi kutoka hali ya umaskini kwa sababu inaajiri zaidi ya asilimia 75 ya idadi ya watu katika nchi wanachama ambao wengi wao wanaishi katika maeneo ya vijijini," alisema.

Aidha, alisema sekta ya kilimo inaboresha maisha ya watu wa vijijini na mijini.

Kwa upande wake, Balozi Mfumukeko, aliishukuru AfDB kwa kuchangia matangamano wa Afrika Mashariki ana anaahidi kwamba jumuiya hiyo itaimarisha ushirikiano na kukua zaidi.

Alisema kwa miaka mitano iliyopita, AfDB, imetoa msaada katika miradi mbalimbali akitaja kwa mfano upembuzi yakinifu na ujenzi wa miundombinu ya barabara kutoka Nyakanazi -Kasulu, Rumonge Bujumbura na Lusahunga - Rusumo, Kayonza, Masaka-Mutukula-Kyaka-Bugen.

# DC akabidhi wazee kadi za matibabu

**Na Zanura Mallel,** LONGIDO

MKUU wa Wilaya ya Longido, Frank Mwaisumbe, amekabidhi kadi za bima ya afya kwa wazee 79 wa Kata ya Longido kwa zitakazowasaidia kupata matibabu ndani na nje ya wilaya.

Akikabidhi kadi hizo juzi, alisema serikali inatambua changamoto wanazopitia wazee, ikiwamo kushindwa kumudu gharama za matibabu na kuona ni vyema ikaingia gharama kuhakikisha mnapatiwa huduma bila usumbufu.

"Si kwamba bima hii ni bure hapana, gharama hizi za matibabu zinalipiwa na serikali, hivyo serikali imesimama kwa niaba yenu wazee," alieleza.

Lakini pia alieleza alimwandikia barua Mkurugenzi wa Halmashauri, Juma Mhina, kumtaka kuhakikisha wazee hawa wanapata ruzuku ya Tasaf ili waweze kujikwamua kiuchumi.

"Umri huu unamahitaji mengi lakini nguvu hakuna tena katika utafutaji, ila nimeshamwandikia barua mkurugenzi ikiwezekana halmashauri pia iwe na mfumo wa kuwawezesha wazee ndani ya wilaya," alidai.

"Palipo na wazee najua mambo yanakwenda vizuri, Wilaya ya Longido tunajivunia kuwa na wazee maana bado tunawahitaji katika nyanja mbalimbali," alisema.

Aidha, alieleza serikali tofauti na kuwajali wazee muweze kupatiwa matibabu bila usumbufu, bado imetoa Sh. bilioni 1.5 kwa ajili ya ujenzi wa hospitali ya wilaya.

Mwaisumbe alisema, ujenzi wa hospitali hiyo utakapokamilika huduma zote zitatolewa, ikiwamo kitengo cha upasuaji wa moyo, huduma ya mionzi pamoja na jengo la kulaza wagonjwa.

Naye Ofisa Ustawi wa Jamii Wilaya ya Longido, Atuganile Chisunga, alisema Wilaya ya Longido ina jumla ya wazee 6,023 lakini kwa sasa wameanza kutoa bima hizi kwa wazee 79 wa Kata ya Longido.

Alisema awali wazee hawa walikuwa wakipatiwa matibabu na barua za utambuzi kutoka ofisi ya watendaji wa vijiji ila kwa sasa wanawapatia bima hizo ili kuepukana na usumbufu.

"Wazee hawa ni wazee kweli, lakini kwa namna nyingine ni wazazi na walezi wa wajukuu walioachiwa na watoto wao, wanakabiliwa na ukosefu wa vyanzo vya kiuchumi DC naomba ulitizame hili," aliomba.

Steave Lesinga mkazi wa Kata ya Longido, ambaye pia ni mnufaika wa bima hiyo aliishukuru serikali ya awamu ya tano kwa hatua hiyo ya kuwatambua wazee kwa kuwawezesha katika sekta ya afya kwa kuwapatia bima.

"Kwa niaba ya wazee wenzangu, tunasema ahsante sana DC, hakika tumeona kazi ya awamu ya tano na ni kwa vitendo, mfikishie salamu zetu Rais Magufuli mwambie wazee wa Longido tunamwombea baraka tele," alisema Baraka.





# Kaya 93 zilizokumbwa na mvua ya mawe zakumbukwa mabati

**Na Godfrey Mushi,** SAME

HATIMAYE kaya 93 za wananchi wa vijiji vya Kadando, Mpirani na Kalimawe ambavyo vilipoteza makazi yao kutokana na maafa ya mvua ya mawe iliyoambatana na upepo wamepata ahueni, baada ya Shirika la Kimataifa la World Vision Tanzania kupeleka msaada wa mabati 928.

Usiku wa Machi 6, mwaka huu, wakazi hao wanaoishi katika safu ya juu ya milima ya Upare katika Jimbo la Same Mashariki walishuhudia hasara kubwa iliyotokana na mvua hizo kuezua mapaa na kuangusha kuta za nyumba wanazoishi pamoja na madarasa matano ya Shule ya Msingi Kadando.

Akikabidhi msaada huo jana kwa Mkuu wa Wilaya ya Same, Rosemary Senyamule, Meneja Miradi wa Shirika hilo Kanda ya Kaskazini, Frida Chilimo, alisema nia yao ni kuona watoto, familia na jamii kwa ujumla wanarejea katika hali yake ya kawaida na kupata huduma zinazotakiwa kwa ufanisi hususani elimu. "Baada ya kufanya tathmini ya kina kwa kushirikiana na serikali, Shirika la World Vision Tanzania kama mmoja wa wadau wa maendeleo katika Wilaya ya Same, liliona haja ya kuingilia kati ili kutoa msaada.

"Hivyo tukaamua kutoa mabati kusaidia kaya 90 zilizoathirika zaidi pamoja na kutoa mabati ya madarasa yote matano yaliyoezuliwa. Jumla ya mabati tuliyoyatoa ni 928 yenye thamani ya shilingi milioni 21,856. Kati ya hizo bati 731 zina kiwango cha G 30 na bati 197 ni za kiwango cha G 28."

Awali akitoa taarifa kuhusu maafa hayo kwa Mkuu wa Wilaya na ujumbe wake kutoka World Vision Tanzania, Ofisa Mtendaji wa Kata ya Maore (WEO) katika wilaya hiyo, Ezekiel Singo, alisema katika vikao vyao vya kamati za maafa wamekubaliana na kupitisha uamuzi wa kuchangisha wafanyabiashara wakubwa kiasi cha Sh. 10,000, watumishi serikali ndani ya kata hiyo Sh. 5,000 na wafanyabiashara wadogo Sh. 5,000.

Baada ya kauli hiyo, Mkuu wa Wilaya ya Same, Rosemary Senyamule, alilipongeza Shirika hilo la World Vision kwa kuona umuhimu wa kuzisaidia kaya hizo kurejea katika makazi yake ya awali.

"Siku zote hawa World Vision Tanzania wamekuwa msaada mkubwa katika wilaya yetu, wamekuwa wadau wa kwanza kabisa kuungana na serikali pamoja na waathirika hawa kutafuta namna ya kuwasaidia. Niwaombe msiache kutusaidia, nifikishieni shukrani zangu kwa Mkurugenzi Mkuu (Gilbert Kamanga)," ameeleza Mkuu huyo wa Wilaya.

Aliagiza maofisa wa serikali akiwamo Mtendaji wa Kata hiyo kuhakikisha msaada huo unagawiwa kwa haki na kumfikia kila mlengwa. Mbali ya wadau hao, Mkuu huyo wa Wilaya aliwaeleza pia wananchi hao kwamba Mbunge wa Viti Maalum Taifa na Mbunge wa zamani wa jimbo hilo (CCM), Anne Kilango Malecela, ametuma msaada wa saruji mifuko 150 pamoja na Sh. milioni moja kusaidia wahanga hao.



Mkuu wa Wilaya ya Same, Rosemary Senyamule (wa tatu kushoto), akimkabidhi msaada wa bati, Hawa Ali ambaye nyumba yake iliezuliwa na upepo. Mabati hayo yalitolewa na Shirika la World Vision Tanzania juzi. **PICHA: GODFREY MUSHI**

# Mila zisizofaa zinachangia ukatili kijinsia

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

WAJUMBE 30 wa kamati za mpango kazi wa taifa wa kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na watoto katika Wilaya ya Rombo mkoani Kilimanjaro, wamesema kama jamii inataka kufanikiwa kudhibiti masuala ya ukatili unaoendelea katika ngazi ya kaya ni lazima kuondokana na mila zilizopitwa na wakati.

Wazo la kutaka jamii ya Wachaga kuweka kando matumizi ya jina la kimila aina ya 'Isale' ambalo hutumika kuombana msamaha baada ya mtu kutenda kosa na kisha kumalizana kienyeji bila kufuatwa taratibu za kisheria, lilitolewa jana na mwanamke mashuhuri kutoka Kata ya Nanjara, Wilaya ya Rombo, Mwanaidi Mkumbo.

Mkumbo aliyasema hayo jana, wakati akihitimisha mafunzo ya siku tatu ya kuzijengea uwezo kamati hizo maarufu kama Mtakuwwa.

Katika mafunzo hayo yaliyoandaliwa na Shirika la Kwieco kwa ufadhili wa Taasisi ya Friedrich Naumann Foundation for Freedom (FNF), mwanamke huyo wamesema kwa sasa ajenda yao kuu wanapokutana na kinamama kwenye vikundi ni kuwashauri kuachana na kuliabudu jani hilo chonganishi katika jamii ya wachaga.

Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Wilaya ya Rombo, Jonathan Mkama, alisema mbali ya kujengewa hoja ajenda hiyo ya kushauri kupuuzwa kwa matumizi ya jamii hiyo, bado iko haja kwa watumishi, wafanyabiashara na watu wanaokosa muda wa kukaa na familia, kutenga siku moja kila wiki kuogesha watoto wao ili kubaini kama wana tatizo.

"Ni vyema angalau mara moja kwa wiki kama wanao ni wadogo uwe unajitahidi kuwaosha, ukimwogesha mtoto kama mzazi unaweza kugundua matatizo aliyonayo.

Utafutaji wa fedha umetutenga mbali sana na familia zetu, watoto wamekuwa ni wa house girl, sasa hiyo imefanya hata kutojua kwamba watoto wetu wanapata ukatili wa namna gani. Ukiwa karibu na watoto wako na kuongea nao mara kwa mara wanaweza wakakuambia matatizo waliyonayo."

Aidha, Ofisa Elimu ngazi ya kata, Thadeus Shayo, ameshauri kuwa katika suala la ujauzito kwa wanafunzi, wao wanataka sheria ing'ate kote kote na itumike kukamata mwanafunzi mwenyewe, mtu aliyemtia mimba na mzazi wa msichana ili wote waweze kushirikishwa na ijulikane ni nani ambaye anatakiwa kuwajibika.

Kwa upande wake, Ofisa Maendeleo ya Jamii Kata ya Ikwiini, Farida Janowalah, ameeleza: "Sisi kama maofisa maendeleo ya jamii kipindi cha nyuma tulipokuwa hatuna mafungu ya kufanyia kazi za utekelezaji wa Mtakuwwa, tulikuwa tunaweza kufanya haya alisema kutumia bajeti ndogo ambayo inapatikana katika halmashauri pamoja na kutumia mashirika ya kiraia ambayo yanaisaidia halmashauri katika kutekeleza mpango wa Mtakuwwa."

Taarifa zaidi zinaeleza kuwa katika Wilaya ya Rombo, bajeti kwa ajili ya Mtakuwwa katika mwaka mpya wa fedha wa 2019/2020 imetengwa kiasi cha Sh. milioni nne pekee kwa ajili ya kufanya ufuatiliaji.

Awali, Ofisa Mradi wa kuzijengea uwezo kamati hizo kutoka Shirika la Kwieco, Veronika Ulomi, alisema mradi huo unalenga kuelimisha kamati za Mtakuwwa na kwamba mafunzo haya yanahusisha kamati ambazo zinajumuisha maofisa watendaji wa kata, waratibu wa elimu kata, maendeleo ya jamii kata pamoja na wamama mashuhuri.

"Tumeanza na Wilaya ya Rombo katika kata saba, lakini kwa mwaka huu tuna mpango wa kufikia kata 14, ambapo ni mwendelezo wa mafunzo mengine ambayo yalishawahi kutolewa tena mwaka jana ambayo yalihusisha kata 10. Tumefanya mafunzo ya siku tatu lakini pia tutaendelea wiki ijayo kata nyingine saba zilizobakia," alisisitiza Ulomi.

## Waomba serikali kusikiliza ushauri wa wataalamu

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

WAFANYABIASHARA wa mazao na baadhi ya wadau wa mazingira katika Mkoa wa Kilimanjaro wameiomba serikali kusikiliza ushauri wa wataalamu wa viumbe kuhusu taarifa ya kuwepo kwa hatari ya kutoweka nyuki wanaochavusha mimea ya mazao ya chakula na biashara.

Mfanyabiashara wa mazao ya chakula, William Majaliwa, alisema utabiri wa wataalamu hao ni muhimu kuzingatiwa kwa sasa ili kulinda afya za walaji na mustakabali wa kizazi kijacho.

Mwingine aliyeomba kutazamwa upya tahadhari hiyo ni Witness Zablon ambaye ni mdau wa mazingira katika mji wa Moshi aliyedai kama hakuna nyuki, kunaweza kuwapo kwa matishio ya baa la njaa miaka ijayo.

Wiki iliyopita, mtaalamu wa nyuki nchini, Dk. Henry Njovu, alinukuliwa na gazeti hili alisema kuwa nyuki wanaosaidia uchavushaji katika mimea inayozalisha chakula na mazao ya biashara hapa nchini wako katika hatari ya kutoweka kutokana na matumizi makubwa ya dawa za kemikali za viwandani wakati wa msimu wa kilimo.

Akizungumza hayo katika kongamano la watafiti na wataalamu wa mazingira lililofanyika katika Chuo cha Kimataifa cha Usimamizi na Uhifadhi wa Wanyamapori Tanzania maarufu kama Mweka.

Kwa mujibu wa Dk. Njovu, matumizi ya dawa za kemikali katika mashamba ya kilimo husababisha nyuki kufa na kuweka viumbe hivyo katika hatari ya kutoweka.

"Tatizo la uharibifu wa mazingira limeathiri kwa kiasi kikubwa nyuki hawa kwa asilimia 90 ambao kimsingi ndio wanaotegemewa kwa ajili ya uchavushaji wa mazao ya chakula na biashara.

"Hivi sasa wako katika hatari ya kutoweka kwa sababu ya kuwapo kwa athari za mabadiliko ya tabia nchi na wakulima kutumia kemikali za viwandani msimu wa kilimo."

## HABARI DODOMA






Mwenyekiti wa Bodi ya Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati na Majini (EWURA), Prof. Jamidu Katima, akizungumza katika mkutano wa wadau wa maji nchini, uliofanyika jijini Dodoma jana. Kulia ni Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa mamlaka hiyo, Nzinyangwa Mchany. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Duwasa kuyafikia maeneo yasiyokuwa huduma maji

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MAMLAKA ya Majisafi na Usafi wa Mazingira mjini Dodoma (Duwasa), imeanza mchakato wa kuyafikia maeneo yote ya pembezoni mwa mji ambayo hayana huduma ya majisafi.

Akizungumza na Nipashe jana, Mkurugenzi wa Mamlaka hiyo, Mhandisi David Pallangyo, alisema lengo kubwa la nchi ni kutomuacha mtu yeyote nyuma kwenye utoaji wa majisafi na usafi wa mazingira.

"Sisi Duwasa kuna miradi mbalimbali ya maendeleo inayotekelezwa na Mhandisi Mshauri ambaye anatarajiwa kukamilisha kazi Aprili," alisema.

Pallangyo alibainisha kuwa baada ya tathmini hiyo, mtaalamu huyo atatoa gharama zinazohitajika pamoja na usanifu wa kina ili kuweza kuyafikia maeneo hayo. "Akimaliza kazi mwezi Mei, tutayafikia maeneo ambayo hatujayafikia," alisema.

Aidha, alifafanua kuwa hadi sasa mamlaka hiyo imewafikia watu kwa asilimia 80 ambapo ni katikati ya mji. "Lakini pembezoni kadri ya mji unavyopanuka na ujio wa makao makuu tunazidi kujipanua kwenda pembeni, kazi tunayoifanya sasa hivi ni kuainisha mahitaji kabla hata ya watu hawajafika huko ili wanapokwenda wakute huduma ya maji yameshafika," alisema.

Mkurugenzi huyo alisema watahakikisha maeneo yote hayo yanapata maji na utekelezaji wake unafanywa kwa kushirikiana na Wizara ya Maji.

Pamoja na hayo, alisema Duwasa kwa sasa inaendelea na utekelezaji wa miradi mbalimbali inayogharimu kiasi cha Sh. bilioni 2 katika mwaka wa fedha 2018/19.

"Kuna maeneo ya pembezoni ambayo pia tulikuwa tumepanga kuyafikia sisi kwa uwezo wetu maeneo hayo ni kama Chidachi, Miganga, Mkonze, Mkalama, Itega, haya ni maeneo ambayo tulikuwa hatujayafikia tumepanga kuyafikia kwa uwezo wetu wa ndani," alisema.

# Watuma salamu Dodoma wapewa somo

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

WANACHAMA wa chama cha watuma salamu redioni mkoani Dodoma, wametakiwa kuchangamkia fursa za serikali kuhamia jijini hapo kujiinua kiuchumi badala ya kuishia kutuma salamu.

Rai hiyo ilitolewa jana na Mwenyekiti wa chama hicho, Mzee Langolango, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari jijini hapo kuhusu maandalizi ya mkutano mkuu wao utakaofanyika Aprili 7, mwaka huu.

Alisema wanachama hao badala ya kujikita kwenye kutuma salamu ni wajibu wao pia kutumia nafasi zao katika fursa zilizopo za kiuchumi ambazo zitawawezesha kujiinua kiuchumi.

"Pamoja na watuma salamu kutoa elimu kwa kupitia tasnia ya habari, lakini wanatakiwa kujishughulisha na uwekezaji unaoweza kujipatia kipato cha kiuchumi badala ya kuishia kwenye kutuma salamu tu," alisema.

Aidha, aliwasisitiza wanachama hao kuiunga mkono serikali katika ujenzi wa uchumi wa viwanda.

"Uchumi wa viwanda vya kati ni kwa Watanzania wote, hivyo watuma salamu ni muhimu waiunge mkono serikali katika kuhakikisha azima hiyo inakamilika ila kwa kufanya kazi na kulipa kodi," alisema.

Aliwataka kuibua miradi itakayowafanya kupata mikopo kutoka taasisi mbalimbali za kifedha.

# RITA watoa vyeti kwa watoto milioni 2.9

**Na Elisante John,** SINGIDA

JUMLA ya watoto 2,978,629 wa mikoa 13 nchini wamepatiwa vyeti vya kuzaliwa chini ya mpango wa serikali kupitia Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (RITA).

Hayo yalibainishwa na Waziri wa Katiba na Sheria, Dk. Augustine Mahiga, katika uzinduzi wa mpango huo, kwa mikoa ya Dodoma na Singida, uliofanyika kwenye viwanja wa stendi ya zamani, vilivyopo Halmashauri ya Manispaa ya Singida.

Alitaja mikoa mingine iliyopo katika mpango huo ni Mara, Simiyu, Lindi, Mtwara, Geita, Shinyanga, Mbeya, Songwe, Mwanza, Iringa na Njombe.

Alisema kutokana na hamasa hiyo anayo imani kubwa idadi ya watoto itaongezeka na kufikia zaidi ya milioni 3.5, iwapo changamoto mbalimbali zilizopo zitajadiliwa na kupatiwa ufumbuzi kupitia viongozi wa mikoa hiyo.

Aliwataka wakuu wa mikoa na wilaya kwenye maeneo yao, kuzikabili changamoto hizo ikiwamo uwepo wa imani potofu, desturi na tamaduni mbalimbali za makabila zilizopitwa na wakati, ili kufanikisha zoezi hilo.

"Maandalizi ya kuanza awamu ya pili yamekwisha anza, wizara itashirikiana na RITA kuangalia uwezekano wa kupata wadau zaidi watakaoongeza kasi... makundi mengine ya umri wa miaka sita hadi 17, ambao wengi wao ni wanafunzi, wanaohitaji vyeti, waweze kupata," alisema.

Dk. Mahiga alilishukuru Shirika la Watoto la Umoja wa Mataifa (UNICEF) na nchi ya Canada, kwa kufanikisha zoezi hilo, hadi mpango huo umeweza kutekelezwa hapa nchini.

Awali, Kaimu Ofisa Mtendaji Mkuu wa RITA, Emmy Hudson, alisema usajili wa kundi hilo katika mikoa ya Singida na Dodoma, unalenga pia kusajiliwa ndani ya muda mfupi baada ya tukio la kizazi kutokea.

Alisema kuwa, mpango huo katika mkoa wa Mwanza haujaweza kufanikiwa sana kutokana na sababu mbalimbali ambazo tayari zimeshabainika na zoezi la marudio linatarajiwa kuanza wakati wowote, ili kufikia lengo lililokusudiwa na serikali.

Mtendaji huyo alisema, katika utekelezaji huo, hadi sasa watoto 45, 173 sawa na asilimia 11.7 wa Mkoa wa Dodoma na 36,194 sawa na asilimia 12.9 kutoka Singida, wamesajiliwa na kupatiwa vyeti vya kuzaliwa, huku akiamini ndani ya wiki mbili zijazo, rika hilo lote litakuwa limefikiwa.





# Mzimu wa Maalim Seif wazidi kupasua kichwa viongozi CUF

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

WANACHAMA wa Chama cha Wananchi CUF wametakiwa kuzingatia sera na kuacha siasa zisizo na tija.

Hayo yameelezwa na Makamu Mwenyekiti wa chama hicho, Abasi Muhunzi, wakati akizungumza na waandishi wa habari mjini Zanzibar.

Makamu huyo aliwataka wanachama hao kufuata sera, katiba na malengo ya chama hicho na kuacha siasa zisizo na tija za kumfuata mtu.

Alisema chama hicho kimeshindwa kufikia malengo ya kushika dola kwa sababu ya kuongozwa na fikra za mtu binafsi.

Aliongeza kuwa wakati umefika sasa CUF kuachana na siasa zisizokuwa na tija za kumfuata mtu mmoja mawazo yake ambayo hayana mwelekeo wa kujenga mshikamano katika chama hicho.

Alieleza kuwa ufinyu wa mawazo na fukuzafukuza katika chama ni mambo ambayo yamekifikicha chama hicho katika wakati mgumu na kuonekana kama taasisi binafsi ya mtu, hatua ambayo ilijenga chuki kwa wanachama na viongozi.

Aliwataka wanachama na wafuasi wa CUF kujipanga na sasa chama hicho kinapita katika harakati za mikakati ya kuzaliwa upya kwa ajili ya kuelekea kushika dola katika uchaguzi mkuu mwaka 2020.

Aidha, alisema CUF haitomvumilia mtu yeyote aliyeshiriki kuhujumu mali za chama hicho ikiwamo kuchoma moto bendera pamoja na matawi ya chama hicho.

Alisema mali zote za chama hicho zinatambulika kisheria, hivyo hakuna haja ya kuona bado zinaendelea kuharibiwa na watu wenye dhamira mbaya kwa chama hicho.

"Tupo katika hatua ya kuandaa mpango wa kutembelea matawi yote ya chama ambayo kwa sasa yamefanyiwa hujuma na mengine kugeuzwa kuwa ofisi za chama cha ACT-Wazalendo, "alisema.

Naye mjumbe wa bodi ya wadhamini wa chama hicho, Mussa Kombo, aliwataka wanachama wa CUF kuimarisha umoja na mshikamano kwa lengo la kukifanya chama kuwa imara katika kuelekea kwenye mapambano ya kushika dola.

Aliwataka wafuasi wa chama hicho wasitetereke kutokana na kitendo cha baadhi ya wanachama kumuunga mkono aliyekuwa Katibu Mkuu wa CUF, Maalim Seif Sharif Hamad na kukihama chama, kwa kuwa bado wapo wanachama wenye uwezo wa kupima ukweli na kufanya uchambuzi wa kina katika mambo ya siasa.

"Chama chetu kinazingatia ubora na siyo kumfuata mtu matakwa yake binafsi...sisi tupo imara wala hatujayumba na wale wanaokihama chama hicho na kujiunga na ACT-Wazalendo kwa kumfuata Maalim Seif hiari yao," alisema.



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Ali Mohamed Shein, akiagana na mgeni wake, Balozi wa Tanzania nchini Zambia, Hassan Simba Yahya, baada ya kumaliza mazungumzo yao yaliofanyika Ikulu Zanzibar jana. **PICHA: IKULU ZANZIBAR**

# Serikali yajipanga kukabiliana bidhaa feki

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ), imesema imejipanga kuhakikisha bidhaa zote zinazozalishwa nchini zinakidhi viwango katika soko la ndani na nje kwa ajili ya kuongeza thamani.

Hayo yalisemwa na Waziri wa Biashara na Viwanda, Amina Salum Ali, katika maadhimisho ya Siku ya Viwango katika bara la Afrika ambazo huadhimishwa kwa mara ya kwanza Zanzibar.

Balozi Amina alisema viwango vya ubora wa bidhaa ndiyo kipaumbele cha serikali katika kufikia malengo ya nchi ya viwanda vya kati hatua ambayo itaifanya Zanzibar kuwa wazalishaji wakubwa na kusafirisha bidhaa hizo nje ya nchi.

Alisema serikali imeanzisha wakala wa viwanda vya kati (Snida) kwa ajili ya kufuatilia kwa karibu wazalishaji wa bidhaa za ndani na kuwapa ujuzi na utaalamu utakaowafanya kuzalisha bidhaa zenye ubora unaokubalika.

Aidha, alisema mikakati ya serikali ni kuwafanya wazalishaji wote wa ndani kufikia viwango bora vya uzalishaji wa bidhaa ambavyo vitakubalika na kuingia katika soko la ndani kwa mafanikio makubwa.

"Niwaombe watendaji wa Shirika la Viwango kuwa waadilifu na kuepukana na vishawishi vya rushwa ambavyo vinaweza kuliangamiza taifa kwa kuruhusu uingizaji wa bidhaa zilizopitwa na wakati," alisema waziri huyo.

Naye Mkurugenzi wa Shirika la Viwango la Zanzibar (ZBS), Khatib Mwadini, alisema wamejipanga vizuri kuhakikisha wanatekeleza malengo na mikakati ya serikali katika kufikia ubora wa viwango kwa bidhaa zinazozalishwa nchini.

Mwadini alisema tayari wapo katika hatua za kujenga maabara nne ambazo zitakuwa na uwezo wa kutoa vipimo vya bidhaa mbali mbali katika malengo ya kufikia ushindani wa uzalishaji wa bidhaa zitakazohimili soko la ndani na nje.

Aidha, aliwataka wazalishaji wa bidhaa ikiwamo wajasiriamali kufikisha bidhaa zao na kupata ubora wa viwango katika shirika la (ZBS) ili kukubalika katika soko kwa mujibu wa masharti ya nchi za Afrika na Kusini mwa Jangwa la Sahara.

"Shirika la Viwango la Zanzibar limepiga hatua kubwa ikiwamo mikakati ya kujenga maabara nne zenye uwezo wa kupima bidhaa mbalimbali za wazalishaji pamoja na wajasiriamali nchini kwa ajili ya kuingia katika soko," alisema.

# Waziri azungumzia umuhimu huduma ya maji

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Ardhi, Maji na Nishati, Salama Aboud Talib, amesema kuwa kulipia huduma ya maji kwa simu za mkononi ni kunaonyesha kwamba bidhaa ni haki ya msingi kwa kila binadamu.

Akizungumza katika maadhimisho ya Siku ya Maji yaliyoambatana na uzinduzi wa ulipaji maji kupitia mtandao wa simu ya TTCL (T-Pesa), alisema uwepo wa huduma hiyo malengo yake moja wapo ni kuiwezesha mamlaka ya majisafi na salama Zanzibar (ZAWA) kuwa na uwezo wa kujiendesha vizuri.

Alisema huduma hiyo pia itapunguza matumizi ya muda kwa wananchi kwa kutolazimika tena kufika vituoni kulipia huduma ya maji na wataweza kulipia kupitia simu zao za mkononi.

"Kwa upande wa wateja wetu utapunguza matumizi ya muda kwa kutolazimika tena kufika vituo vya malipo ya maji Zawa na badala yake mteja popote alipo atalipia na kumwezesha kuendelea na harakati zake nyengine za kiuchumi," alisema waziri huyo.

Aliwataka wananchi kutunza mazingira na vianzio vya maji katika maeneo mbalimbali ili kuwa na huduma endelevu ya majisafi na salama kwa muda wote.

Aidha, aliwapongeza wateja wote wanaolipia huduma ya maji bila ya kushurutishwa na kwa uwepo wa huduma hizo ni faraja kwao kwa kuwa unawapa ukaribu zaidi na mamlaka ya maji Zanzibar.

Hata hivyo alisema uwepo wa huduma za malipo kwa njia za simu za kiganjani ni sehemu ya utatuzi wa kero za maji na ni njia sahihi za kuimarisha huduma za maji Zanzibar sambamba na matumizi sahihi ya maji.

Alisema kila tone moja la maji ni gharama, hivyo kila mmoja atumie maji kwa uwangalifu na wale wanaopata huduma ya maji kulipia huduma hiyo bila ya kushurutishwa.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mkuu wa Kampuni ya Simu Tanzania (TTCL), Waziri Kindamba, alisema kuwa wataendelea kuboresha huduma za mawasiliano ili kwenda sambamba na wakati huu wa teknolojia.

Alieleza kuwa shirika hilo limejikita kuondosha usumbufu kwa wananchi ili serikali nayo iweze kukuza uchumi kwa haraka.

Maadhimisho hayo ya Siku ya Maji yaliyoambatana na uzinduzi wa huduma ya kulipia maji kwa simu ya kiganjani kupitia mtandao wa mawasiliano wa TTCL umefanyika jana katika viwanja ya Mapinduzi Sque Michenzani Zanzibar na kauli mbiu ya siku hiyo ni 'hakuna atakayeachwa bila ya huduma ya majisafi na salama'.




**AMBER LULU BORA UMEJIKUBALI**

Soma UK.15

Nipashe
MWANGA WA JAMII
BT
BURUDANI TELE

JUMAMOSI MACHI 23, 2019



# ALIPENDELEWA

## BASI SAWA



## Saida kumbe ulihama Dar?

KIFO cha Ruge Mutahaba kimevuruga mipango ya Saida Karoli kuendelea kuishi jijini Dar es Salaam, badala yake amuamua kujichimbia kikazi mkoani Mwanza.

Amesema Ruge alikuwa msaada mkubwa katika sanaa yake, lakini kifo chake kimevuruga kila kitu.

"Ruge alikuwa msaada mkubwa kwangu alipanga kunitafutia meneja wa kusimamia kazi zangu na kama angempata, ningehamia rasmi Dar es Salaam, lakini sasa amekufa siwezi tena kuhamia huko," amesema Saida.



## Wakazi ajiweka kati ya Nikki Mbishi, Fid Q

RAPA Wakazi ametoa ushauri katika ugomvi wa Nikki Mbishi na Fid Q, kuwa kila mtu hakuwa sawa katika ugomvi wao.

Amesema Nikki alikosea kutoa taarifa katika mitandao ya kijamiii kuwa hakupendezwa kitendo cha Fid Q kumpatia mtu bure albamu yake, jambo ambalo angeweza kumweleza pale walipokutana.

"Fid Q kutokana na tunavyomuheshimu naye si jambo zuri kutoa zawadi aliyopewa na kumpatia mtu mwingine bure, wote hawakufanya sawa lakini sijui kinachoendelea kati yao," amesema Wakazi.



# ALIPENDELEWA
# Beka afichua Yamoto Band

MSANII Beka Flavour ameamua kusema ya moyoni baada ya kueleza Yamoto Band, ilififisha nyota yake na badala yake alipendelewa Dogo Asley pekee.

Amesema baada ya kundi hilo kuvunjika na kuanza kufanya kazi peke yake, hali imekuwa tofauti kwa kuwa nyota yake imezidi kung'aa na jina lake limepata umaarufu zaidi tofauti na huko nyuma.

"Naona nyota yangu inaang'aa na nimekuwa miongoni mwa wasanii maarufu nchini, ninamiliki gari, nyumba na vitu vingine muhimu, vitu ambavyo sikuwa navyo nilipokuwa Yamoto Band," amesema Beka.

## INSTA-TWITTER





**Uzee** kudadadeki kha gym inanihusu mapaja yamekuwa...nitakomaa tu na watoto jamani-**Faiza Ally**



**Captain is** here Tanzania inakwenda fainali za AFCON 2019 nawaambia..afe kipa afe beki. Sasa msini-angushe basi Jumapili 24/03 twendeni tukaujaze uwanja-**Mwana FA.**



## Paschal Cassian alia 'Turudi kwa Mungu'

WAKATI mwimbaji wa Gospel, Paschal Cassian, akitua nchini India kwa ajili ya matibabu, ameamua kuwaachia mashabiki wake kibao kipya.

Mshindi huyo wa shindano la kuibua vipaji la Bongo Star Search mwaka 2009, ametambulisha wimbo wake 'Turudi' ambao unawakumbusha watu kumrudia Mungu wao.

Cassian anapambana kunusuru maisha yake baada ya kupata majeraha mabaya katika ajali ya gari aliyoipata mwaka jana.

UNASEMAAA...

# Kala kama wangekuelewa wasingerudia

RAPA Kala Jeremiah amefunguka kwamba anakerwa na nyimbo za baadhi ya wasanii zenye mwelekeo wa matusi akisema zinapotosha watoto.

"Wasanii wasifikirie pesa tu bali waangalie kile wanachokipeleka kwenye umma kama kina maadili, vinginevyo watakuwa na mchango mkubwa katika kukiharibu kizazi hiki kwa nyimbo zao za ovyo," amesema Kala.

Amesema wasanii ni kioo cha jamii na wanatazamwa na kuaminiwa, hivyo wawe makini katika tungo zao badala ya kuangalia pesa zaidi kuliko maadili.



BODA 2 BODA

# Flora uzazi unamfanya kuwa na subira



Mwanamuziki wa Injili, Flora Mbasha, amesema anatamani kurudi kwenye kazi yake, lakini malezi ya mtoto yanamkwamisha kufanya hivyo.

Akizungumza na BT, Flora amesema mtoto wake bado anahitaji kuwa karibu naye, hivyo hata kama anahitaji kurudi katika uimbaji inakuwa vigumu kwake.

"katika malezi ya mtoto kunahitajika ukaribu wa mama, nipo kwenye malezi kwanza na pale nikiona inatosha nitarudi nikiwa mpya na nyimbo nzuri za kumtukuza Mungu," amesema Flora.




**@burudanitele**

**>>> Usikose Jarida hili la Burudani Tele (BT) ndani ya Gazeti lako la Nipashe kila Jumamosi, pia lipo kwenye mtandao wa kijamii Twitter, tu' follow**

## INSTA-TWITTER


Tuffolow/ Tu-tag
**@burudanitele**



**Twendeni** wote tukaujaze uwanja kwa imani na madua ya kutosha tunawapiga awa wajukuu wa Iddi Amini-**Babu Tale.**



**Pamoja** na kwamba mimi ni Yanga damu haswa ila kwa Jumapili hii nasimama na Taifa langu. Tukaujaze uwanja na tuishangilie kwa makelele makubwa sana Taifa Stars-**Wema Sepetu.**



**Ungetaka** awe wa kwako peke ako ungemzaa wewe kwani sisi hatuna macho silembii-**Amber Lulu.**

# Kuumbe!

## AMBER LULU
### bora umejikubali mwaya



**Na Adam Fungamwango**

KWA kawaida binadamu wana tabia ya kukataa mambo ambayo huyafanya kwa siri na wakati mwingine hata yale yanayoonekana hadharani.

Mtu anaweza akawa anakunywa pombe, lakini ukimwambia anakataa, kuna wale waliobobea katika utumiaji dawa za kulevya na hata mwonekano na mwenendo unaonekana hivyo, lakini ukimwambia jambo hilo ataruka futi mia moja kukataa.

Huku kwa wasanii ndiyo kabisa, wengi wao wanakataa kila kitu, hata ukimkuta amekumbatiana na mtu kwenye hali ya kimahaba, lakini ukimuuliza atakataa na kukwambia siyo wangu.

Katika hali isiyokuwa ya kawaida, msanii na 'video queen' maarufu nchini Amber Lulu amekiri kuwa anatumia vipodozi vya kuifanya ngozi yake kuwa nyeupe maarufu kama 'mkorogo'.

Akasema mng'arisho huo wa ngozi yake huja na tenda ya kusaka losheni itakayomsaidia kutoa sugu au mbadala wa mkorogo utakaompa matokeo mazuri zaidi ya alioutumia awali.

Akabainisha kuwa hutumia gharama kubwa kuifanya ngozi yake kuwa mithili ya mzungu.

"Ndio natumia, rangi nyeupe naipenda nikifikia kuwa kama Sara, Mzungu wa Harmonize nitafurahi sana nahisi nitakuwa pambe," amesema."Mkorogo unanigharimu kwa sababu nanunua mafuta kuanzia shilingi 300,000 hadi 500,000 kwa mwezi, huu ukinikataa inabidi ninunue mwingine so ni kitu ambacho nakipenda," alisema.

Mara nyingi wasanii wengi wa kike na wa kiume hukataa kutumia vipodozi vikali vya kuwafanya kuwa weupe na kudai ni wa asili na wengine wakieleza eti wanakunywa maji mengi ambayo huwasaidia kung'aa.

Huu unaweza kuwa mfano mzuri kwa wasanii wengine, kwani mara nyingi ukweli ndiyo unakuweka huru.

Na wakati mwingine ili mtu asaidiwe ni lazima aseme kinachomtatiza au ugonjwa wake badala ya kuficha.

Mtu anayeficha ugonjwa hawezi kupata dawa kwa sababu hataki watu wajue kuwa anaumwa.



## 'WACHAWI' BONGO MUVI HAWA HAPA



**Na Mwandishi Wetu**

DUNIANI kote, waigizaji hutengeneza filamu kutokana na maudhui na utamaduni wa nchi husika, mila na tamaduni za watu wake.

Mfano za kizungu utakutana na maudhui na tamaduni za kizungu, za Kihindi halikadhalika utakutana na mitazamo, mikasa na visa inavyopatikana huko kutokana na tamaduni zao ambayo huwezi kuipata kwingine.

Afrika pia ni hivyo hivyo. Na kwa bahati nzuri, tamaduni za Kiafrika nyingi zinafanana na hata dhana.

Kuna dhana kwenye Bara la Afrika kuwa kuna watu ambao usiku kazi yao kubwa ni kuchukua watu na kwenda kuwafanyia kazi zao mbalimbali, ikiwamo kuwalimisha mashamba, maarufu kama msukule.

Pia kuna dhana kuwa wakati mwingine mtu anaumwa au kufa si kwa sababu ya magonjwa ya kawaida, bali ni kulogwa.

Na kwa maana hiyo, watu wenye tabia ya kuroga wenzao kuwatesa au kuwaua wanaitwa wachawi.

Dhana hii isiyofutika kirahisi, imekuwa ikirithiwa vizazi hadi vizazi na kuaminiwa na watu wengi hata ambao wanaonekana wameendelea au kuelemika hadi leo.

Na kwa sababu kuna dhana ya wachawi, pia kuna watu anaodai kuwatibu watu wanaopata matatizo hayo kwa kulogwa, wao wanaitwa au kujiita waganga wa kienyeji.

Kutokana na dhana hiyo, hata waigizaji wetu wamekuwa wakitengeneza filamu zao na kuonyesha dhana hiyo ili kuweka uhalisia wa maisha halisi ya jamii zetu za Kitanzania na Kiafrika yanavyokuwa wakati mwingine.

Kwenye filamu za Kitanzania wapo wasanii ambao pamoja na kucheza nafasi nyingine nyingi, lakini wamejipambanua kucheza kwenye nafasi za 'wachawi' ili kuonyesha uhalisia wa dhana hiyo.

Na baadhi yao wamekuwa wakicheza kwa ustadi mkubwa.

**Fatuma Makongoro 'Bi Mwenda'**

Msanii huyu wa siku nyingi, ameanza kusikika tangu mwanzoni mwa mwaka 2000 na kujinyakulia umaarufu kwa kucheza sehemu ya aina hiyo.

Pamoja na kwamba ana uwezo wa kucheza kwenye vipengele mbalimbali anavyopangiwa, lakini ukitaka kuona uwezo wake awekwe eneo la kucheza kama mshirikina.

Alishawahi kusema kuwa huko nyuma kuwa awali hata njiani alikuwa akiogopwa anapopita akidhaniwa kuwa ana tabia hiyo, kutokana na kucheza kwa makini na uwezo wa hali ya juu.

Mashabiki wengi wa bongo movie wanadai kuwa hakuna msanii yoyote nchini anayeweza kucheza eneo la 'kichawi' na kusisimua watazamaji kama Bi. Mwenda.

**Msisili wa Msisili**

Ni msanii mkongwe aliyejipambanua kwenye maeneo mawili tofauti.

Huyu utamfaidi zaidi akicheza kama mfalme au mmoja wa watemi kwenye himaya za makabila mbalimbali nchini waliopata kutawala miaka mingi iliyopita kabla ya Uhuru.

Lakini pia huweza kucheza kwa uwezo wa hali ya juu kama mchawi, akiwakilisha zilezile dhana za vizazi vya Kiafrika ambavyo baadhi vinaamini kuwa kuna watu kama hao wapo kwenye jamii na maisha yetu ya kawaida.

**Hamisi Kolongo**

Huyu pia ni mmoja wa waigizaji wakongwe nchini. Mbali na kuweza kuigiza kama mzee wa kawaida, lakini baadhi ya filamu zake za kusisimua amecheza kama mchawi.

Amekuwa na uwezo wa kuwafanya watazamaji kusisimkwa anapoigiza eneo hilo, na wakati mwingine huigiza kama ni mkuu wa wachawi, huku upande wa pili akiwa ni mzee mwenye heshima, hekima na busara kwenye maisha ya kawaida, kiasi kwamba inakuwa ni ngumu kudhani kuwa usiku anaongoza jopo na wachawi.

**Mohamed Fungafunga 'Jengua'**

Huyu anasifika sana kuigiza sehemu ambazo anasimama kama baba au mume mkali, mwenye msimamo mkali, ambaye anaongoza familia kwa amri na 'mkono wa chuma'.

Na amekuwa akiitendea sehemu hiyo haki na kubaki na nembo hiyo kila anapoonekana mbele ya watazamaji.

Lakini kwa upande wa pili, Mzee Jengua pia ni 'mtaalamu' wa kucheza sehemu zenye dhana ya uchawi.

Amepata kucheza filamu mbalimbali za hivyo na kufanya vizuri.

**Chuchu Hans**


Msanii huyu wa kike yeye ni tofauti kidogo. Badala ya kuigiza dhana ya uchawi wa Kiafrika, yeye hucheza zaidi kwenye dhana za uchawi ulio kwenye utamaduni wa Kiarabu, yaani majini.

Kifupi hucheza kama jini kwa baadhi ya filamu zake. Na amekuwa akiitendea haki kazi yake hiyo na kuwakumbusha wengi hadithi za zamani za Kiarabu za Alfu Lela Ulela ambazo karibuni zote zilikuwa hazikosi kuwa na viumbe wa aina hiyo.

Bi Mwenda



Msisili



Kolongo



Jengua



Chuchu Hans

# Vijimambo

## PICHA ILIYOPITA



1. Pole sana jamaa wa baiskeli, itakuwa ni adhabu - Sininyo.
2. Akiongeza na uchawi, atalivuta - Robi Moshi.
3. Nikiwatazama tu najua nyie wote chenga - Majuto Magazeti, Miyomboni Iringa.
4. Kama mkilivuta hilo, najua mtakuwa mnatoka mkoa fulani - Majuto Magazeti, Miyomboni Iringa.
5. Hapo lazima liondoke tu, usicheze na Sumbawanga - Mama Nah, Manzese DSM.
6. Mkisikia bonge nyanya sio kila kitu, vingine havijaribiwi nyinyi - Kibena, Buguruni DSM.
7. Na bado mwaka huu machizi wataongezeka sana - Majuto Magazeti, Miyomboni Iringa.
8. Hata kama mmekunywa supu ya pweza, hilo hamliwezi ng'ooo! - Baiya Mponde, Sinza DSM.
9. Milembe lazima itakuwa inawaita hao jamaa. Khaaa! - Baba Juma, Mtongani Kunduchi DSM.
10. Ongeza kasi kidogo, limeshaanza kusogea - Beneali Moussa Beneali, Migombani Zenji.
11. Acha kamba, katoe 'hand break' nikushtue - Shirima, Morogoro.
12. Hapo ndipo tunasema 'mbuzi kafia kwa muuza supu' - Agatha Mbale, Moro Town.
13. Leo nimepewa nafasi ya kuonyesha uwezo wa baiskeli yangu, acha waone - Michael Mbatta, Makumbusho DSM.
14. Ule uchawi niliofundishwa na babu hapa ndio pa kujaribia kama unafaa - 0758 148 508.
15. Duuuh, sio kawaida! Atapigwa mawe - Diana Martin, Singida.
16. Duuuh! Kweli sawa na kutwanga maji kwenye kinu - Damuu, DSM.
17. Jamaa mbunifu wa wakati wake - Hamis J. Kuchanga, Tambani Mkuranga.
18. Nakuvuta mpaka liwake, lakini utanipa elfu 70 - Mfaume Mbugi, Mshindo Iringa.
19. Japokuwa linajifanya zito kusogea, hapa ndio Giningi, litawake tu - Moussa Beneali, Migombani Zenji.
20. Acha uvivu wewe, mwenzio kavuta gari kala hilo kwa mkokoteni tu - Job Mbunda, Msamala Songea.
21. Stua basi, ntaacha kukuvuta. We lete mzaha tu - Anitha Bwege, Tandika DSM.
22. Mateja si mchezo, hapo akili zao zinawatuma kupata hela ya 'unga' tu - Bina, Kijiweni Sinza DSM.


**SMS Bomba ya Leo:**

**Ule uchawi niliofundishwa na babu hapa ndio pa kujaribia kama unafaa - 0758 148 508.**

## PICHA MPYA



**TUMA MESEJI - 0773 477 311**




# Ndoa inapovunjwa na wanandoa

**Na Adam Fungamwango**

HAKUNA mtu yeyote duniani mwenye uwezo wa kuvunja ndoa ya mwenzake. Anayevunja ndoa ni mwanandoa mwenyewe.

Hitimisho la talaka linatokana na kusikiliza maneno ya watu, uzembe au kutotekeleza yanayotakiwa kwenye ndoa.

Mwanandoa yeyote ambaye hapelekwi kama gari bovu na wapambe au watu wa nje, ni aghalabu sana ndoa yake kuyumba, achilia mbali kuvunjika.

Hebu tuangalie filamu hii ya 'Kamanda Mstaafu' jinsi mke alivyokuwa akilazimisha kutaka kuivunja ndoa yake mwenyewe kwa sababu za kijinga kabisa.

Imechezwa na Jacob William 'Ringo', Asha Boko, Jumanne Alela 'Mzee Matata', Martin White 'Tin White', Mohamed Salehe, Habibu Mrisho na wengine.

Inaanza kwa kumwonyesha Ringo akiwa amelala kwenye kituo cha basi. Rafiki yake Tin anamkuta na kumuuliza kulikoni? Anamwambia hayo yote anayesababisha ni mkewe kwa kuwa amekuwa akinyanyasa kwa kumnyima chakula na kumpiga kila kukicha.

Tin anampa rafiki yake pesa ya kula na kumtaka arejee nyumbani.

Njia anakutana na mshenga wake mzee Matata. Naye Ringo anajaribu kumwelezea masaibu yote anayokutana nayo kwenye ndoa. Matata anaamua kuongozana naye hadi nyumbani kwake. Kufika tu anashuhudia mwenyewe kwa macho yake Ringo akipokea kisago kutoka kwa mkewe ambaye ni Asha Boko.

Mke anampiga mumewe huku akijitapa kuwa yeye ni kamanda mstaafu, hivyo hababaishwi na mtu yoyote yule.

Siku moja Ringo anakutana na mshenga wake Matata ili kujadili mustakabali wa ndoa yake, ili asiendelee kunyanyaswa, lakini mpango huo ulishtukiwa na Asha Boko na alipofika alimkuta mumewe, akampiga hadi kumvunja mkono.

Kitendo hicho na vingine huko nyuma viliwakera mno majirani na kuamua kuingilia kati, lakini na wao waliambulia vipigo kabla ya kutimua mbio. Hali ikazidi kuwa mbaya. Ringo akaamua sasa anywe sumu ili kujiua. Kabla hajafanya hivyo, aliitwa mjumbe wa nyumba kumi ambaye alifanikiwa kumzuia. Mjumbe alichofanya ni kumpigia simu mjomba wa Asha Boko.

Alipofika hapo alisimuliwa visa vyote ambavyo mpwawe anamfanyia mumewe. Kumbe huyo mjomba ndiye aliyemfundisha ngumi na karate Asha akiwa bado mdogo. Mjomba aliposikia hivyo alikasirika na kuanza kumfokea mpwawe Asha Boko. Akamwambia kuwa alimfundisha sanaa za mapigano kwa ajili ya kujilinda na si kunyanyasa watu mitaani, hususan mumewe wa ndoa anayepaswa aishi naye kwa upendo na mahaba. Asha Boko alinywea na akaomba msamaha, akaahidi kuwa hatorudia tena na atampenda mumewe.

**Simu 0716 350534.**
**afungamwango@gmail.com**



# MCHUNGAJI DMX SOMA HIYOO!

WAKATI mkali wa nyimbo za RnB, R.Kelly, anapambana kufa na kupona kuepukana na kifungo kutokana na kutuhumiwa kuwanyanyasa kingono wasichana wenye umri mdogo, mkongwe mwenzake katika muziki DMX, yupo huru baada ya kutumikia kifungo chake.

Wiki hii DMX ameamua kutoka hadharani tangu kutoka jela mwezi Januari, mwaka huu, lakini msanii huyo amekuwa na mwonekano mpya na kuwa kama mchungaji kutokana kufanya maombi mazito ndani ya nyumba ya Kanye West.

Rapa huyo alialikwa nyumbani kwa West katika maombi ya Jumapili iliyofanyika nyumbani kwake mjini Los Angeles, Marekani.

DMX alikuwa ni moja ya watu walioshusha maombi kwenye ibada hiyo, ambapo aliiombea jamii ya watu weusi na kumshukuru Mungu kwa kumwepusha na majanga mbalimbali aliyopitia siku za nyuma.

Kwenye video iliyosambaa kwa kasi katika mitandao ya kijamii, msanii ambaye alifungwa baada ya kukutwa na kosa la kukwepa kodi, alionekana akitoa maneno ya kiimani, huku akiporomosha maombi ya nguvu kama wachungaji wengine wanavyofanya.

Alielezea janga lake la kukwepa kodi lilivyomyumbisha hadi kupata dhamana mwezi Januari mwaka huu, huku akiwataka watu kujikabidhi kwa Yesu kwani ndiye kimbilio.

Maisha ya DMX (49) yamekuwa na misukosuko toka tangu miaka ya 2010, ambapo alishawahi kukutwa na skendo za kutumia dawa za kulevya.

Rapa huyo baba wa watoto 15 na amekuwa akiandamwa na matumizi ya dawa za kulevya.

Kwenye video hiyo, amekiri kuwa kwa sasa hawezi kurudia tena maisha yake ya zamani na ataendelea kumtumikia Mungu.

Misukosuko imezidi kuwakumba wanamuziki weusi wa Marekani na kujikuta wakishuka kisanii. Bado mashabiki wa muziki wanafuatilia mwenendo wa kesi ya R.Kelly licha ya mwenyewe kusimama imara kutokana na tuhuma hizo akidai zimepangwa kwa makusudi maalum.




# Maombi yenu tu kwa Justin Bieber



KIZA kimetanda kuhusu ndoa ya mwanamuziki wa pop, Justin Bieber na mpenzi wake Hailey Baldwin, baada ya familia kuisogeza mbele.

Ndoa hiyo iliyokuwa ifungwe ndani ya mwezi ujao, lakini taarifa za kushtua zimetolewa na kueleza hakutakuwa na ndoa hiyo hadi hapo pale itakapotolewa maelezo mengine.

Taarifa iliyotolewa na watu wa karibu na 'couple' hiyo kupitia mtandao wa TMZ umeripoti kuwa wapenzi hao wamelazimika kuipeleka mbele ndoa yao kwa sababu za kiafya anazokabiliana nazo Bieber.



## Drake watu wanataka burudani si maneno

RAPA kutoka nchini Canada ambaye amehamishia makazi yake Marekani Aubrey Drake Graham almaarufu Drake, amelazimika kuiahirisha shoo katika Jiji la Amsterdam nchini Uholanzi.

Onyesho hilo la muziki katika Jiji la Amsterdam ambalo lilitarajiwa kufanyika tarehe 23 Aprili, limefutwa kwa mara nyingine, kutokana na mwanamuziki huyo kubanwa na ratiba.

Hata hivyo, Drake amepanga shoo hiyo ifanyike Aprili 25 na 26, kulingana na tovuti ya Ziggo.

## Adesua waambie utamu wa embe anaujua mlaji

MWIGIZAJI nyota kutoka Nollywood, Adesua Etomi, amejibu tuhuma zinazotolewa na watu mbalimbali kutokana na picha yake kupamba jarida maarufu la Vogue.

Baadhi ya watu wametoa maoni yao kuhusu picha hiyo na kueleza inafanana na enzi ya utumwa kutokana mwonekano wake.

Adesua Etomi akijibu maoni hayo amesema anajivunia kuwepo katika jarida hilo na kueleza fursa hiyo ni muhimu kwa nchi ya Nigeria kutokana na kuwa mmoja wa wasanii waliotambuliwa ulimwenguni.





## Omoni we ndio malkia wa nguvu

MKALI wa filamu nchini Nigeria, Omoni Oboli, amekuwa mwanamke wa mfano baada ya kujitokeza katika mitandao ya kijamii kujivunia na kueleza watoto wake watatu sawa na kumiliki kila kitu.

Omoni ambaye anatajwa kuwa ni msanii anayependwa na mashabiki wa filamu nchini humo, kutokana na maisha yake. Ni jambo la kawaida kwake kuweka video fupi ikimwonyesha akicheza muziki na mume wake pamoja na watoto wake wa kiume.

## Jay Z aweka rekodi nyingine Marekani

RAPA maarufu Jay-Z amevunja rekodi baada ya albamu yake 'The Blueprint' kuingizwa katika makumbusho ya taifa eneo ambalo huhifadhiwa kazi bora za wasanii zilizoegemea kiutamaduni, ubora wa mpangilio na historia.

Album ya The Blueprint iliyotoka Septemba 11, 2001, inatajwa kuwa bora zilizowahi kufanya vizuri kwa muda wote duniani.

Inaelezwa kuwa album hiyo iliachiwa rasmi sawa na siku ambayo Marekani ilipata shambulio la kigaidi 'Septemba 11' na kusababisha vifo vya maelfu ya wananchi wa Marekani katika jengo la Twin Towers.



SAFU



Na John Juma
0716217615

**Mionzi ya Sheria**

# Wasomi tujifunze kwa Waziri Jafo-2

WIKI iliyopita tulichapisha sehemu ya kwanza ya makala hii iliyoshauri watu kujifunza kwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Seleman Jafo.

Anayezitaka taasisi zinazosimamia mifumo ya elimu kuacha kuweka vikwazo na masharti magumu kwa vijana wenye ufaulu mdogo kuendelea na kozi wanazodhani wanaziweza.

Anatoa kauli hiyo Ijumaa, Machi 08, 2019, wakati akizindua mpango wa elimu changamani kwa vijana walio nje ya mfumo rasmi wa elimu (IPOSA). Anasisitiza kuwa kukwamisha vijana wenye ufaulu mdogo kuendelea na kozi mbalimbali kwa vigezo vya kuwa na ufaulu wa chini ni kuwanyima vijana haki ya kupata ujuzi.

"Tuache kuweka mifumo yenye roho mbaya inayokwamisha vijana kielimu na ndoto zao za kushiriki maendeleo ya taifa na kujenga uchumi," anasema.

Akiongeza zaidi anasema suala hilo linachochewa na uwepo wa baadhi ya wataalamu wanaokaa tu maofisini na kuweka au kupitisha vigezo ambavyo vinalenga kukwamisha vijana kuendelea na mafunzo zaidi yakiwamo ya ufundi, hatua ambayo itasababisha siyo tu kuwanyima fursa adhimu ya kushiriki moja kwa moja katika ujenzi wa uchumi wa viwanda, bali hata pia haki yao ya msingi ya kupata elimu kama Ibara ya 11 (1) - (3) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977, inavyosisitiza umuhimu wa elimu.

Pamoja na maofisa hao, suala jingine ambalo ni kikwazo kwa wasomi wa Tanzania ni mienendo ya wahadhiri ambao huwahujumu wanafunzi. Huwafelisha mitihani badala ya kuwasaidia, lakini pia mifumo ya wanafunzi waliofeli kuomba rufani ni ya kizamani na kikandamizi kiasi kwamba haimsaidii mwanafunzi anayelalamika.

Kwa mfano utasikia sifa za kijinga wanazovishwa mafisadi wa elimu katika vyuo vikuu. "Profesa fulani, yule bwana kiboko, kila mwaka wanafunzi kadhaa lazima washindwe kumalizia kwa ajili yake, ikitokea amekukamata kwenye somo lake...bora tu mapema umfuate umuombe kwenye mtihani wa marudio asikung'ang'anie," huku ni kuhujumu elimu.

Tukumbuke na tena tuweke akilini kuwa wahadhiri nao ni binadamu. Tujiulize swali hili dogo hivi mahakamani mahakimu na majaji wangeachwa huru kiasi hicho watumie utaratibu kandamizi kama huu hasa zinapobadilika rufani kutoka mahakama za ngazi za chini, bila ya mrufani kuwa na haki ya kuomba na kupatiwa nakala ya hukumu kama kiambatanisho muhimu kwa taratibu za rufani, hatima ya haki kwa washtaki na washtakiwa ingekuwaje?

Ni wakati wa wasomi kubadilika, ili wawe chachu ya mabadiliko chanya ndani ya jamii, wawaenzi kwa heshima waasisi wa taifa hili Mwalimu Julius Nyerere na Abeid Amani Karume, kwa kuwa wangekuwa na choyo, chuki na ubinafsi leo hii uhuru, amani na utulivu visingekuwapo na elimu ya vyuo vikuu kama Dar es Salaam, Sokoine, Taasisi za Ufundi za Dar es Salaam na Arusha, zisingekuwapo na pengine, mambo mazuri yaliyoko nchini leo yangesikika kwa majirani, iwapo viongozi wangekuwa wabinafsi.

Ukandamiza kwenye elimu unasababisha watoto wa maskini leo hii, ambao daima Baba wa Taifa aliwatazama kwa jicho la huruma, wanalazimishwa kuishi kitumwa katika nchi yao na baadhi ya wahadhiri wenye choyo cha elimu kwa sababu zao binafsi.

Hofu na huruma ya Mungu ishuke kwa walimu hao wa elimu ya juu. Kwa mfano binti au mwanafunzi mpaka anapata nafasi ya kufikia kuweza kujiunga na masomo ya elimu ya juu amepambana sana, ameishi kwa shida, ameumizwa na njaa, dhiki na shida vyote vilikuwa upande wake. Hata wakati mwingine iliwalazimu wazazi au walezi wake kuuza baadhi ya mali kumudu kulipia gharama za masomo yake.

Lakini mwisho wa siku, akiwa mwaka wa mwisho wa masomo au katikati ya safari kufikia malengo yake, pengine kwa somo moja tu anafelishwa kwa makusudi kabisa bila hata ya msingi kwa sababu binafsi za mhadhiri.

Niulize, hivi Watanzania mtakejeli na kufumbia macho "wizi huu au hujuma hizi za kitaaluma mpaka lini?" Wasomi kote Tanzania waamke kuunga mkono "Fikra za Kimapinduzi" alizothubutu kuzionyesha Waziri Jafo. Kwa sababu tusipokuwa makini mambo hayo yataligharimu taifa.

Mamlaka husika zenye dhamana na kusimamia maadili na elimu, ziache kuendesha mambo haya kwa mazoea. Wahadhiri nchini wasiachwe kwa muda mrefu kufurahia madaraka mapana sana. Hii inapelekea baadhi yao kuyatumia vibaya kwa sababu zao binafsi.

Ni dhahiri, bila kificho, kutokana na choyo na chuki binafsi, taifa kila mwaka linapoteza "nguvu kazi ya wasomi" ambayo ingesaidia kuinua uchumi wa familia, jamii zao na taifa kwa ujumla. Endapo kwa namna moja au nyingine wasingekwamishwa kufikia ndoto za kuwa wasomi wa elimu ya juu.

Hii siyo mara ya kwanza, kuandika na kushauri juu ya kero na changamoto wanazozipitia wanafunzi wa elimu ya juu nchini, hususan vyuo vikuu vya serikali.

Ni ushauri wa wengi kuwa ni wakati wa kutunga sheria kuwawajibisha wahadhiri mafisadi wa nguvu kazi ya taifa ili washtakiwe kwa kuhujumu uchumi.



Reubeni Lumbagala

**Kalamu ya Mwalimu**

# Mkono wa serikali uwafikie wabunifu wasiorasmi vijijini

DIRA ya Maendeleo ya Tanzania inaelekeza kuwa ifikapo mwaka 2025, Tanzania iwe ni nchi ya viwanda na ya uchumi wa kati. Juhudi kubwa zinaendelea kufanywa na serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi na wadau wa maendeleo ili kuhakikisha kuwa azima hiyo inafanikiwa.

Uchumi wa viwanda unategemea sana mchango wa wabunifu ambao ni nyenzo muhimu katika kufanikisha jitihada hizo. Kama wabunifu waliopo katika shule, vyuo na wale waliopo mitaani watatumika kikamilifu, ni dhahiri mwelekeo wa nchi utakwenda vizuri na kufika kule dira inapotaka.

Wabunifu wengi hutumia sayansi na teknolojia, hivyo, serikali ina wajibu mkubwa wa kuhakikisha masomo ya sayansi yanawekewa mkazo na umuhimu wa kipekee ili wanafunzi wengi wasome masomo hayo kwa lengo la kutoa mchango kwenye ujenzi wa uchumi wa viwanda.

Kama wanafunzi wengi shuleni na vyuoni watasoma sayansi ambayo ni nguzo muhimu katika uchumi wa viwanda, kasi ya ubunifu itaongezeka na suala la kufikia uchumi wa kati litapata msukumo mpya.

Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi) zishirikiane ili kuhakikisha wanafunzi waliopo katika shule za msingi, sekondari, vyuo vya kati na vikuu wanahamasishwa kuwa wabunifu wa vitu mbalimbali ili kuchangia jitihada za kuifikisha Tanzania kwenye uchumi wa viwanda.

Machi 7 mwaka huu, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Joyce Ndalichako, alitoa wito kwa wanafunzi na wabunifu kuibua kazi mbalimbali ili kusaidia maendeleo ya uchumi wa viwanda. Waziri Ndalichako alitoa wito huo katika kilele cha Mashindano ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu, ambapo kauli mbiu ya mashindano hayo ilikuwa ni "kukuza ujuzi na ubunifu kwa uchumi wa viwanda".

Kauli mbiu hii inaonyesha umuhimu wa kupata ujuzi kwanza ili utumike katika kubuni vitu mbalimbali na hatimaye kuchangia katika maendeleo ya viwanda. Hivyo basi, ni vyema Watanzania ambao ni wadau muhimu wa kuijenga nchi kujielekeza katika kutafuta maarifa na ujuzi katika taasisi mbalimbali zinazotoa elimu ili waitumie kubuni zana, mashine na mitambo mbalimbali kufanikisha kufikia mafanikio ya uchumi wa viwanda.

Katika mashindano hayo, Ndalichako, anawahakikishia washindi kuwa wataendelezwa ili waweze kukuza tafiti na ubunifu wao kuchangia maendeleo ya nchi. Pia anatoa wito kwa wabunifu kubuni vitu vitakavyorahisha shughuli mbalimbali.

"Ninatoa wito kwa wabunifu kujikita kwenye kuangalia namna gani wanarahisisha shughuli zinazofanyika katika mazingira yao. Ikumbukwe ubunifu hauna umri na hauchagui kwa sababu mwisho wa siku mkono unaenda kinywani."

Njia mojawapo ya kukuza ubunifu ni kuandaa mashindano ya ubunifu kwa wanafunzi katika sayansi na teknolojia kwenye shule zote za msingi, sekondari hadi vyuoni hapa nchini. Wale watakaoandaa kazi bora zaidi watambuliwe na wapewe zawadi na vyeti maalum kutambua uwezo wao kiubunifu.

Mashindano hayo pia yanaweza kuvuka mipaka kwa kushindanisha ubunifu kutoka shule moja na nyingine au chuo na kingine ili kukuza ubunifu zaidi miongoni mwa wanafunzi.

Nje na taasisi za elimu, wapo wabunifu waliopo mitaa na vijijini ambao serikali haiwatambui na baadhi yao hawana elimu au wana viwango vidogo, lakini wamejaliwa vipaji vikubwa vya kubuni vitu mbalimbali. Hawa nao wanapaswa kupewa kipaumbele kikubwa katika ujenzi wa uchumi wa viwanda.

Katika halmashauri ni wakati wa kuanzisha dawati maalum la kupokea kazi mbalimbali za wabunifu ili waweze kuendelezwa na kazi zao zichangie katika maendeleo ya nchi. Kwa kutowapa fursa za kutambua wabunifu nje na mifumo rasmi ya kiserikali, nchi itapoteza wataalamu wengi wenye ubunifu unaohitajika sana katika kipindi hiki muhimu.

Wabunifu wakithaminiwa kwa kuendelezwa na kuwezeshwa katika tafiti zao, wengi watashawishika kujikita katika kubuni vitu mbalimbali. Ni wakati wa Tanzania kuwa na uwezo wa kutengeneza mashine zake yenyewe zikatazotumika viwandani badala ya kuziagiza kutoka nje ya nchi.

Vyuo vya Mafunzo ya Ufundi (Veta) na Idara za Masomo ya Sayansi na Teknolojia katika vyuo vikuu nchini zipewe ruzuku ya kutosha itakayofanikisha utekelezaji wa utafiti na uvumbuzi wa mitambo mbalimbali inayohitajika kufikia maendeleo ya viwanda.

Utamaduni wa kutiana moyo pamoja na kupongezana miongoni mwa wabunifu upewe msukumo mkubwa ili wagunduzi hawa wasikatishane tamaa katika kazi zao. Kama nchi Watanzania washirikiane katika kuhakikisha kazi za kibunifu zinaendelezwa ili nao wachangie maendeleo ya viwanda na hatimaye kufikia uchumi wa kati.

Reubeni Lumbagala ni Mwalimu wa Shule ya Sekondari Mlali iliyoko Wilaya ya Kongwa mkoani Dodoma.

**Maoni: (+255) 764 666349.**



Na Elizabeth Zaya

NYUMBA YANGU

# Je, unapolala panakuvutia?

CHUMBA cha kulala katika nyumba ni miongoni mwa vitu muhimu kwa ustawi wa maisha ya binadamu.

Hili ni eneo muhimu ambalo linaweza kuweka akili sawa za binadamu na ikamsaidia kuendesha shughuli zake kwa ufasaha zaidi.

Kutokana na umuhimu wa chumba hiki katika maisha ya binadamu, kuna haja ya kupewa kipaumbele zaidi tofauti na ilivyo kwa vyumba vinginevyo, kwa kuhakikisha kwamba kinakuwa na vitu vya muhimu ambavyo kwa namna moja ama nyingine vinaweza kuimarisha utulivu wa akili.

Inafahamika kwamba chumba kilichokamilika lazima kiwe na sehemu ya ukuta, mlango, dari na dirisha lakini mbali na hivyo, vipo vitu vingine ambavyo vinaweza kukikamilisha zaidi.

Makala hii inaangalia vitu muhimu vinavyohitajika ndani ya chumba hicho cha kulala ambavyo vitakifanya kionekane kwamba kimekamilika.

Chumba ambacho kwa lugha yako mwenyewe unaweza kukipa heshima ya kipekee unayoona inafaa kwako. Ni vema kujenga taswira yako kichwani kwanza juu ya aina na namna unavyohitaji kiwe hata kabla ya kufanya uamuzi wowote ule.

Jambo la kwanza ambalo linapaswa kuzingatiwa katika chumba cha kulala ni kitanda na godoro.

Hili ni eneo muhimu kwa kuwa kabla ya kufanya uamuzi wa kununua na kuweka katika chumba unapaswa kutulia na kutafakari ni aina gani au muundo gani unahitaji kadri ulivyopangilia kukitengeneza.

Hakikisha haufanyi makosa katika kipengele hiki cha uchaguzi wa kitanda na gorodo.



Jambo la pili ambalo unapaswa kufanya ni uchaguzi wa aina ya mashuka na mito inayoendana na aina au muundo wa kitanda husika, fanya haya yote kwa kuzingatia picha au taswira ya aina ya chumba unachohitaji kutengeneza.

Si jambo baya kuwa na mito kuanzia miwili hadi sita au zaidi ya hiyo kulingana na ukubwa wa kitanda lengo ni kuigawanya kupata ya kutumia wakati wa kulala pamoja ya mapambo.

Zulia nalo katika chumba huongeza mvuto kwa kiwango kikubwa, hivyo katika muundo wako wa chumba unaweza kuangalia namna ya kuliwekea bajeti.

Kumbuka kwamba hakuna sakafu inayoweza kuburudisha miguu peku unapotoka kuamka asubuhi kuliko ya zulia, si vibaya kama hili nalo likazingatiwa na ili kutengeneza hatua ya mwanzo wa siku kuwa ya burudani.

Hata kama huwezi kununua zulia la kutosha chumba kizima, lakini unaweza kuweka hata nusu yake pembezoni mwa kitanda.

Jambo jingine ambalo linafaa kwenye chumba hiki cha kulala ni sehemu ya kuketi ambalo linaweza kusaidia kulitumia kuketi na kusoma kitabu au mazungumzo kabla ya kulala kitandani.

Eneo hilo linaweza kutumika pia kunyanyulia miguu wakati wa kuvaa soksi au nguo pamoja na kuwekea mapambo yanayotumika kupambia kitanda wakati wa usiku yanapotanduliwa badala ya kuweka chini.

Sanaa na picha katika chumba nayo ni muhimu japokuwa unatakiwa kuhakikisha unaweka zile muhimu na zinazokuvutia na kuepuka kuwa na mrundikano wa picha hizo.

Ni vizuri kukumbuka kwamba vitu vichache unavyovipenda eneo unaloviona kwa muda mrefu husaidia kuongeza furaha na utulivu wa akili na hata kupata usingizi mwororo.

Na kwa wale wanaopendelea kuamka usiku na kusoma neno la Mungu, si vibaya kuweka pembeni ya kitanda kunakoelekezwa kichwa, taa hafifu ambazo haziwezi kumsumbua mwingine hasa wenye wenza wao.

Taa hizi pia hutumika kama mapambo ya kupendezesha chumba kumbuka ili kikamilike, pia kinatakiwa kiwe na mapazia.

Ni muhimu kukumbuka kwamba chumba cha kulala kinahitaji kiwe cha faragha, kwa hiyo kinahitaji kuwekwa pazia sahihi kulingana na uhitaji wa kifaragha.



MAKALA

# Kompyuta yaanza kufikiri kibinadamu

Na Gaudensia Mngumi

KITAALAMU teknolojia hii huitwa Artificial Intelligence (AI) ambayo ni jihudi za wanasayansi wa kompyuta kuifanya kompyuta iweze kujifunza kama binadamu wanavyojifunza.

Niseme hivi: "It is an attempt to build computing machines or programs that mimic reasoning of human."

Ni maelezo ya Dk. Katule Ntwapichani, ambaye ni mhadhiri katika Idara ya Mifumo ya Kompyuta na Hisabati ya Chuo cha Ardhi, jijini Dar es Salaam, anapozungumza na Nipashe kuhusu utaalamu huo mpya wa kuifanya 'kompyuta kuwa kama mtu.'

Awali Dk. Ntwa alitoa maelezo yake kwenye Siku ya Maadhimisho ya Miaka 55 ya Ushirikiano wa Kiufundi na Kiuchumi baina ya India na Mataifa ya nje ikiwamo Tanzania, hafla ya ushirikiano huo unaojulikana kama India Technical and Economic Cooperation (ITEC) , ilifanyika katika Ubalozi wa India Dar es Salaam na kuwapa nafasi walionufaika na mpango wa ushirikiano kuelezea wananchi jinsi walivyonufaika.

Dk. Ntwa, akiwa miongoni mwa waliosoma utaalamu wa kisasa wa kompyuta baada ya kueleza kwa ufupi kwa washiriki, anafanya mahojiano na Nipashe na kueleza zaidi juu ya utaalamu wa 'Artificial Intelligence' na jinsi unavyoweza kutumika hapa nchini.

Anaendelea kueleza kuwa kawaida wanasayansi wanapotaka kompyuta ifanye kazi fulani lazima waiwekee programu. Ndiyo maana kuna msemo kuwa 'garbage in garbage out'.

Na programu huandaliwa na wataalamu wa programu za kompyuta, kwa njia hii hawaifunzi kompyuta bali wanaiwekea maelezo ya nini cha kufanya.

"Kwenye Artificial Intelligence badala ya kuipa kompyuta maelezo ya nini cha kufanya, tunaipa mifano ya kitu fulani halafu kupitia hiyo mifano kompyuta inapata maarifa ya jinsi ya kufanya kitu hicho tunachokikusudia," anafafanua Dk. Ntwa.

Mtaalamu huyu anafafanua kuwa lengo ni kuiwezesha mashine hiyo inapokutana na mfano ambao haijawahi kufundishwa au kuonyeshwa, iweze kutumia utaalamu 'knowledge' iliyonayo kusema na kuona kwamba hiki ni kitu fulani au hapa kuna uwezekano wa kuwepo kitu fulani.

Moja ya maeneo maarufu ya 'artificial intelligence' ni kwenye utaalamu wa 'machine learning.'



Dk. Katule Ntwa



Balozi wa India nchini Sandeep Arya, Ubalozi wa nchi hiyo ndio unaoratibu mafunzo ya sayansi na teknolojia pamoja na fani nyingine kupitia program za ITEC.

Hapo wataalamu wanaweza kuifundisha kompyuta kwa kutumia data ambazo ni taarifa mbalimbali ili iweze kufanya utabiri. Mfano mtaalamu anaweza kuwa na data zinazoonyesha hali ya mvua kwa miaka kadhaa pengine mwaka juzi, jana na sasa ambayo inaonyesha, nyuzi joto, kiasi cha unyenyevu na kiasi cha mvua zilizonyesha kwa kila siku.

Sasa unaweza ukaifundisha kompyuta na data za nyuma, kiasi kwamba ikawa na uwezo wa kutabiri kama mvua itanyesha kwa kiasi gani, sababu imeshaonyesha mifano mingi ya kwamba nyuzi joto ikiwa hivi na unyevu nyevu ukiwa hivi, matokeo ya mvua huwa hivi.

Kwa hiyo kama nyuzi joto na unyevunyevu vina uhusiano na kunyesha au kutonyesha kwa mvua, basi ukipata nyuzi joto ni ngapi, na unyevu nyevu ni kiasi gani, inaweza kutabiri kunyesha au kutonyesha kwa mvua.

Dk. Ntwa anasema hilo linaweza kufanywa kwa sababu kompyuta hiyo imeshaonyeshwa mifano mingi. Mathalani, imefundishwa kwamba nyuzi joto zikiwa hivi na unyevunyevu ukiwa hivi, matokeo ya mvua huwa pengine ya namna hii. Kwa hiyo kama nyuzi joto na unyevunyevu vina uhusiano na kunyesha au kutonyesha mvua, ukipata nyuzi joto ni ngapi na unyevunyevu ni kiasi gani, kompyuta inaweza kutabiri kunyesha au kutonyesha mvua.

**KUIFIKIRISHA KOMPYUTA**

Kompyuta ina 'memory' au uwezo wa kutunza kumbukumbu kubwa zaidi kuliko ubongo wa binadamu kwa hiyo inaweza kufanya vitu vingi sana, vikubwa na kwa muda mfupi, anaeleza Dk. Ntwa.

"Lakini, ukilinganisha intelligence, uwezo wa akili ya binadamu na kompyuta binadamu ana akili nyingi zaidi kuliko kompyuta na ndiye aliyeiunda, lakini hana memory -kumbukumbu kubwa ya kutunza mambo kwenye akili yake. Kompyuta ina uwezo mkubwa wa kushughulikia data kubwa zaidi kwa kiwango cha mabilioni kwa muda mfupi mno hata kwa sekunde," anaeleza.

Mwalimu huyo wa Chuo cha Ardhi, anafafanua zaidi kuwa lengo la AI ni kujaribu kutumia akili za binadamu au 'intelligence' yake na kuiweka kwenye kompyuta ili kurahisisha na kufanyakazi kwa weledi zaidi.

**MATUMIZI YA AI**

Artificial Intelligence inaweza kutumika kwenye maeneo mengi ili mradi data za kuifundisha mashine hiyo kazi na majukumu mbalimbali ziwepo, anasema mtaalamu huyo.

Anakiri kuwa tatizo ambalo linaikabili Tanzania ni upatikanaji wa data kwa ajili ya kuipa au kuifundisha mashine hiyo ili ifundishwe.

Hata hivyo, anasema sayansi hiyo inaweza kutumika katika kufanya uchunguzi wa tiba mfano, saratani. Kinachofanywa ni kuifundisha picha za seli ya kansa zinavyofanana na ikishafunzwa ikionyeshwa picha ngeni inaweza kutambua kama ni kansa au laa.

Anatoa mfano wa pili kuwa ni benki zikitaka kujua kama wanalioko watarejesha ama watakwama wanatumia AI kwa kuifundisha kompyuta data za watu ambao tayari walishawahi kushindwa kulipa na ambao hawajawahi kukimbia mkopo.

Kupitia mafunzo wataitumia kompyuta kujua iwapo mteja anayeweza kulipa au hawezi, kwa hiyo mashine inajua ni vigezo vipi na kwa kiasi gani uwezekano ni mkubwa wa kulipa au kukimbia na mkopo.

Aidha, Dk. Ntwa, anasema AI inaweza kutumiwa na Wizara ya Afya kwa kuwa inazo data za miaka mingi ambazo zimekusanywa kutoka vituo mbalimbali vya afya kuonyesha kiasi cha watu waliopimwa malaria au pengine ugonjwa wowote, na idadi gani waliogundulika na maradhi hayo.

"Kupitia AI wanaweza kutabiri wapi na kipindi gani kutakuwa na mahitaji makubwa ya dawa za malaria. Kwa hiyo kwa kupitia Artificial Intelligence, serikali na taasisi zinaweza kufanya upangaji bora wa rasilimali zilizoko," anaeleza.

Si hivyo tu, inawezekana kutumia AI kwenye sekta ya usafiri, mfano mabasi yaendayo haraka ya UDART, kwa sababu tayari wanazo data nyingi kuhusu muundo na taratibu za wasafiri wanaweza kukadiria idadi ya mabasi yanayohitajika kupeleka abiria kwa mfano, Kivukoni, Gerezani, Kimara na Morocco kwa wakati fulani, tofauti na sasa ambapo mwendokasi imekuwa haina mfumo bora wa kuchukua abiria vituoni, anashauri mhadhiri huyo na kuongeza mifano mingine.

"Tunaweza kuwa na data kuhusu migogoro ya wafugaji na wakulima, na jinsi inavyotokea na tukaweza kujua uwezekano wa mgogoro kutokea pale hali fulani inapokuwapo (labda ukosefu wa mvua au picha za satelaiti zikionyesha ukame). Mifano ni mingi sana.

Hata kwenye mambo ya usalama, mashirika ya usalama yanaweza yakakusanya taarifa kwenye mitandao ya kijamii na kuweza kuzipanga kwenye viwango mbalimbali kufahamu uwezekano wa kutokea vitisho na ikasaidia kwenye kufanya maamuzi ya kiulinzi na usalama," anaongeza kuwa AI ni muhimu sana zama hizi kwa sababu inawezesha kutumia data katika kufanya maamuzi mbalimbali.

ITAENDELEA WIKI IJAYO

## WIKI YA MAJI DAR ES SALAAM

# Waliokosa maji miaka mingi waanza kufaidika



Naibu Meya wa Manispaa ya Ilala, Omar Kumbilamoto, akimtua mama ndoo kichwani baada ya kuzindua mradi wa maji mtaa wa Majengo Vingunguti Jijini Dar es Salaam, utakaohudumia wananchi 1,440 ikiwa ni maadhimisho ya Siku ya Maji Duniani. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

**Na Frank Monyo**

KWA miongo miwili sasa Tanzania, inaadhimisha Wiki ya Maji, mwaka huu, maadhimisho yalianza Jumamosi iliyopita Machi 16 na kuhitimishwa jana kitaifa mkoani Dodoma.

Mwaka huu umekuwa wa neema kwa wateja wengi wa Jiji la Dar es Salaam, wakiwamo wakazi wa Salasala na Kinzudi, ambao hawakuwa na maji miaka mingi, lakini sasa wanapata huduma hiyo.

Ikumbukwe kuwa kauli mbiu ya mwaka huu ni 'Usimwache mtu nyuma katika kupata huduma ya maji.' Ikimaanisha kuwa Watanzania wanaoishi mijini wanafikiwa na huduma hiyo kwa asilimia 95 wakati wa vijijini ni kwa asilimia 85.

Katika wiki hiyo, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Mamlaka ya Majisafi na Majitaka Dar es Salaam (Dawasa), Cyprian Luhemeja, anazungumza na Nipashe na kueleza kuwa mamlaka hiyo imetekeleza miradi iliyofikisha maji kwa wananchi ambao awali walikuwa hawana huduma hiyo.

"Mfano ni eneo la Salasala na Kinzudi ambalo halikuwa na maji, lakini sasa wananchi wanapata huduma baada ya mradi kukamilika. Hii ilihusu ulazaji wa bomba kwa umbali wa kilometa 48 na ujenzi wa tangi kubwa la ujazo wa lita 6,000,000 katika eneo hilo, pamoja na kituo cha kusukuma maji," anaeleza Luhemeja.

Kadhalika, anataja kuwa katika mradi huo zaidi ya wateja 5,400 wa maeneo hayo wameunganishwa kwenye mtandao wa huduma hiyo, huku akitoa wito kwa wananchi ambao wanahitaji kuunganishwa ili kupata maji wajitokeze.

Akizungumzia mradi mwingine ambao sasa wananchi wanapata maji, Luhemeja, anasema ni ule wa eneo la Kiembeni Bagamoyo mkoani Pwani ambalo halikuwa na maji kabla ya mradi huo.

"Baada ya kukamilika, wananchi zaidi ya 2,000 wameunganishwa na kuanza kupata huduma ya maji safi na salama," anaongeza na kufafanua kuwa mradi mwingine ni wa 2D uliofikisha maji Kiluvya, Kibamba, Hondogo, Mloganzila na Kwembe wilayani Ubungo.

"Mradi huu nao umekamilika na wananchi wa maeneo haya wataanza kunufaika na huduma ya maji kwa awamu, kadiri maunganisho yanavyoendelea kufanyika, ambapo hadi sasa takribani wateja 6,500 wanafurahi huduma hii," anaongeza Mtendaji Mkuu wa Dawasco.

Anasema katika kutatua changamoto ya upatikanaji wa huduma hiyo muhimu kwa wakazi wa Kiwalani Bombom na vitongoji vingine, Dawasa imekamilisha mradi wa maji sehemu hiyo.

### KUONANA NA WATEJA

Mwaka huu maadhimisho yalishuhudia kuonana na wateja. Mamlaka ya Majisafi na Majitaka Dar es Salaam, ilifungua dawati maalum kwa ajili ya kuhudumia wateja katika viwanja vya Mnazi Mmoja lililolenga kuwasikiliza na kumaliza kero zao, anaeleza Neli Msuya.

Akizungumza katika viwanja hivyo, wakati wa uzinduzi, Msuya, Mkuu wa Kitengo cha Habari wa Dawasa, anasema mwaka huu maadhimisho yamekwenda pamoja na kuhakikisha kuwa kila idara ya shirika hilo inasikiliza kero na changamoto za wateja na kuzitatua kwa wakati. "Dawasa imefungua dawati maalum kwa wateja ambalo ni la Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (Tehema), Miradi ya Maji na dawati la manispaa zote za Jiji la Dar es Salaam pamoja na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, hivyo, tunawahamasisha wananchi kujitokeza ili tuwahudumie," anasema Msuya.

Anaongeza kuwa katika maadhimisho hayo, ambayo kitaifa yalihitimishwa jana mkoani Dodoma, kama kauli mbiu inavyoeleza , hakuna atakayeachwa katika kuongeza, kasi ya upatikanaji wa huduma ya majisafi na usafi wa mazingira katika dunia inayobadilika kitabia nchi, juhudi nyingi zimefanyikiwa.

Anaeleza, kuwa wananchi watakaofika katika viwanja vya Mnazi Mmoja watapata fursa ya kupata maelezo ya mipango inayoendelea kutekelezwa ili kuboresha sekta na huduma ya maji Dar es Salaam na miji jirani ya mkoa wa Pwani.

### MIRADI IJIONGEZE

Akizindua mradi wa maji Mtaa wa Majengo ulioko Vingunguti utakaohudumia wateja 1,440 kwa siku, Naibu Meya wa Manispaa ya Ilala Omar Kumbilamoto, anapongeza juhudi zinazofanywa na Ofisi ya Mhandisi wa Maji Manispaa ya Ilala uliofanikisha kumalizika kwa kazi ya kuwapa wananchi maji kwa wakati.

Anaeleza kuwa baada ya kukamilika kwa mradi huu ambao ulikuwa unasubiriwa na wananchi kwa muda mrefu, jumuiya ya watumia maji ijiongeze ili kusimamia mradi huu kwa weledi ujiendesha na uweze kuzalisha miradi mingine.

"Tunajua kunakuwa na changamoto hususani kwenye jumuiya za maji kwa kushindwa kusimamia miradi iliyopo kwenye mitaa ila napenda kuwaambia kuwa jumuiya wahusika mjiongeze kwa kusimamia miradi ili ijiendeshe yenyewe na kuzalisha mingine kwa kuwa visima vya watu binafsi vimekuwa na maendeleo kuliko vya serikali," ni kwa sababu ya usimamizi anasema Kumbilamoto.

Aidha, anaziagiza Manispaa kuangalia bei za maji na kuweka utofauti kati ya gharama zinazotozwa na visima vya watu binafsi na vya serikali ili wananchi wengi wapate maji safi na salama.

"Wananchi watunze miundombinu ya maji ili iweze kudumu na wapate maji safi na salama kwa kuwa lengo la serikali ya awamu ya tano kama inavyoainishwa na makamu wa Rais Samia Suluhu ni kumtua mama ndoo kichwani,"anasisitiza Kumbilamoto. Kwa upande wa Kaimu Mkurugenzi wa Manispaa ya Ilala Upendo Lugongo, akizungumzia gharama za mradi huo anasema, kuanzia eneo lililojengwa mradi huo, kuchimba kisima, kujenga vizimba vya kuchotea maji na tangi lenye uwezo wa kuzalisha lita 4,800 kwa siku kwa ajili ya wananchi wa mtaa wa Majengo gharama ya Sh milioni 28, imetumika.

Lugongo aliwaomba wananchi kuendelea kulinda miundombinu pamoja na kutumia maji hayo kwa uangalifu na kwa manufaa ya wote.

Mwenyekiti wa serikali ya mtaa wa Majengo, Chande Msoke, ameishukuru serikali pamoja na kamati ya utendaji ya mtaa kwa kupitisha bajeti iliyofanikisha kumalizika kwa mradi huo ndani ya wakati na kuwa kwa sasa kero ya maji kwenye mtaa wake umemalizika.

Katika kusherehekea Wiki ya Maji iliyoanza Machi 16 na kumalizika Machi 22, miradi mbalimbali ya maji ilizinduliwa ikiwa mikakati ya kuhakikisha kuwa ikifika mwaka 2020 asilimia 95 ya wakazi wa mijini wawe wanapata maji safi na salama na asilimia 85 kwa upande wa vijijini.

## HABARI KIMATAIFA

# Rwanda yakataza raia wake kuwa na uhusiano na Burundi

**KIGALI, Rwanda**

SERIKALI ya Rwanda imewataka wananchi wake walioko karibu na mpaka wa nchi hiyo na Burundi kusitisha biashara yoyote na majirani zao wa Burundi. Haya yanatokea siku chache baada ya Rwanda kuwakataza raia wake kwenda nchini Uganda, ikiwashutumu majirani hao kusaidia makundi ya waasi yanayoipinga serikali.

Wito wa kuwakataza wananchi wa maeneo ya mpaka baina ya Rwanda na Burundi kutokwenda nchini humo, ulitolewa na Ofisa wa Jeshi la Rwanda, Jenerali Mbarac Muganga, wakati wa mkutano wa usalama uliohusisha wananchi na viongozi wa maeneo ya mpakani upande wa kusini mashariki.

Jenerali Muganga aliwataka kusitisha shughuli zote zinazoweza kuwalazimisha kwenda nchini Burundi hata kama itakuwa ni kuoa au kuolewa na mtu kutoka upande wa pili.

"Majirani wale walituchimbia shimo, kila Mnyarwanda anayekwenda huko anatupwa ndani yake, hii ni kwa mujibu wa taarifa za uhakika tulizo nazo. Hatutawashambulia nchini mwao kwa kuwa sisi tunalinda mipaka yetu. Rwanda tunajitosheleza kwa chakula ndiyo maana tunawasihi kutumia kile kidogo tulicho nacho," na kuongeza:

"Kuna wengi pia wanaokwenda kuoa au kuolewa upande wa pili wa mpakani si kwamba tunataka kuvunja ndoa zenu, lakini tunawasihi kusitisha safari za kwenda huko na vilevile kupunguza wageni mnaowapokea kutoka huko kwa sababu wanakuja wakiwa na malengo mengine mengi."

Awali Burundi iliishaitangaza Rwanda kama adui wake mkubwa. Nchi mbili zinashutumiana kuunga mkono makundi ya waasi kutoka kila upande. Miaka mitatu iliyopita Burundi ilitangaza kusitisha biashara yake na Rwanda hasa mboga na matunda na pia kusitisha misafara ya mabasi ya abiria kutoka Rwanda.

Rwanda imekuwa na tahadhari kubwa kwenye mipaka yake kutokana na makundi mbalimbali ya waasi yanayotishia kuishambulia.

Hayo yamejiri wakati ambapo Rwanda iliwakataza wananchi wake kwenda nchini Uganda, nchi iliyokuwa na biashara kubwa na Rwanda. Serikali ilishutumu Uganda kuwanyanyasa wananchi wake wanaokwenda ama kuishi nchini Uganda na pia kusaidia makundi ya waasi wanaotaka kuangusha utawala wa Rais Paul Kagame.

*BBC Swahili*

## EU yaipa Uingereza muda zaidi Brexit

**LONDON, Uingereza**

VIONGOZI wa Umoja wa Ulaya (EU), wakiwa wamechoshwa na hali ya kutokuwa na uamuzi nchini Uingereza kwa shingo upande, jana waliipa nchi hiyo muda zaidi wa kujitoa kutoka umoja huo, mchakato uliopewa jina la Brexit.

Viongozi hao walisema Uingereza inaweza kuahirisha tarehe ya kujitoa ya Machi 29 hadi Mei 22, iwapo bunge la nchi hiyo litaidhinisha makubaliano aliyofikia Waziri Mkuu Theresa May, ya kujitoa kutoka Umoja wa Ulaya.

Rais wa Ufaransa Emmanuel Macron, alisema na kupongeza kuwa viongozi wa EU wamechukua hatua sahihi.

Iwapo makubaliano hayo yaliyokataliwa mara mbili yatatupiliwa mbali tena, Umoja wa Ulaya umesema Uingereza itapewa muda hadi Aprili 12, kuonyesha njia gani inataka kujitoa.

Waziri Mkuu May ambaye alitumia miaka karibu mitatu kuwaambia Waingereza kwamba watajitoa kutoka Umoja wa Ulaya Machi 29, 2019, alionyesha kufurahishwa na hatua hiyo.Viongozi wa umoja huo, walikusanyika jana Ijumaa baada ya uamuzi wao kwamba mzozo wa kisiasa nchini Uingereza kuhusiana na kusitishwa kwa muda mchakato wa Brexit kunatoa kitisho kikubwa katika kundi hilo kubwa la mataifa duniani.

*DW Swahili*

## Mabasi yaungua, yaua abiria zaidi ya 50

**ACCRA, Ghana**

ABIRIA zaidi ya 50 wamefariki dunia katika ajali ya kuungua wakiwa ndani ya mabasi iliyotokea nchini Ghana.

Picha za kutoka eneo la tukio ilipotokea ajali hiyo kwenye mji wa Kitampo uliopo katikati mwa nchi hiyo, zilionyesha kuwa watu zaidi 50 walikufa baada ya mabasi mawili kugongana jana.

"Wengi miongoni mwa abiria waliokuwamo kwenye mabasi yote mawili walikufa hapo hapo. Baadhi ya majeraha walikimbizwa hospitalini," alisema msemaji wa polisi.

Baadhi yao walikwama na kunaswa katika mabasi hayo mawili, polisi ilisema na kuongeza kuwa huduma za zimamoto zilikuwa zimefika eneo la ajali.

*BBC Swahili*



Mabaki ya mabasi yaliyoungua katika Mji wa Kitampo huko Ghana. **PICHA: MTANDAO.**

# Marekani yaweka vikwazo Tume ya Uchaguzi DRC

**WASHINGTON DC, Marekani**

SERIKALI ya Marekani imewawekea vikwazo maofisa watatu wa Tume ya Uchaguzi ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, (DRC) pamoja na wale wa serikali ya aliyekuwa Rais wa taifa hilo Joseph Kabila kwa tuhuma za ufisadi.

Taarifa iliyochapishwa katika mtandao wa Wizara ya Fedha nchini Marekani, inasema kuwa watatu hao walidaiwa kula rushwa ili kuzuia na kuchelewesha maandalizi ya uchaguzi wa haki na uloshirikisha pande zote.

Watatu hao ni Rais wa Tume ya Uchaguzi nchini DRC (CENI) Corneille Yobeluo Nangaa, Naibu wake Norbert Basengezi Katintima na mwanawe Marcellin Basengezi Mukolo ambaye ni mshauri mkuu katika tume hiyo ya uchaguzi.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo iliyosainiwa na Katibu wa Masuala ya Ugaidi na Intelijensia ya Kifedha nchini Marekani, Sigal Mandelker, watuhumiwa hao walifanya vitendo ambavyo vilikandamiza mikakati ya kidemokrasia au taasisi zake nchini DRC.

"Leo idara ya fedha inayosimamia mali ya kigeni OFAC imewawekea vikwazo maofisa watatu wakuu wa tume ya uchaguzi nchini DR Congo CENI kwa kukandamiza demokrasia nchini humo," ilisema taarifa hiyo.

Tume hiyo ya uchaguzi ilisimamia mchakato wa kumchagua rais na wabunge katika matokeo ya uchaguzi huo uliompatia ushindi Rais aliyeko madarakani Felix Tshisekedi uliopingwa na jamii ya kimataifa ikiwamo Marekani pamoja na mpinzani mkuu wa Joseph Kabila katika uchaguzi huo, Martin Fayulu.

Kwa mujibu wa CENI, Felix Tshisekedi alipata kura milioni 7.051 sawa na asilimia 38.57, Martin Fayulu Madidi milioni 6.36 ambayo ni asilimia 34.83, wakati Emmanuel Shadary aliambulia kura milioni 4.35 ambazo ni asilimia 23.84

Waliojitokeza kupiga kura hizo kwa mujibu wa CENI walikuwa asilimia 47.56. Katika taarifa hiyo Marekani ilisema kuwa inaunga mkono hatua ya raia wa DR Congo kujitokeza kwa wingi kushiriki katika uchaguzi huo wa Desemba 30, licha ya kuwa bado ina wasiwasi kuhusu mchakato mzima wa uchaguzi huo na kushutumu tume hiyo ya uchaguzi nchini humo CENI kushindwa kuhakikisha kuwa matokeo ya kura hiyo ni sambamba na matakwa ya raia hao.

Ilisema kuwa Marekani itaendelea kuwasaidia wale walio tayari kukabiliana na ufisadi, lakini haitasita kuwachukulia hatua kali wahusika wanaokandamiza mchakato wa kidemokrasia na kuendeleza ufisadi nchini DRC na duniani kwa jumla.

*BBC Swahili*

# HADITHI

AJALI kubwa iliyotikisa nchi inatokea eneo la Mikese mkoani Morogoro baada ya basi la abiria kuungua moto, kuua na watu wengine kujeruhiwa.
Awali inachukuliwa poa kama ajali za kawaida. Lakini nyuma ya pazia, ni ajali iliyopangwa na muuaji mwenye akili za kiwendawazimu, akibebwa na hisia za chuki, wivu na kisasi bila kujali madhara kwa watu wengine wasiohusika. Eddy Kamal, mpelelezi makini, anategua kitendawili hiki. Fuatilia kisa hiki...

# Kisanduku Cheusi-40

**Na Adam Fungamwango**

**(0716 350534)**




EDDY aliingiza mfukoni na kutoa kitu mfano ya simu ndogo na akawaonyesha. "Hii ndiyo nilikuwa nawarekodia na kila kitu ulichokisema kiko humu, huwezi kukwepa." Alisema hivyo huku akibonyeza kitufe. Maneno ya Mapunda akijitapa, akieleza mpango mzima kuanzia mwanzo hadi mwisho wa kutengeneza mkasa wa mauaji ya Careen na wenzake.

"Nadhani umesikia. Muda mfupi tu baadaye nitawakabidhi polisi ushahidi, pamoja na mtuhumiwa mwenyewe." Alisema huku akizima kitufe.

Kwa mara ya kwanza Mapunda alianza kujiona mjinga. Pia kujilaumu kwa mpango wake huo ambao anauona ulikuwa mzuri, lakini ni kama hauna mwisho mzuri. Hata hivyo, bado aliona anaweza kuokoka.

Alimhusudu askari yule kwa staili yake ya kuuliza maswali ambayo yeye alikuwa akimweleza ili amuue, lakini kumbe alikuwa anakusanya ushahidi.

"Ndiyo maana alionekana akauliza maswali mengi na pia hakuwa na wasiwasi wowote ule kama mtu aliyetekwa." Mapunda alijiambia mwenyewe.

"Mapunda hakuna mtu mjinga kama wewe." Eddy alisema huku akimtolea macho.

"Ulichotakiwa kufanya ni kitu kimoja tu, kumuoa Careen.

Mwenyewe alichokuwa akikitaka ni ndoa. Ukamchezea unavyotaka, huku ukimpumbaza kwa kumpa starehe za kila aina, ukimpeleka anakokutaka, ukimpa anachokipenda. Lakini alipozoea, alijikuta bado hana kile alichokuwa akihitaji. Alihitaji ndoa. Alikuomba mpaka kukulazimisha kuoa, lakini hukuwa tayari. Tayari ulimuona ni kama mateka wako. Hukuwa tayari kwa sababu uliona ni kama utajifunga, kuendelea kutanua na warembo wengine. Ulijua kabisa ukimuoa, basi hautokuwa tena huru." Eddy alikuwa akimpasha Mapunda.

Aliingiza mkono wa kushoto mfukoni na kutoa kitu mfano wa kitufe.

"Mnakiona hiki? Hiki ni kitu kifaa cha kubonyeza ili mabomu yalipuke. Hayo mabomu madogo niliyoyasambaza hapo ili yafyatuke, ni lazima ubonyeze hiki. Sasa mkijifanya kusogea hatua japo moja, nabonyeza na chumba hiki chote kitageuka majivu, haijalishi kama mimi nitakuwa mmoja wa watakaoungulia humu au nitakuwa nimejiokoa." Alitahadharisha huku mkono wa kulia ukiingia mfukoni na kuiweka bastola.

Mkononi sasa hakuna tena bastola, bali kitufe. Alivuta kitu kilichokuwa mbele yake akakaa akiwaangalia mateka wake waliokuwa wamekaa chini umbali wa mita kadhaa kwenye sebule hiyo kubwa.

"Sasa mtoto wa watu alipoona kuwa hapa hakuna ndoa akaona atafute mtu atakayekuwa na mapenzi ya kweli na kumuoa. Akampata Mayambua. Wewe ukasikia. Ukawatisha wote wawili. Lakini mapenzi ni mapenzi, hawakukuelewa, wakaendelea na dhamira yao. Ulichofanya ni kumtuma mtu ampeleleze Careen na kujua ndoa ni lini na ataelekea Ifakara lini.

Ulipojua ukaende kwenye gereji moja kule Mabibo ukatengenezewa bomu ambalo liliwekwa kwenye kisanduku cheusi 'breafcase', kabla ya kumtuma Seif kwa mujibu wa maelezo yako mwenyewe na sauti ninayo hapa, na ukaeleza jinsi alivyofanya mpaka kulipua basi la Bomoa Trans. Mapunda nakwambia wananchi wakitambua hili watashangaa sana kuwa kuna binadamu ambao ni wendawazimu, ambao upande mmoja ni wapole, wanaosaidia jamii wenye kuongoza taasisi kubwa au kufanya biashara kubwa, lakini upande mwingine baadhi yao wana wazimu kama wewe. Umeamua kumuua mtoto wa watu kwa sababu ya hisia zako za mapenzi. Tena mwanamke mwenyewe alikuwa mikononi mwako, ulichokuwa unatakiwa ni kumuoa tu, lakini ukapinga, sasa kosa lake lilikuwa lipi?"

"Ni kweli Mapunda ulifanya kazi kwa ufanisi mkubwa na kila mmoja alidhani kuwa ile ajali ilikuwa ya kawaida tu. Kwa bahati mbaya sana ni mtu mmoja pekee nje ya wasaidizi wako alibaki na siri hiyo. Naye ni Hellen. Na alijua na kubaki nayo kwa sababu ulikuwa umegeuza kibao sasa unataka kumuoa yeye badala yake mdogo wake.

Kwa sababu wamefanana sana, uliona kama hapo ndipo kwa kuponya majeraha yako baada ya kuona umekosea sana. Ni kweli huyu ulitaka kumuoa moja kwa moja na alikubali kwa sababu tu ya kuogopa usalama wake, lakini hakuna mwenye mipango hiyo na wala hakukupenda, tangu ulipomweleza ukweli kuwa ni wewe uliyepanga kumuua pacha wake." Eddy alizidi kumpa mipasho Mapunda ambaye alikuwa akishangaa vitu anavyoelezwa Eddy, kwani vilikuwa na asilimia kubwa ya ukweli.

Ingawa vingine anajua alimweleza yeye mwenyewe kabla ya lengo lake la kutaka kumuua, huku akijua kilichotokea, lakini vingine hakumwambia, hivyo alishangaa alivitoa wapi.

"Kwa sababu bado ulikuwa huna uhakika naye, ukaamua kumfungia mtambo mtoto wa watu ili

**"Ni kweli Mapunda ulifanya kazi kwa ufanisi mkubwa na kila mmoja alidhani kuwa ile ajali ilikuwa ya kawaida tu. Kwa bahati mbaya sana ni mtu mmoja pekee nje ya wasaidizi wako alibaki na siri hiyo. Naye ni Hellen. Na alijua na kubaki nayo kwa sababu ulikuwa umegeuza kibao sasa unataka kumuoa yeye badala yake mdogo wake.**

uwe unapata maneno yote anayoongea.

Na ulifanya hivyo kwa sababu hukutaka kumuua kwa kuwa ulitarajia kumuoa, vinginevyo kwanza usingemwambia, na hata kama angejua kwa mtu mwingine ungemuua mapema na wala usingepata hamu ya kununua mitambo." Eddy alizidi kuuweka ukweli hadharani.

Watu wako walimtumia marehemu Said kumwekea mtambo huo wenye ukubwa wa choroko kwenye pete yake na Hellen ameuawa bila kujua kuwa kwenye pete yake kulikuwa na mtambo wa kurusha sauti kwenda kwako Mapunda.

Mlimtumia Said kwa sababu yeye ndiye mtu wa karibu wa Hellen kwa kuwa alikuwa akimsafisha kucha na kumpaka rangi. Mlimrubuni kwa pesa, mkampa akazifaidi, lakini mwisho wa siku naye mkamuua kwa sababu ya kuficha siri." Edyy alizidi kutiririka.

"Ahadi ya ndoa yako na Hellen ilivunjika kwa sababu kuna siku Hellen alikutana na mtu akamwambia kuwa pacha mwenzake Careen hakufa kifo cha kawaida bali ni cha ajali iliyopangwa na haikuwa mipango ya Mungu. Kwa sababu ulimwekea mtambo maneno yale uliyasikia na yakakutisha sana na kuona Hellen amekiuka maagizo yako kwa kumweleza mtu mwingine siri hiyo. Ingawa alikuwa bado hajaeleza, lakini Hellen alimwambia huyo mtu kuwa wakikutana siku nyingine atamweleza kila kitu, basi ukaamua siku ile ile auawe." Maneno hayo yalianza kumtisha Mapunda kwani mengine hakumwambia Eddy.

"Kingine kilichokuuma mpaka ukamuua Hellen mara moja ni kwamba mtu huyo aliyekuwa akiongea naye walionekana ni kama wapenzi, au wanaotarajia kuwa wapenzi baadaye wakati wewe umeshamwambia kuwa utamuoa na akakwambia umpe muda. Wivu na woga wa siri kutoka ndicho kilichosababisha utume huyo kikaragosi wako amuue mpenzi wangu." AlipOsema neno mpenzi wangu Mapunda alishtuka mno.

"Ndiyo Hellen alitarajia kuwa mpenzi wangu na siku hiyo alipokuwa akiongea maneno hayo alikuwa na mimi hapa." Macho yalimtoka Mapunda. Hakutarajia kitu kama kile. Ni kweli alisikia maneno ya kimapenzi baina ya Hellen na mwanaume mmoja ambaye hakumfahamu kwa sababu mtambo ule ulikuwa ni wa sauti tu na si picha. Lakini leo huyu jamaa ambaye awali alipomteka akidhania kuwa ni Mayambua mchumba wa Careen, baadaye kuja kujulikana kuwa ni askari, lakini cha ajabu kuwa yeye ndiye aliyekuwa na Hallen siku ile na ni mpenzi wake, kichwa kilianza kumvuruga. Alimuona Eddy ni mtu wa ajabu sana kama siyo mzimu.

"Alikutana na Hellen wapi? Nia ilikuwa ni kupeleleza au alimpenda Hellen? Alijiuliza Mapunda.

"Sikiliza Mapunda, mimi nilikutana na Hellen kwa bahati mbaya na nilimpenda na yeye alinipenda, lakini katika mapenzi yetu alinipa picha ambazo zilikuwa za watu waliofanana, lakini mmoja kama alikuwa amenenepa kidogo, akaniambia yule ni pacha mwenzake na alifariki kwenye ajali na akaniambia ilikuwa ya kupangwa hivi.

Kwa sababu mimi ni askari nilitaka kudadisi, lakini akaniambia siku ile ilikuwa ni maalum kwetu na ataniambia siku nyingine, kwa sababu wewe ilisikia maneno yale, usiku mkaja Tabata Kimanga kumuua nilipoondoka. Kwa sababu mimi ni askari tena mpelelezi, nilihisi kifo hiki kina sababu maalum na huenda kinahusiana na maelezo ambayo Hellen alitaka kunipa, nikaingia mzima mzima kupeleleza tukio hilo hadi hivi sasa.

**ITAENDELEA JUMAMOSI**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## VIWANJA/MASHAMBA

**VIWANJA VINAUZWA,** Viwanja vinauzwa chanika mita 100 kutoka stendi mpya ya Chanika umeme upo bei kuanzia 2m vimebaki vichache. Mawasiliano: 0714-187555 au 0755-288879

## NAFASI ZA KAZI


**NAFASI ZA KAZI UALIMU / CERTIFICATE** au diploma / english/mathematics na science 0656490706/0655628640


**NIPASHE NI JIBU LAKO**

NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0767 223311


## CHETI KIMEPOTEA



**Joseph Christopher Mbata** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S.1327/0117/2010** namba ya cheti CS 100074787 kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa mwaka 2010 katika shule ya Sekondari Kleruu.
Yeyote atakayekiona atoe taarifa kwenye kituo cha polisi kilicho karibu.
Taarifa ya polisi: **IR/RB/1875/2019**

215134402

---

**JAMHURI YA MUUNGANGO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455.
Fax: +255 26 2323233.
Barua Pepe: ps@mow.go.TZ.
Tovuti: www.mwtc.go.TZ.

Mtaa wa Moshi
S.L.P 2888,
40470DODOMA
22/03/2019

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya Jumamosi tarehe23-03-2019 kampuni ya **AMANI LOGISTICS LIMITED** itasafirisha Mzigo wake wenye vipimo vikubwa

1. Kutoka **DAR ES SALAAM kuelekea GEITA** kupitia VIGWAZA gari hilo lenye namba za usajili: **T274 AKK/T441 APT**

2. Garihilolinavipimovifuatavyo:

**Urefu - mita 23.00**
**Upana - mita 3.50**
**Kimo - mita 5.20**

Gari zitasafiri muda wa mch*ana tu (kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12.00 jioni)*

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***

215134602

---

**JAMHURI YA MUUNGANGO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455.
Fax: +255 26 2323233.
Barua Pepe: ps@mow.go.TZ.
Tovuti: www.mwtc.go.TZ.

Mtaa wa Moshi
S.L.P 2888,
40470DODOMA
22/03/2019

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya Jumamosi tarehe 23/03/2019 kampuni ya **AMANI LOGISTICS LIMITED** itasafirisha mzigo wake wenye vipimo vikubwa.

1. kutoka M**OROGORO (MAHENGE) kuelekea KILWA (KILANJILANJI)** kupitia MKURANGA.,gari hilo lenye namba za usajili: T274 AKK/T441 APT

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:
**Urefu - mita 23.00**
**Upana - mita 3.50**
**Kimo - mita 5.20**

Gari litasafiri muda wa mchana tu **(kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)**

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***

115134602

---

**JAMHURI YA MUUNGANGO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455.
Fax: +255 26 2323233.
Barua Pepe: ps@mow.go.TZ.
Tovuti: www.mwtc.go.TZ.

Mtaa wa Moshi
S.L.P 2888,
40470DODOMA
22/03/2019

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya Jumamosi tarehe23-03-2019 kampuni ya **MTWARA BALANCE INVESTMENT LIMITED** itasafirisha Mzigo wake wenye vipimo vikubwa.

2. Kutoka **KIMORO (BAGAMOYO)** kuelekea **POLICE STAKISHARI** kupitia TEGETA .,gari hilo zenye namba za usajili: **T607 DGA / T989 BGL**

3. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:
**Urefu - mita 23.00**
**Upana - mita 3.00**
**Kimo - mita 5.00**

Gari itasafiri muda wa mchana tu(kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12.00 jioni)

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***

215135002

---

## KADI YA GARI IMEPOTEA

**RAFIKI FRANCIS SYLVESTER** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari **TOYOTA CALDINA** yenye namba za usajili **T.670 APN** Chassis n.o **ST1910086760, Engine no.356759372** Yeyote atakayeiona atoe taarifa polisi. Taarifa ya polisi: **CD/TR/RB/03741/2019**

115134702

## KADI YA PIKIPIKI IMEPOTEA

**PETER FIDELIS MINJA** anatangaza kupotelewa kwa kadi ya Pikipiki **BOXER BAJAJ** yenye namba za usajili **MC 174 BFG** Chassis No.**MD2A21BZ2GWL93596**, Engine no.PFZINGL99934 Yeyote atakayeiona atoe taarifa polisi. Taarifa ya polisi:**URP/RB/1571/2019**

115133602

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**Anneth Henry Maumbosho** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye usajili wa namba **T792 CCH** aina ya TOYOTA IST, yenye chasis namba **NCP600079878,** engine namba **NZN988700AU.** Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Taarifa Polisi: **KJN/RB/4372/2019**

115134202

## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**LILIAN MSUYA** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki aina ya BOXER yenye namba za usajili **MC 190 ACW.** Chassis namba **MD2A21BZ2EWB81250**. Engine namba **PFZWEA28480.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DOM/TR/RB/1886/2019.**

115133602

---

**IN THE DELIGATE DISTRICT COURT OF DODOMA AT DODOMA**

**PROBATE ADMINISTRATION CAUSE NO.19 OF 2019**

**In the matter of the Estate of the late TIMOTH DAUD SUDA**

**AND**
**In the matter of the Application for letters of Administration by DAVID TIMOTH SUDA**

**GENERAL CITATION**

(Rule 75 of probate rules Gn. 369 of 1963)

All person claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of administration is made to the above named petitioners.

Objections to the grant should be filled on or before 10th/04/2019.

The will if any of the said deceased is deposited and open for inspection of the court.

Dated….19TH /02/2019

DODOMA

215134302

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KUITWA SHAURIN MDAIWA**
**Mahakama ya mwanzo Chamwino**
**Wilaya ya Dodoma Mjini**
**Madai Nambari. 123/2019**
**Mdai: LISIOUSLIGHT FINANCIAL SERVICE CO. LTD**
**DHIDI YA**
**Mdaiwa: MOHAMED AHMED MOHAMED**

**Kwa: MOHAMED AHMED MOHAMED**

Kwa kuwa mdai ameleta madai yake kwamba Madai ya Tsh. 13,820,000 Mkopo

Kwa hiyo unahitajika mahakamani kuhudhuria binafsi katika mahakama hii siku ya Alhamisi 04/04/2019 saa 08:30 asubuhi kwa kujibu madai hayo na kwa kuwa siku ya kukatwa shauri hilo ni lazima kuleta mashaidi wako na hati zote zilizohusu shauri hilo kwa ajili ya kujitetea katika shauri hilo.

**Angalia** kama hukuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu. Mahakama ikidhibitisha kama umepokea kuitwa shaurirni hii, itaweza kutoa hukumu kuwa umeshidwa.

Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya mahakama hii leo tarehe 21/03/2019

115134802

---

**JAMHURI YA MUUNGANGO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455.
Fax: +255 26 2323233.
Barua Pepe: ps@mow.go.TZ.
Tovuti: www.mwtc.go.TZ.

Mtaa wa Moshi
S.L.P 2888,
40470DODOMA
22/03/2019

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwasiku ya Jumatatu tarehe25-03-2019 kampuni ya **M.M CORP LTD** itasafirisha Mzigo wake wenye vipimo vikubwa. Kutoka MKURANGA kuelekea CHALINZE gari hilo zenye namba za usajili: **T898 APY / T933 AFZ**

2. Garihilolinavipimovifuatavyo:

**Urefu - mita 22.00**
**Upana - mita 3.50**
**Kimo - mita 4.80**

3. Njia itakayotumika **Mkuranga hadi Chalinze** Kupitia Vigwaza road. Gari zitasafiri muda wa mchana tu **(kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12.00 jioni)**

***Tunaombaradhikwausumbufuutakaojitokeza.***

115134002

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI FORM II**
**(S.M.M. 1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)**
**Katika Mahakama ya mwanzo MJINI -TANGA**

**Usimamizi wa Mirathi NAMBA 44/2019**

**Ombi la SAID SALUM KHAMIS NA MOHAMED MALIK kuteuliwa**

**Msimamizi wa mirathi marehemu RADHIAH KHAMIS FADHIL**

**Kwa YEYOTE ANAYEHUSIKA**

Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 11/4/2019 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia wa marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa. Tarehe 21/3/2019

2151333902

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**HATI YA KIAPO**

Mimi **RAJABU MAYAPA NAKUDANA** wa S.L.P 178 TANGA, nikiwa mzima na akili zangu timamu ninaapa mbele ya Hakimu/Wakili kama ifuatavyo:-

1. Kwamba, mimi **RAJABU MAYAPA NAKUDANA** ndiye mwapaji katika kiapo hiki.
2. Kwamba, mimi **RAJABU MAYAPA NAKUDANA** ndiye mmiliki halali wa kiwanja Plot Na. 36 BLOCK "CI" Martin shamba,Tanga.
3. Kwamba, hati ya kumiliki kiwanja hicho imepotea na nimefika Polisi nikapewa Loss Report MKR/RAB/245/2019 ya tarehe 14/03/2109.
4. Kwamba kwa kiapo hiki ninaiomba Ofisi ya Ardhi Mipango inipatie hati nyingine kwa jina hilo hilo la **RAJABU MAYAPA NAKUDANA** ili niweze kulipa ada ya serikali.

**UTHIBITISHO:** Ninathibitisha kuwa maelezo yote niliyoyaeleza hapo juu ni ya kweli, kweli tupu, kama nijuavyo kwa sheria ya viapo kwa kutia nguvu kiapo hiki nimefika mbele ya Hakimu/ Wakili na kutia sahihi yangu.

**Imethibitishwa hapa leo tarehe19/03/2019**
**MBELE YA: K.S.KITOGO**
**CHEO: HAKIMU**

215133802

---

**UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**JUDICIARY**
**IN THE HIGH COURT OF TANZANIA AT BUKOBA**
**MISC. LAND APPLICATION NO. 23/2018**

**JONATHAN ALLON LUGAIMUKAMU…………….APPLICANT**

**VERSUS**

**ADBU ABIBU SHABAN**
**RICHARD PAULO NYATANI……………………RESPONDENT**

**TO: RICHARD PAULO NYATANI**
**Karongo Village-Ibwera Ward-BUKOBA RURAL DISTRICT**

**RE: NOTICE OF DATE OF MENTION**

Where as the above mention Applicant lodged a case registered as Misc. Land Application No. 23/2018 against you at the High Court of Tanzania at Bukoba.

Take notice that the above said case has been scheduled for Mention on 9th day of April, 2019 at 9:00 am before Hon. Judge L.M. Mlacha. You are authorized to appear in person or through your Advocate. Take further notice that in default of your appearance on that date and time for the said mention the case may proceed in your absence. Given under my hand and the seal of the Court this 13th day of April, 2019.

115135202


KWA MATANGAZO

MADOGO MADOGO

TUPIGIE

**0767 223311**

**Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku**
**Tupigie 0767 223 311**


TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# GIGGS AJITOSA KUMJIBU IBRAHIMOVIC

**LONDON, England**

**BAADA ya nyota wa zamani wa timu ya taifa ya Sweden anayeichezea Klabu ya LA Galaxy ya Marekani, Zlatan Ibrahimovic, kuwakosoa wachambuzi wa soka ambao ni wachezaji wa zamani, wao wameamua kumjibu.**

**Zlatan aliwashutumu wachezaji wa zamani wa Manchester United, Paul Scholes, Ryan Giggs na Gary Neville kwa vitendo vyao vya kupenda kuwakosoa sana wachezaji wa sasa wa Man United.**

**"Hawachezi tena pale (Man United) wapo kwenye televisheni na wanalalamika muda wote kwa sababu hawapo tena katika timu."**

**"Kama unataka kwenda kufanya kazi katika klabu nenda katafute hiyo kazi, Pogba alikuwa Man United wakati anachipukia, halafu alihama na baadaye akarudi tena katika utawala wa Alex Ferguson hakuwa anapenda hilo ndio maana hawakuwahi kumuhama Ferguson."**

**Kufuatia kauli aliyoitoa Zlatan ambaye pia amewahi kuichezea klabu hiyo, Giggs ameamua kujibu mapigo kwa kutoa kauli kuwa kama Zlatan anaifahamu Man United zaidi yao sawa, lakini wao wamekuwa wakizungumza kama mashabiki wa kawaida.**

**"Sisi ni mashabiki ndivyo mpira ulivyo, kuna watu watakuwa na mawazo tofauti, lakini ni wazi inawezekana anaijua (Man United) zaidi yetu," amesema Giggs.**





# BALE:

## NILIKUWA SHABIKI MKUBWA WA HENRY, BERGKAMP

**MADRID, Hispania**

NYOTA wa klabu ya Real Madrid, Gareth Bale, ameshindwa kuzuia hisia zake na kuweka wazi kuwa alipokuwa mdogo alikuwa akifurahi zaidi kuishabikia timu ya Arsenal inapocheza.

Mshambuliaji huyo wa Real Madrid alikuwa kizazi cha mwisho kuondoka ndani ya klabu ya Tottenham na kuweka historia kubwa katika usajili wa timu hiyo.

Mchezaji huyo mzaliwa wa Cardiff huko Wales amekiri kuwa shabiki mkubwa wa magwiji wa Arsenal, Thierry Henry na Dennis Bergkamp ambao wamemsaidia kukuza kipaji chake kila alipokuwa akiwafuatilia wakati akiwa mdogo.

"Nilikuwa nikiwafuatilia Arsenal, na ukweli nilikuwa ninafurahi zaidi nikimwangalia Thierry Henry," amesema Bale.

"Nilikuwa nikipenda kumtazama pia Dennis Bergkamp, walikuwa na timu bora mashabiki wa Tottenham hawawezi kujiskia furaha kwa hili."

Bale mwenye umri wa miaka 29, amewataja Henry, Bergkamp na Ryan Giggs, huku Gigs kwa sasa akiwa ndiye kocha mkuu wa timu yake ya taifa ya Wales.

Bale amesema kuwa kucheza na Cristiano Ronaldo kwa miaka kadhaa ndani ya Real Madrid ni moja kati ya vitu ambavyo anajivunia. Moja kati ya vitu ambavyo vimekuwa vikizungumzwa ni juu ya mahusiano yake na Cristiano Ronaldo.

Lakini Bale, aliamua kununua pamoja na jezi ya Ronaldo huku akisisitiza kuwa walikuwa na mahusiano mazuri ndani na nje ya uwanja.

"Cristiano ni mchezaji wa ajabu, nilikuwa nafurahia nikicheza naye," amesema Bale.

"Ni dhahiri vyombo vya habari vinajaribu kututengenezea matatizo, jambo ambalo halikuwapo. Tulikuwa vizuri sana, yeye ni mchezaji wa ajabu na kile alichofanya ndani ya klabu Real akiwa na kiasi kikubwa cha mabao aliyofunga. Ni mchezaji wa ajabu na bado anaendeleza."

"Ninakubaliana na kila kitu kutoka Tottenham walichonifanyia, lakini nafikiri walikuwa wanafahamu kuwa kuna klabu kubwa itakuja kunihitaji kama ilivyo kwa Real Madrid."

Akiwa hapo Hispania, Bale amefunga jumla ya mabao 102 akiwa ametoa pasi za mwisho 63 kwenye mechi 224 alizocheza Real Madrid.

# Solskjaer awafukuza Sanchez, Rojo na Valencia

**MANCHESTER, England**

KOCHA wa muda wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer, amewataka wachezaji Alexis Sanchez, beki wa Argentina Marcos Rojo na beki wa kulia wa Ecuado Antonio Valencia kuondoka katika klabu hiyo mwisho wa msimu huu.

Solskjaer ambaye alichukuliwa na klabu hiyo kama zoezi la muda, hivi sasa anaonyesha ni jambo la muda tu kuweza kujichimbia katika nafasi hiyo moja kwa moja.

Solskjaer mwenye umri wa miaka 46 alibainisha hilo wakati alipokutana na mmiliki mwenza wa klabu hiyo, Avram Glazer, mwezi uliopita na Mwenyekiti Mtendaji wa klabu hiyo, Ed Woodward.

Wiki hii, Solskjaer alitoa ishara ya wazi zaidi kwamba ataendelea kuisimamia klabu hiyo msimu ujao pia, akikiri kabisa kwamba bado hajaanza kutazama sehemu nyingine ya kwenda kufanyia kazi.

"Ni wazi kwamba sasa nafanya kazi kama vile nitaendelea kuwa hapa. Ninaifikiria klabu hii mnamo miaka mitano na kumi ijayo," alisema.

Ni katika mazingira haya, Solskjaer amempa kabisa Woodward orodha ya wachezaji anaotegemea kuwa nao msimu ujao, ikiwa ni pamoja na nyota wa Uingereza anayechezea klabu ya Dortmund ya Ujerumani, Jadon Sancho.

Licha ya Dortmund kusema mchezaji huyo atabaki uwanja wa Westfalenstadion, gazeti la Mirror Football limesema United wako radhi kuvunja benki na kulipa fedha yoyote kubwa zaidi ili wampate mchezaji huyo kwa ajili ya Ligi Kuu ya England.



## HABARI MICHEZO



# POGBA AWANUNULIA PETE WACHEZAJI WA UFARANSA

**PARIS, Ufaransa**

NYOTA wa Klabu ya Manchester United Mfaransa, Paul Pogba, ameamua kuwanunuliwa wachezaji wenzake wa Timu ya Taifa ya Ufaransa pete ikiwa kama ishara ya ukumbusho baada ya kutwaa taji la Kombe la Dunia.

Pogba aliwanunulia wachezaji wenzake hao pete hizo wakati wakiwa kwenye mechi za kimataifa za kufuzu kwa michuano ya Euro 2020.

Pogba alisema Antonine Griezmann pia alisaidia katika kubuni pete hizo, ambayo ina alama ya Timu ya Taifa ya Ufaransa na yenye maneno 'Mabingwa wa Dunia.'

Pete hizo pia zina pande tatu zinazovutia za almasi nyeupe, rubi na samafi, kwa mujibu wa gazeti la Daily Mail.

Pete hizo zinajumuisha majina ya wachezaji wote walioshiriki katika michuano ya Kombe la Dunia na upande mwingine zikiwa na jina la 'Mabingwa wa Kombe la Dunia'.

Na upande mwingine kuna orodha ya matokeo yote ya Ufaransa kwenye michuano ya Kombe la Dunia iliyofanyika Urusi katika kipindi cha majira ya joto mwaka jana.

Akizungumza na waandishi wa habari Pogba alisema: "Ni zawadi ndogo baada ya kushinda Kombe la Dunia na wachezaji wenzangu."

Pogba aliongeza kusema kuwa anawahesabu wachezaji wenzake kama familia yake. Ni zawadi ndogo kutoka kwangu."

# PSG yajipanga kumshtaki Evra

**PARIS, Ufaransa**

KLABU ya Paris Saint Germain ya Ufaransa imepanga kumshtaki beki wa zamani wa Manchester United, Patrice Evra, kutokana na kutoa lugha ya kebehi na dharau.


Evra aliwakebehi na kuwaonyesha dharau wachezaji wa PSG baada ya kutolewa na United kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya 16 bora msimu huu.

PSG sasa inapanga kumshtaki mchezaji huyo kutokana na kauli yake hiyo kwa kueleza kwa kejeli kuwa wachezaji wa PSG hawana kiu ya mafanikio, kitu ambacho uongozi wa PSG umekitafsiri kama dharau kubwa na kauli ya kuwavunjia heshima wachezaji wao ambao wamekuwa wakiipambania timu.

United iliitoa PSG katika michuano hiyo licha ya kupoteza mchezo wa kwanza Old Trafford kwa mabao 2-0, na katika mchezo wa marudiano PSG wakapoteza nyumbani kwao magoli 3-1.

Ingawa haijabainika ni lini PSG itamshtaki mchezaji huyo, lakini maandalizi ya wanasheria wake yameshaanza.

Evra aliwahi kuichezea United kwa miaka nane kuanzia mwaka 2006 hadi 2014 na kujiunga na Juventus ya Italia.




# Mourinho amtolea uvivu Scholes

**LONDON, England**

BAADA ya mchezaji wa zamani wa Manchester United ambaye alikuwa kocha wa Oldham FC ya Ligi ya Daraja la Pili England, Paul Scholes, kujiuzulu katika klabu hiyo, Jose Mourinho amemkosoa kwa kejeli na kueleza kuwa ukocha sio kazi ya kuzungumza.

Mourinho ametoa kauli ya kumkosoa Scholes baada ya kudumu na timu hiyo kwa siku 31, huku akimwambia arudi studio kuzungumza.

Scholes kwa muda mrefu amekuwa mchambuzi katika televisheni ya Sky Sports na alichukua nafasi ya ukocha kwa muda mfupi.

"Paul Scholes alikuwa akinikosoa mimi nilipokuwa kocha katika klabu mbalimbali kubwa duniani wakati yeye ameweza kuifundisha klabu kwa siku 31 tu akiwa na Oldham Athletic, arudi tena studio," alisema Mourinho.

Sababu kubwa iliyosababisha Scholes kujiuzulu nafasi yake hiyo ni kutokana na tuhuma za kuingiliwa majukumu na mmiliki wa klabu hiyo, kitu ambacho hakukipenda na kuamua kubwaga manyanga akiwa ana siku 31 tu katika nafasi ya ukocha wa Oldham katika klabu hiyo.



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# SANTO ANUKIA CHELSEA

Pia mkongwe Lampard naye atajwa katika nafasi hiyo ya kumrithi Sarri Stamford Brigde ...

**LONDON, England**

CHELSEA inajipanga kumwajiri Kocha wa Wolves, Nuno Espirito Santo au mchezaji wake mkongwe, Frank Lampard, kuchukua mikoba itakayoachwa na Maurizio Sarri baada ya kuondoka klabuni hapo.

Sarri anatajwa kuwa kocha aliyekalia kuti kavu kwenye Ligi Kuu England baada ya kushindwa kuipa mafanikio Chelsea katika msimu huu unaoelekea ukingoni.

Mtaliano huyo alianza vyema katika klabu hiyo ya Stamford Bridge, lakini anamaliza vibaya msimu kwa kupata matokeo yasiyoridhisha, yakiwamo kichapo cha mabao 6-0 kutoka kwa Manchester City, ambacho kimewafanya kuwa katika wakati mgumu wa kumaliza kwenye nafasi nne za juu maarufu "Top Four".

Gazeti la The Sun, limeandika kuwa mabosi wa klabu hiyo wamekubaliana kwamba Mtaliano huyo hana muda mrefu kwenye timu yao na sasa wanajiandaa kumpata kocha mwingine atakayekabidhiwa majukumu hayo.

Zinedine Zidane alitajwa kuwa kocha namba moja ambaye walihitaji atue klabuni hapo, lakini uamuzi wa Mfaransa huyo kurejea Real Madrid kwa mara ya pili kumewalazimisha kuanza kusaka kocha mwingine.

Espirito Santo anapewa nafasi ya kwanza ya kutua Chelsea baada ya kuipa mafanikio klabu ya Wolves inayoshiriki pia Ligi Kuu England.

Tangu aipandishe timu hiyo daraja kutoka katika Ligi ya Championship msimu uliopita, ameifanya klabu hiyo kuwa kwenye nafasi 10 za juu katika msimamo na vile vile ameifikisha katika hatua ya nusu fainali ya Kombe la FA.

Lampard, ambaye aliitumikia Chelsea mechi 649 na kushinda mataji matatu ya Ligi Kuu England na moja la Ligi ya Mabingwa Ulaya amekuwa na msimu mzuri pia na kuibeba Derby hadi kuifikisha katika mechi ya mtoano.

Katika hatua nyingine, imeelezwa kuwa Roma inajiandaa kumrejesha Italiana Sarri kwa kuchukua mikoba ya kuiongoza timu hiyo licha ya kutangaza kumwajiri Claudio Ranieri.

Kuna taarifa kwamba mashabiki wengi walivutiwa na Mtaliano huyo mwenye umri wa miaka 60 alipokuwa akiiongoza Napoli.

Ranieri alitua Roma wiki mbili zilizopita baada ya kutimuliwa Eusebio Di Francesco, lakini alipewa mkataba wa muda mfupi.

## KWA UFUPI

**UNITED KUMNASA MAGUIRE**
MANCHESTER United inaamini itafanikiwa mchakato wa kumsajili beki wa Timu ya Taifa ya England na Leicester, Harry Maguire (26) kwa dau la pauni milioni 65. ***(Star)***

**LIVERPOOL YAJITOSA SOKONI**
LIVERPOOL imeungana na Bayern Munich pamoja na Borussia Dortmund katika vita ya kuwania saini ya winga wa Chelsea, Callum Hudson-Odoi ambaye ana umri wa miaka 18. ***(Bild - in German)***

**ERIKSEN ANUKIA MADRID**
KIUNGO mchezeshaji wa Tottenham, Christian Eriksen (27), anahusishwa na mipango ya kujiunga klabu ya Real Madrid. ***(Talksport)***

**ALABA AITAKA ARSENAL**
BEKI wa Bayern Munich, David Alaba (26), ameweka wazi kuwa yeye ni shabiki wa Arsenal tangu akiwa kijana mdogo na atafurahi kama ataweza kujiunga na timu hiyo akitokea Allianz Arena. ***(Bild via Daily Mail)***

**ANDERSON ATAJWA MADRID**
WINGA wa West Ham, Felipe Anderson (25), ambaye thamani yake ni pauni 65 ametajwa kuwa ndio chaguo la kwanza la Real Madrid endapo itamkosa mshambuliaji, Eden Hazard kutoka Chelsea. ***(Sky Sports)***

**RONDON ANUKIA EVERTON**
EVERTON inajipanga kumsajili straika wa Venezuela, Salomon Rondon (29), ambaye kwa sasa anaitumikia kwa mkopo klabu ya Newcastle akitokea West Brom. ***(Star)***

**HERRERA ATUA PSG**
PARIS St-Germain imefanikiwa kumsajili kiungo wa Manchester United Mhispania, Ander Herrera (29), ambaye mkataba wake unatarajiwa kumalizika katika kipindi cha majira ya joto. ***(Sun)***

**MILAN YAMWINDA**
AC Milan imeanza mazungumzo na Cagliari kwa ajili ya kumnasa kiungo ambaye anatajwa kuwa na thamani ya juu, Nicolo Barella (22). ***(Sky Italia, via Sempre Milan)***

**HIGUAIN KUREJEA JUVE**
CHELSEA inatarajia kukamilisha mkataba wa mkopo wa straika wa Argentina, Gonzalo Higuain, itakapofika mwishoni mwa msimu huu na hiyo inamaana kwamba nyota huyo atarejea Juventus. ***(Marca)***

**NEYMAR, DYBALA MAMBO MAGUMU**
MCHAKATO wa mshambuliaji wa Paris St-Germain, Neymar (27), kutua Real Madrid unaonekana kuwa na mlolongo mrefu kama ilivyo kwa straika wa Juventus, Paulo Dybala (25) kuelekea Atletico Madrid. ***(Calcio Mercato)***

**CAMARA ANUKIA CITY**
MANCHESTER City imesema ina matumaini ya kunasa saini ya kiungo mchambuliaji chipukizi wa Benfica, Ronaldo Camara ambaye ana umri wa miaka 16. ***(Evening Standard)***

**INTER, EVERTON VITANI**
INTER Milan imesema kuwa iko tayari kupambana na Everton kwa ajili ya kunasa saini ya kiungo wa Barcelona na Timu ya Taifa ya Ureno, Andre Gomes (25) ambaye kwa sasa yuko kwa mkopo Goodison Park. ***(Sport)***



## HABARI MICHEZO

# BOCCO AAHIDI SIMBA KUENDELEZA USHINDI




Bondia Mtanzania, Hassan Mwakinyo (kushoto), akitunishiana misuli na mpinzani wake, Eduardo Gonzalez kutoka Argentina ambaye atapambana naye leo jijini Nairobi, Kenya. **PICHA: SPORTPESA**

**Na Faustine Feliciane**

NAHODHA wa Simba, John Bocco, amesema licha ya jukumu walilonalo la kupeperusha bendera ya Taifa katika mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, kikosi cha timu hiyo hakitaacha "kitu" kwenye michezo yao ya Ligi Kuu Tanzania Bara.

Simba ina viporo saba vya Ligi Kuu Bara ambavyo vimetokana na kuwa na jukumu la michuano ya kimataifa wanayoshiriki na sasa wametinga hatua ya robo fainali.

Akizungumza na gazeti hili, Bocco ambaye yupo katika kikosi cha Timu ya Taifa (Taifa Stars), alisema kuwa bado wanafahamu jukumu la kufanya vema katika Ligi Kuu na wataendelea kupambana ili kushinda mechi zote zilizobakia msimu huu.

"Michezo ya kimataifa tuliyofanya vizuri imetupa molari na hamasa ya kutaka kuona tunatetea ubingwa wetu, hii ndio sababu tunakuwa makini katika michezo yetu ya Ligi Kuu, kila mmoja wetu anataka kuona hatupotezi mchezo wowote ili kujiweka katika mazingira mazuri ya kutetea ubingwa," alisema Bocco.

Kuhusu mchezo wao na TP Mazembe ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC), Bocco alisema wanafahamu timu ni kubwa hapa barani Afrika yenye wachezaji wenye uzoefu wa michuano hiyo.

**"Tunawaheshimu kwa jambo hilo kwa sababu wameshatwaa ubingwa wa michuano hii, la kini na sisi tuna timu nzuri, tuta pambana katika mechi zote mbili ili kuhakikisha tu nasonga mbele," Bocco alisema.**

Mabingwa hao watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara walisonga mbele katika michuano hiyo baada ya kuifunga AS Vita ya DRC na kumaliza katika nafasi ya pili kwenye Kundi D lililoongozwa na Al Ahly ya Simba.

## MSIMAMO LIGI KUU BARA

| | P | W | D | L | F | A | PTS |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1.YANGA | 28 | 21 | 4 | 3 | 45 | 19 | 67 |
| 2.AZAM | 28 | 17 | 8 | 3 | 46 | 18 | 59 |
| 3.SIMBA | 21 | 17 | 3 | 1 | 45 | 7 | 54 |
| 4.LIPULI | 31 | 11 | 11 | 9 | 26 | 26 | 44 |
| 5.KINONDONI MC | 29 | 9 | 14 | 6 | 32 | 20 | 41 |
| 6.MTIBWA SUGAR | 29 | 12 | 5 | 12 | 30 | 23 | 41 |
| 7.TZ PRISONS | 30 | 9 | 11 | 10 | 24 | 25 | 38 |
| 8.COASTAL UNION | 30 | 8 | 14 | 8 | 27 | 30 | 38 |
| 9.MBEYA CITY | 29 | 10 | 7 | 12 | 30 | 32 | 37 |
| 10.ALLIANCE | 30 | 9 | 10 | 11 | 23 | 30 | 37 |
| 11.MWADUI | 31 | 10 | 6 | 15 | 35 | 39 | 36 |
| 12.KAGERA SUGAR | 29 | 8 | 12 | 9 | 23 | 27 | 36 |
| 13.JKT TANZANIA | 31 | 8 | 12 | 11 | 18 | 26 | 36 |
| 14.MBAO | 30 | 9 | 9 | 12 | 19 | 29 | 36 |
| 15.STAND UTD | 31 | 10 | 6 | 15 | 29 | 40 | 36 |
| 16.RUVU SHOOTING | 31 | 8 | 11 | 12 | 27 | 37 | 35 |
| 17.SINGIDA UTD | 30 | 8 | 9 | 13 | 20 | 31 | 33 |
| 18.NDANDA | 28 | 8 | 9 | 11 | 17 | 29 | 33 |
| 19.BIASHARA UTD | 29 | 7 | 9 | 13 | 21 | 29 | 30 |
| 20.AFRICAN LYON | 31 | 4 | 10 | 17 | 19 | 39 | 22 |

# Wabunge wawaita mashabiki Taifa kesho

**Na Renatha Msungu, DODOMA**

MASHABIKI wa soka nchini wametakiwa kujitokeza kwa wingi kwenda kuishangilia Timu ya Taifa 'Taifa Stars' katika mechi yake ya kuwania kufuzu Fainali za Afrika dhidi ya Uganda (Cranes) itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.

Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, anatarajiwa kuwa mgeni rasmi katika mechi hiyo itakayochezeshwa na waamuzi kutoka Gabon ambao ni Eric Arnaud Otogo Castane akisaidiwa na Moussounda Montel na Marlaise Ditsoga Boris.

Akizungumza kwa niaba ya wabunge wenzake, jana jijini hapa, Mwenyekiti wa Bunge SC, William Ngeleja, alisema kuwa anawataka Watanzania kujitokeza kwa wingi kuujaza uwanja ili kuwapa hamasa wachezaji.

"Sisi tukiwa watungaji na wasimamizi wa sheria tupo wabunge 390 na zaidi ya wafanyakazi wa Bunge 200 tukiongozwa na Spika tumewiwa kuitakia Stars ushindi. Kwa niaba ya Spika tunawahakikishia tuna imani na benchi la ufundi, wachezaji na kamati iliyoundwa, shime Watanzania tukiwa kama mchezaji wa 12 twendeni tukaishangilie timu yetu," alisema Ngeleja.

Naye Kocha wa Bunge SC ambaye ni Mbunge wa Kilolo, Venance Mwamoto, aliwataka Watanzania kuvaa jezi za Stars ili kuwapa hamasa wachezaji.



Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Harrison Mwakyembe, akicheza na wanafunzi wa Shule ya Fountain Gate Academy wimbo wa kuhamasisha ushindi wa Timu ya Taifa (Taifa Stars) inayojiandaa kuwavaa Uganda hapo kesho. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Fountain Gate waibeba Stars

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Harrison Mwakyembe, ameelezea kufurahishwa na vipaji vilivyoonyeshwa na wanafunzi wa shule za Fountain Gate Academy kwa kuimba wimbo wa hamasa kwa ajili ya Timu ya Taifa (Taifa Stars).

Wanafunzi hao walionyesha umahiri wa hali ya juu kwa kuimba na kucheza wimbo wa kuhamasisha ushindi kwa Taifa Stars ambayo itaikaribisha Uganda katika mechi ya kuwania kufuzu tiketi ya kucheza fainali za Afrika itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa Taifa.

Waziri Mwakyembe ambaye jana alikuwa ametembelea uwanjani hapo kuangalia maandalizi ya Taifa Stars, alijikuta akiungana na wanafunzi wa shule hizo "kuselebuka" baada ya kuvutiwa na umahiri wao katika kuimba wimbo huo maalumu.

Mkurugenzi wa shule hizo, Japhet Makau, alisema wimbo huo wa kuhamasisha umetungwa na vijana wa shule hiyo kupitia mpango wao wa kuibua vipaji wa Fountain Gate House of Talent.

"Tulifika Uwanja wa Taifa kwa ajili ya kuwapa moyo vijana wetu wa kikosi cha Stars na ndipo Waziri Mwakyembe alivutiwa kuwaona vijana wa Fountain Gate wakiimba wimbo huo kwa umahiri wa hali ya juu," alisema Makau.

# Michezo

Jumamosi Machi 23, 2019

Nipashe


## Santo anukia Chelsea

HABARI UK 30



MAZOEZI...



Wachezaji wa Timu ya Taifa (Taifa Stars) wakifanya mazoezi kujiandaa kuikaribisha Uganda katika mechi ya Kundi L itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam. **PICHA: SOMOE NG'ITU**

# SAMATTA ASEMA HAKUNA 'KUFELI'

## ●●●Ni katika mchezo dhidi ya Uganda utakaochezwa kesho kwenye Uwanja wa Taifa...

**Na Somoe Ng'itu**

NAHODHA wa Timu ya Taifa (Taifa Stars), Mbwana Samatta, amewataka Watanzania kutokuwa na wasiwasi na kikosi chao kuelekea mchezo dhidi ya Uganda (Cranes) utakaofanyika kesho kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam, kuanzia saa 12:00 jioni kwa sababu wamejipanga kutowaangusha.

Taifa Stars inanolewa na Mnigeria, Emmanuel Amunike, inahitaji ushindi wa aina yoyote ili kujihakikishia nafasi ya kufuzu Fainali za Afrika zitakazofanyika Juni mwaka huu nchini Misri.

Akizungumza na gazeti hili jana, Samatta alisema kuwa timu hiyo imejipandaa vema kuwakabili Uganda na kila mchezaji ana morali ya hali ya juu ili kuhakikisha wanaibuka na ushindi katika mchezo huo wa mwisho wa Kundi L.

Samatta alisema kuwa watakuwa makini zaidi katika mechi hiyo ili kuwafanya wageni hao ambao wameshafuzu kutotawala mchezo huo utakaochezeshwa na waamuzi kutoka Gabon.

"Tumepata maandalizi mazuri kuelekea mchezo wetu dhidi ya Uganda, tunaahidi umakini wa hali ya juu kuelekea mchezo dhidi ya Uganda utakaochezwa Jumapili," alisema nahodha huyo ambaye anacheza katika klabu ya KCR Genk ya Ubelgiji.

Naye Mkurugenzi wa Ufundi wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Ammy Ninje, amesema kuwa kikosi cha timu hiyo kimekamilika kutokana na wachezaji wote waliotwa kuwasili.

Ninje alisema kuwa ili Stars iweze kushinda mchezo huo kila mchezaji atakayepata nafasi atatakiwa kutimiza jukumu lake kikamilifu.

"Tuna kikosi kizuri, ila kila mchezaji anatakiwa kufahamu anafanyanini anapokuwa na mpira na vile vile afanye nini pale anapopoteza mpira, hapo tutakuwa kwenye nafasi nzuri, na vile vile kutumia vema nafasi tutakazozitengeneza," alisema Ninje.

Taifa Stars itawakaribisha Uganda ambayo baadhi ya nyota wake akiwamo mshambuliaji, Emmanuel Okwi wa Simba wakiwa na kumbukumbu ya sare ya bila kufungana walipokutana katika mchezo wa kwanza uliochezwa Septemba 9, mwaka jana, kwenye Uwanja wa Mandela (zamani Namboole) jijini Kampala.

Uganda yenye pointi 13 ndio inaongoza kundi hilo ikifuatiwa na Lesotho yenye pointi tano sawa na Taifa Stars, huku Cape Verde yenye pointi nne ambayo leo itakuwa nyumbani inaburuza mkia.

## Alliance waanza kuitisha Yanga

**Na Faustine Feliciane**

WAKATI bado wakiwa katika mbio za kuwania ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Kocha Msaidizi wa Yanga, Noel Mwandila, amesema kuwa wapinzani wao Alliance FC si wa kuwabeza na wanapaswa kujipanga vizuri.

Mwandila alisema kuwa kurejea uwanjani kwa nyota wake Ibrahim Ajibu kutasaidia kuongeza nguvu na kuimarisha mikakati ya kufanya vema katika mechi hiyo ya hatua ya robo fainali ya Kombe la FA itakayochezwa Machi 30 kwenye Uwanja wa CCM, Kirumba jijini Mwanza.

"Hautakuwa mchezo mwepesi, tumeona kwenye mchezo wetu wa ligi ambao tulifanikiwa kupata ushindi, lakini hali ya upinzani ilikuwa kubwa sana... wapinzani wetu ni wazuri sana hasa wanapocheza nyumbani," alisema Mwandila.

Aidha, alisema wanapaswa kuwaheshimu wapinzani wao kama wanataka kupata matokeo mazuri katika mechi hiyo na hatimaye kusonga mbele katika michuano hiyo.

## Mwakinyo atamba kumchapa Gonzalez

**Na Mwandishi Wetu, NAIROBI**

BONDIA nyota wa ngumi za kulipwa nchini, Hassan Mwakinyo, anatarajia kupanda ulingoni kuzichapa na Sergio 'El Tigre' Gonzalez wa Argentina katika pambano la kimataifa litakalofanyika leo kwenye ukumbi wa mikutano wa mikataifa wa Kenyatta jijini hapo.

Mwakinyo ambaye anadhaminiwa na Kampuni ya Michezo wa Kubahatisha ya SportPesa Tanzania, jana alishiriki katika zoezi la kupima uzito lililosimamiwa na Kamisheni ya Ngumi za Kulipwa ya Kenya (KPBC).

Akizungumza na gazeti hili jana baada ya kumaliza kupima uzito, Mwakinyo alitamba kushinda pambano hilo kutokana na maandalizi aliyofanya chini ya kocha wake, Tony Bellew na kudhaminiwa na SportPesa Tanzania.

Mwakinyo alisema kuwa hawezi kuwaangusha Watanzania na wakazi wa Afrika Mashariki na kuahidi kumchapa mpinzani wake kwa staili ya 'knockout' (KO).

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >